**20 JUNI, 2024**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**Kikao cha Hamsini – Tarehe 20 Juni, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni zetu Mheshimiwa Waziri Mkuu ana uwezo wa kutoa Taarifa kabla au bila kuwa na maswali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kutujalia uzima na kutuwezesha kushiriki katika Kikao hiki cha Hamsini cha Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge Tukufu tukiwa na afya njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuungana na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na wewe Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wenzangu na Watanzania wote kutoa pole na salamu za rambirambi kufuatia kuondokewa na Mheshimiwa Dkt. Shogo Mlozi, Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki. Kama mtakumbuka kifo chake kilitokea tarehe 13 Juni, 2024 katika Hospitali ya *Mount Meru* huko Arusha. Mheshimiwa Dkt. Shogo Mlozi atakumbukwa kwa uthubutu, uzalendo na uwakilishi wake ulioheshimisha Taifa letu katika Bunge muhimu la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, niungane na Wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro kutoa salamu za pole kufuatia kifo cha aliyekuwa Katibu Tawala wa Mkoa Bwana Tixon Nzunda kilichotokea tarehe 18 Juni, 2024 kwa ajali ya gari. Marehemu Tixon Nzunda tutamkumbuka kwa utumishi wake ndani ya nchi yetu kupitia nafasi mbalimbali alizowahi kuhudumu ikiwemo nafasi ya Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, Mwenyezi Mungu awapumzishe marehemu wote kwa amani, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari 2023 zimetoa fursa ya uwepo wa maswali ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu kwa siku ya Alhamisi, vilevile Kanuni ya 44(4) imeruhusu Waziri Mkuu kutumia kipindi cha maswali ya papo kwa papo kutoa taarifa au ufafanuzi kuhusu suala lolote linalohusiana na Shughuli za Serikali na lenye maslahi kwa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nimesimama mbele ya Bunge lako Tukufu nikiwa na huzuni kubwa kutokana na matukio ya kikatili yaliyotokea hivi karibuni. Tarehe 31 Mei, 2024 kulitokea tukio la kutekwa kwa mtoto Asimwe Novart mwenye ualbino, mwenye umri wa miaka miwili na nusu mkazi wa Kitongoji cha Mbale, Kijiji cha Mulamula, Kata na Tarafa ya Kamachumu, Wilaya ya Muleba Mkoani Kagera nyumbani kwao Kyeberwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 1 Juni, 2024 Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kagera na Ofisi ya Rais - TAMISEMI walithibitisha kutokea kwa tukio hilo. Mtoto huyo alikuwa na mama yake wakati

alipovamiwa na vijana wawili majira ya saa mbili na robo usiku ambapo mmoja alimkaba koo mama yake ambaye pia alikuwa nje ya nyumba na mwingine aliingia kwa haraka ndani na kumchukua mtoto na kutokomea kusikojulikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 17 Juni, 2024 Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ilipokea taarifa kutoka kwa uongozi wa Mkoa wa Kagera kuhusu kifo cha mtoto huyo ambaye mwili wake ulipatikana ukiwa kwenye mfuko wa *plastic* kando ya kalvati pembeni mwa barabara itokayo Kijiji cha Ruhanga kwenda Kijiji cha Malele Kata ya Ruhanga. Sina shaka nyote mtakubaliana nami kuwa mauji haya yameibua hisia ya maumivu yasiyoelezeka kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, tukio hili linaelekea kufanana na tukio lingine lililotoka tarehe 04 Mei, 2024 ambapo mtoto Julias Kazungu mwenye umri wa miaka kumi mwenye ualbino, mkazi wa Katoro Geita alivamiwa majira ya saa mbili usiku na mtu asiyejulikana ambaye alikuwa ameficha sura yake na kuanza kumkata na mapanga kichwani na mikononi, mtoto huyu alilazwa na sasa anaendelea vizuri na Serikali ya Mkoa inagharamia matibabu ya mtoto huyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhai ni zawadi ya thamani isiyo na kifani lakini kwa masikitiko makubwa zawadi hii imekuwa ikitwaliwa kwa njia za kinyama na za kikatili kwa ndugu zetu wenye ualbino kwa sababu ya imani potofu. Mauaji haya yameacha majonzi yasiyofutika mioyoni mwa Watanzania, yametuacha tukiwa na huzuni isiyopimika na kupoteza nguvu kazi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zilizochukuliwa na Serikali, Serikali imelaani vikali vitendo vya kikatili dhidi ya watu wenye ualbino na kwa kuzingatia nia thabiti ya kukomesha tabia hiyo, Serikali imefanya yafuatayo: -

(i) Uchunguzi ulianza mara baada ya tukio hilo;

(ii) Washukiwa tisa wa tukio la kutekwa na kuuawa mtoto Asimwe wamekamatwa na Jeshi la Polisi*; (Makofi)*

(iii) Jeshi la Polisi Mkoani Kagera linaendelea na upelelezi wa tukio hili; na

(iv) Wataalamu wetu wa ustawi wa jamii wanaendelea kutoa huduma na misaada ya kisaikolojia kwa waathirika kupitia Maafisa Ustawi wa Jamii katika ngazi ya Mkoa wa Kagera na Halmashauri ya Wilaya ya Muleba.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nitumie nafasi hii kuungana na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoa pole kwa wazazi, ndugu, jamaa na Watanzania kwa tukio hilo ambalo limeleta simanzi kubwa kwa Watanzania wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taharuki kubwa iliyotokana na tukio hilo nimeona nitumie kipindi cha leo kwanza kwa kutoa pole, lakini pia kuwakumbusha Watanzania wote wajibu wao katika masuala ya ulinzi wa mtoto na usalama wa jamii nzima kwa ujumla. Vilevile, kutoa taarifa kuhusu hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali katika kuhakikisha kuwa ulinzi na usalama wa makundi mbalimbali likiwemo kundi la watoto na jamii ya watu wenye ulemavu wakiwemo wenye ualbino.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatoa haki ya mtu kuishi na kupata hifadhi ya maisha yake kutoka kwa jamii kwa mujibu wa sheria. Kwa msingi huo watu wenye ualbino na ulemavu wa aina yoyote ile wanalindwa na Katiba ya Nchi. Haki zote zinaoanisha kisheria kwa mujibu wa Katiba kwa Watanzania wote wakiwemo wenye ulemavu wanastahili kuzifurahia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukweli huo ni jambo lisilokubalika kwa Mtanzania au mtu mwingine yoyote kuondoa haki hiyo ya Kikatiba au haki zingine zinazotambuliwa na sheria au haki za kijamii. Kitendo chochote cha aina hiyo na vinavyofanana na hivyo havikubaliki na Serikali haiwezi kufumbia macho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uwepo wa dhana potofu zinazoambatana na ukatili na mauaji ya watu wenye ualbino zikiwemo tamaa za kupata mali nyingi, utajiri, cheo au mafanikio ya aina yoyote ile, naomba kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa dhana hizo ni potofu na hazistahili kufumbiwa macho na jamii zetu na wananchi wote wanawajibika kushiriki kikamilifu katika kuyakemea matendo hayo kwa nguvu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako Tukufu lilitunga Sheria ya Uchawi Sura Namba 12 ya Mwaka 1998 ambayo inabainisha pamoja na mambo mengine kuwa ni kosa la jinai kwa mtu yeyote anayeshauri kuhusu matumizi ya uchawi au vifaa vyovyote vya kichawi. Pia, sheria inabainisha kuwa ni kosa kwa mtu yeyote anayedhamiria kusababisha kifo, ugonjwa, madhara au msiba kwa jamii, mtu au kikundi cha watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya sheria hiyo, Sheria ya Kanuni ya Adhabu *(Penal Code)* Sura ya 16 inaweka bayana kuwa ni kosa kisheria kuteka, kutesa, kusababisha madhara au kuua mtu yeyote. Kwa upande mwingine Sheria ya Mtoto Sura Namba 13 sambamba na katazo la mtoto kufanyiwa ukatili, unyama, vitendo visivyo vya kibinadamu au udhalilishaji unaohusisha matendo ya kimila yanayoondoa utu wa mtu au kuathiri ustawi wa akili au maumbile yake, inatoa wajibu kwa Serikali za Mitaa kulinda na kutetea maslahi ya mtoto ili kuhakikisha analelewa kwenye mazingira stahiki na kwa maadili ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kuwa utendaji wa makosa ya kuteka, kunyanyasa au kuua mtoto, walemavu na watu wenye ualbino hayatokani na ombwe la sheria zetu, makosa haya yanatokana na tamaa ya mtu mmoja mmoja kama nilivyoeleza hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuimarisha mifumo ya kisheria na kitaasisi ili kuhakikisha masuala ya ulinzi na usalama wa makundi mbalimbali katika jamii, kama tunavyofahamu masuala haya ni mtambuka na ufanisi wake unahitaji ushiriki wa wadau wote muhimu zikiwemo Wizara za

Kisekta, sekta binafsi, mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, taasisi za kimataifa na jamii kwa ujumla. Hii inatokana na ukweli kwamba wadau hao wanahusika katika kutekeleza sera, sheria, miongozo, programu na mikakati ili kuimarisha mfumo wa ulinzi na usalama wa makundi mbalimbali katika jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na kuimarisha mifumo hiyo Serikali pia imeendelea kutekeleza matakwa ya itifaki na mikataba ya kikanda na kimataifa inayolenga kuimarisha mfumo wa utoaji haki kutoa huduma kwa makundi mbalimbali pamoja na kutoa elimu kwa jamii kuhusu wajibu wa kila mwananchi katika masuala ya ulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika Serikali imeendelea kutekeleza mpango, mikakati, na hatua mbalimbali mahususi ili kuhakikisha matakwa hayo ya kisheria yanasimamiwa kikamilifu. Hatua hizo zimekuwa zikitekelezwa ili kuhakikisha makundi yote katika jamii yanaishi kwa amani, utulivu na furaha pamoja na kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali kwa ajili ya kudhibiti na kukabiliana na vitendo vya kiukwaji wa sheria ikiwemo kutoa adhabu kali kwa wote wanaobainika kufanya vitendo vya ukatili kwa watoto, watu wenye ualbino, wanawake pamoja na makundi mengine. Katika hatua nyingine Serikali imeendelea kutoa elimu na kushirikisha jamii katika masuala ya ulinzi pamoja na kuweka mifumo thabiti katika ngazi mbalimbali. Baadhi ya hatua hizo ni pamoja na hizi zifuatazo: -

(i) Kumefanyika maboresho ya mifumo ya kisheria ili kuimarisha ulinzi na usalama wa mtoto na kufuata Sheria ya Mtoto Sura Namba 13, Kanuni za Ulinzi wa Mtoto za Mwaka 2015 na Mfumo wa Taifa Jumuishi wa usimamizi wa mashauri ya watoto katika kuwahudumia watoto wanahitaji ulinzi na usalama;

(ii) Kuanzisha mfumo wa taarifa jumuishi wa kitaifa wakushughulikia mashauri ya watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi nchini. Hadi mwezi Aprili, 2024 jumla ya watoto 708,957 wakiwemo wanaume 340,631 na wanawake 368,296 wanaoishi katika mazingira hatarishi wametambuliwa katika halmashauri zote nchini na kupatiwa huduma kulingana na mahitaji yao;

(iii) Kuanzisha kamati za ulinzi wa wanawake na watoto kupitia Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto. Halmashauri zote 184 zimepewa jukumu la kutoa elimu, kulinda na kutoa taarifa kuhusiana ukatili;

(iv) Kuanzisha Kikosi Kazi cha Taifa cha kuzuia ukatili wa watoto mtandaoni pamoja na kuzindua Kampeni ya Kitaifa ya Ulinzi na Usalama wa Mtoto Mtandaoni. Tarehe 10 Februari, 2024 Jijini Dodoma wadau zaidi ya 460 walishiriki. Lengo la kampeni hii ni kuelimisha watoto, wazazi, walezi, walimu, viongozi wa dini, viongozi wa taasisi zisizokuwa za Serikali Wizara za kisekta pamoja na jamii kuhusu kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vya ukatili mtandaoni sambamba na ukatili wa aina nyingine yoyote ile;

(v) Kuanzisha dawati la ulinzi na usalama wa mtoto ndani na nje ya shule, jumla ya madawati 617 katika shule za sekondari na msingi katika mikoa kumi Tanzania Bara yameanzishwa hadi Disemba, 2022. Madawati haya yameundwa sambamba na mabaraza ya watoto 377 katika shule za msingi na sekondari;

(vi) Kuanzisha nyumba salama kwa ajili ya kuhudumia wahanga wa ukatili. Jumla ya nyumba salama 16 katika mikoa tisa Tanzania Bara zimeanzishwa hadi kufikia Aprili, 2024; *(Makofi)*

(vii) Kuanzisha simu ya bure ya msaada namba 116 ambayo hutumika kutoa taarifa za vitendo vya ukatili kwa jamii kuanzia Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 jumla ya simu 240,657 kuhusu ukatili kwa watoto zilipokelewa na kupatiwa huduma; na

(viii) Kutoa elimu ya malezi chanya kwa wazazi, walezi na vikundi vya malezi. Elimu hii ilitolewa kupitia vyombo vya habari vya kitaifa ikiwemo redio jamii, mikutano ya hadhara na kwenye nyumba za ibada. Lengo ni kuwawezesha wazazi, walezi na jamii kuzuia vitendo vya ukatili katika familia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati ya ulinzi kwa wenye ualbino Serikali inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuhakikisha watu wenye ualbino wanalindwa kama ifuatavyo: -

(i) Serikali inaandaa mpango wa kuzuia ukatili dhidi ya watu wenye ualbino kwa kushirikiana na Chama cha Watu wenye Ualbino (*TAS)* na wadau wengine wote na jana tulikuwa na Uongozi wa Kitaifa wa Wenye Ualbino (*TAS)* kujadili masuala mbalimbali yanayohusiana na jamii hii ya wenye ualbino; *(Makofi)*

(ii) Serikali inaandaa kikao cha wakuu wa mikoa wote Tanzania Bara kitakachofanyika tarehe 03 Julai, 2024 kwa lengo la kuweka mikakati ya pamoja ya ulinzi wa watu wenye ualbino; *(Makofi)*

(iii) Kutoa elimu ya ukatili dhidi ya watu wenye ulemavu wakiwemo watu wenye ualbino kupitia Maafisa Ustawi wa Jamii, Maafisa Maendeleo ya Jamii na Maafisa Elimu Maalum kwa mikoa yote hapa nchini;

(iv) Kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2014 na kuandaliwa kwa mkakati wake wa utekelezaji wake wa miaka mitano *(National Five-Year Implementation Strategy 2024/2025 up to 2029/2030)* na mkakati wa ufuatiliaji wa tathmini wa miaka mitano ambao utazinduliwa mwaka ujao wa fedha wa 2024/2025;

(v) Kukamilisha na kuzindua mkakati wa miaka mitatu kutoka mwaka 2024 mpaka 2027 wa upatikanaji wa teknolojia saidizi kwa watu wenye ulemavu wakiwemo

wenye ualbino na mkakati huu umepangwa kuzinduliwa mwezi Julai, 2024;

(vi) Kuandaa na kukamilisha Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Watu Wenye Ulemavu unaoanza mwaka 2024/2025 mpaka mwaka wa fedha 2026/2027;

(vii) Kuendelea na ubainishaji na usajili wa wenye ulemavu ngazi ya kijiji na mtaa kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kanzidata ya watu wenye ulemavu niliozindua siku ya kilele cha Maazimisho ya Kitaifa ya Watu wenye Ulemavu Duniani tarehe 02 Disemba, 2023 hapa Jijini Dodoma; na

(viii) Kuendelea kusimamia kikamilifu utekelezaji wa mwongozo wa ujumuishwaji wa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muktadha uliopo vitendo vya mauaji ya albino vinahusisha mtandao wa watu na siyo mtu mmoja mmoja. Isitoshe kutokana na maelezo yaliyotangulia ni dhahiri kwamba tayari Serikali imeshajenga mifumo thabiti ya udhibiti na suala lililobaki ni upande wa ushiriki wa makundi yote ya jamii katika kuhakikisha vitendo hivyo viovu vinakomeshwa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi kwa kutambua jukumu lililonalo kama Taifa, nitumie nafasi hii kuyataka makundi na taasisi mbalimbali katika jamii kuendelea kushiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya vitendo hivyo vya kikatili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuzuia unyanyasaji na mauaji ya watu wenye Ualbino, Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa zinawajibika katika usimamizi, ulinzi na utoaji wa huduma kwa watu wenye ualbino. Hivyo basi, Wakuu wa Mikoa na Wilaya hakikisheni kila Halmashauri inaanzisha operesheni maalum za ulinzi kwa watu wenye ualbino. Operesheni hizi zihusishe vikosi vya usalama ili kuhakikisha ulinzi wa watu wenye ualbino dhidi ya mashambulizi na vitisho. Mamlaka za Mikoa na Wilaya zihamasishe

uhakiki wa jamii katika kuhakikisha kwamba ulinzi na haki za watu wenye ualbino unazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wajibu wa makundi mbalimbali, wazazi na walezi. Wazazi wanaowajibu kwa watoto wao. Wajibu wa wazazi kwa watoto ni kuwapa malezi bora yatakayowawezesha kuinukia kuwa watu wema katika jamii ambayo wataiweza kuitawala dunia. Malezi hayo yanahusu yale yote anayofanyiwa mtoto tangu akiwa tumboni kwa mama hadi anapofikia umri wa kujitegemea. Wazazi wote wawili yaani baba na mama wanahusika kikamilifu kwa malezi haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali ya wajibu wa wazazi na walezi naomba nitumie fursa hii pia kusisitiza majukumu ya viongozi wa dini kwenye suala la kukemea uonevu unaotendeka kwenye jamii yetu hususani kuua watu wenye ualbino hapa nchini na kuoneshana upotofu wa maadili na kukemea kuonekana upototu wa maadili na kukosa hofu ya Mungu. Vitendo hivi vinapaswa kukemewa kwa nguvu na nitumie nafasi hii kuwaomba viongozi wa dini tuungane pamoja katika kupambana na mauaji haya ya watu wasiokuwa na hatia hata kidogo. Hivyo, niwasihi watumie majukwaa yao ya ibada kuwahubiria waumini wao kuachana na vitendo hivyo vya ukatili ambavyo hata Mwenyezi Mungu anavikataza. Watu wenye ualbino wana haki ya kuishi kama walivyo watu wengine.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waganga wa jadi wanayo nafasi kubwa ya kutoa mchango wao katika mapambano na vita hii ya kuwalinda ndugu zetu wenye ualbino. Hivyo, basi ni wajibu wao kushiriki, kukemea vitendo hivyo vya mauaji na kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kuheshimu na kuthamini maisha ya kila mtu bila kujali hali ya maumbile yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwasisitize waganga wa jadi nchini kote, washiriki kikamilifu katika kampeni ya kupinga mauaji ya watu wenye ualbino. Wakati umefika kwenu nyote kushirikiana na Serikali katika kutokomeza imani potofu zinazochangia mauaji haya. Ninawasihi sana elezeni wazi kwamba hakuna tiba wala mafanikio yanayoweza kupatikana kwa kutumia viungo vya watu

wenye ualbino, badala yake matendo haya yanavunja haki za binadamu na kumomonyoa utu wetu kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Tiba Asili na tiba mbadala lifanye usajili wa waganga wa jadi na vituo vyao sambamba na aina ya huduma wanazotoa kwa wateja wao ili kuweza kudhibiti huduma holela isiyofuata misingi ya utu na haki za binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe wito kwa Chama cha Waganga wa Tiba Asili na Tiba Mbadala Tanzania (CHAWATIATA) kiwakatae na kuwatenga waganga wa jadi wanaotumia njia za imani potofu, ramli chonganishi ikiwemo kutoa masharti ya kufanya mauaji ya watu wenye ualbino ili kufanikisha mahitaji ya wateja wao. Vilevile, toeni taarifa kwa mamlaka husika ili hatua kali za kisheria ziweze kuchukuliwa dhidi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunatambua kuwa viongozi wetu wa kimila wana nafasi kubwa sana katika jamii na wanakuwa nguzo muhimu katika jamii kwa karne nyingi. Viongozi hawa wanaheshimika na kusikilizwa na jamii na wanao uwezo mkubwa wa kuhamasisha na kuongoza mabadiliko. Kwa kutambua nafasi yao pekee, niwasihi viongozi wa kimila Machifu nchini kote kutoka kila kona Tanzania washiriki kikamilifu katika kukemea na kupinga mauaji ya watu wenye ualbino.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaomba viongozi wetu wa kimila wakiwemo Machifu washirikiane na Serikali kutoa taarifa kwa vyombo vya usalama pindi wanapopata fununu na mipango au vitendo vya mauaji ya watu wenye ualbino kwenye maeneo wanamoishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza awali, sote tunao wajibu wa kuwalinda watu wenye ualbino kwa kufichua njama zenye nia ovu na kutoa taarifa pindi tunapozibaini ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa. Vilevile, nitumie fursa hii kuwasisitiza wananchi waache tabia ya kufanya mizaha isiyokuwa na staha hususani kuhusisha matumizi ya viungo vya watu ama kuelezea kwamba viungo vya watu wenye ualbino vinaweza kuwaletea

utajiri. Mizaha kama hii siyo tu inaonesha ukosefu wa heshima kwa watu wenye ualbino na familia zao lakini pia inachochea ubaguzi na unyanyapaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa wito kwa watanzania wote kuheshimu haki za binadamu na kuepuka kutumia lugha au kufanya vitendo ambavyo vinaweza kudhalilisha au kuumiza hisia za wengine. Ni wajibu wetu kama jamii kuhakikisha kuwa kila mtu anaishi katika mazingira salama na yenye heshima bila kujali tofauti zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na matukio ya aina hii ili yasiendelee kutokea, naelekeza Jeshi la Polisi kufanya yafuatayo: -

(i) Kuchukua hatua za haraka pindi wanapopata fununu za uwepo wa njama za utekaji wa mauaji ya watu wenye ualbino.

(ii) Kuendelea kufanya Oparesheni ya kuwakamata wote waliotajwa na watakaotajwa kuhusika kwenye matukio ya aina hii kwa lengo la kuua mtandao mzima wa wahalifu hawa na operesheni hizo ziwe endelevu.

(iii) Polisi Jamii ishirikishwe kikamilifu ili kupata taarifa zote muhimu katika eneo husika na watoa taarifa wote walindwe ipasavyo.

(iv) Kutumia Taarifa za makazi na idadi ya watu wenye ualbino ili kuelekeza nguvu zaidi na ulinzi kwenye maeneo hayo.

(v) Kuendelea kufuatilia na kutumia taarifa fiche zinazopatika kutoka katika vyanzo mbalimbali, hii itasaidia kubaini mipango inayopangwa na wahalifu wakiwemo wanaotafuta wateja wa biashara hizo na kuwabaini na kuwachukulia hatua za kutenda tukio.

(vi) Tuendelee kufanya upelelezi kwa weledi ili kesi zinazopelekwa Mahakamani ziwe na ushaidi wa kutosha.

(vii) Kutumia Polisi Kata ili kuhakikisha maeneo wanayoishi watu wenye ualbino wanatembelewa mara kwa mara ili kupata taarifa zao na kutambua mapema viashiria vyovyote ambavyo ni vya kihalifu na kuwapa elimu kumtambua mtu mwema na mwenye nia ovu na yule mwema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nielekeze Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa tukio hili la Kagera, mara baada ya upelelezi, wale watakaobainika wafikishwe Mahakamani haraka sana ili watuhumiwa waweze kuhukumiwa. Hii itasaidia kutoa fundisho kwa wengine wanaofikiria kufanya hivyo wakijua kuwa mkono wa sheria hautawaacha salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho nimalizie kwa kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kushiriki kikamilifu katika kukemea vitendo vya mauaji ya watu wenye ualbino kupitia Bunge hili Tukufu. Nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu kushiriki katika kuongeza hamasa kuhusu elimu kwa wananchi katika maeneo yenu na kusimamia kikamilifu kuhusu utekelezaji wa mipango ya Serikali kuhusu ulinzi wa jamii ya watu wenye ualbino.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote kwa pamoja Serikali, mashirika ya dini, mashirika yasiyokuwa ya kiserika, taasisi za haki za binadamu na Wtanzania wote kwa ujumla tukae na tutafute njia muafaka itakayotumika kuelimisha jamii ili watu waachane na tabia hiyo ambayo siyo nzuri na inayopoteza maisha ya watu wenye ualbino.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Waheshimiwa Wabunge tunao muda kidogo kwa ajili ya maswali.

Nitatoa swali la kwanza kwa Mheshimiwa Shangazi, kwa hoja hii tu.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na maelezo ambayo umeyatoa ambayo yanaonesha msimamo wa Serikali lakini Ibara ya 15 (1) ya Katiba inatoa uhuru na inasema: "Kila mtu anayo haki ya kuwa huru na kuishi kama mtu huru". Katika maelezo yako umesema kutaandaliwa kambi maalumu ya kuwaweka watu wenye ualbino. Sasa huoni kwamba kuwaweka katika makambi ni kuwanyima haki yao ya kuwa huru?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shangazi, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera yetu ya Serikali ni kuanza kuwalinda hawa wote wenye ulemavu wa aina yoyote ile ili pia na wao waweze kushiriki kwenye maendeleo ya Taifa letu wakiwa salama. Tunaendelea kutafuta njia mbalimbali ambazo zinaweza kuwafanya hawa kuwa salama zaidi, huku tukiimarisha ulinzi wao kwenye vyombo vyote vya ulinzi na usalama, hapa malengo yetu ni kutoa uhakika wa maisha yao wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia hizi mbalimbali tunazozitafuta wakati mwingine tunafikiria kwamba tukiwaweka pamoja wanakuwa salama zaidi, tukiwaweka pamoja tuna tatizo la kisaikolojia la kujiona wao ni walemavu. Tumeanza kufanya marekebisho ya vijana wote wenye ulemavu kote nchini kwamba, badala ya kuwapeleka kwenye shule maalumu ya watoto wenye ulemavu wa aina hiyo, tunajaribu sasa kuwachanganya kwenye shule za msingi na sekondari pamoja ili na wao washiriki pamoja kwenye shughuli mbalimbali za kijamii, michezo wakiwa darasani na kila mmoja kwa ulemavu wake na sasa tumeanza kuona na tunaanza kupata mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunapoelekea kujaribu hili na kuona mafanikio haya pia Serikali imekwishaanza kutoa ruzuku kwa maana kunaongeza kwenye bajeti ya Wizara ya TAMISEMI kwenye kila Halmashauri. Tumewapelekea fedha katika kila Halmashauri ili fedha hii iende kwa wanafunzi walioko shuleni wenye uhitaji maalumu. Kwa mfano, tukiwa na mwanafunzi mwenye uono hafifu, fedha ile itatumika kununua fimbo lakini pia ule mtambo *braille* ya kuandikia na sasa hivi tuna kompyuta. Kwa hiyo, kila Halmashauri inawajibika kununua fimbo na *braille* kwa ajili ya vijana wetu ambao wana uono hafifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wenye ualbino tunanunua *lotion* (mafuta ya kupaka ngozi) na kununua kofia zinazosaidia kuzuia mionzi ya jua. Hili linaendelea kutekelezwa. Vilevile, kwa wale ambao wana tatizo la viungo (hawawezi kutembea) Halmashauri inawajibika kununua baiskeli kupitia fedha ile ili mtoto aweze kutembea, kushiriki na wenzake. Hata kwenye michezo tunaona pia kuna baiskeli za walemavu wanacheza michezo kama *basketball* na *baseball*. Kwa hiyo, tunaendelea kufanya haya tukijaribu kuona ni njia ipi itaweza kufanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge aendelee kutupatia nafasi Serikali tuendelee kufanya tafiti na tathmini ni njia ipi nzuri zaidi inayoweza kuifanya jamii ya wenye ulemavu kushiriki kikamilifu pamoja na jamii husika kwenye shughuli mbalimbali za maendeleo, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa Maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu umekwisha kwa mujibu wa Kanuni. Mheshimiwa Waziri Waziri Mkuu, ahsante. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Tunapongeza hatua hii nzito ambayo Serikali imeichukua. Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali hongera sana. *(Makofi)*

Kipindi cha Maswali tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Omari Shekilindi.

Na. 642

### Malipo ya Mafao kwa Wastaafu kwa Wakati

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI** aliuliza:-

Je, ni lini wazee wanaostaafu watapata mafao yao kwa wakati?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mafao ya pensheni kwa wastaafu yanalipwa kwa mujibu wa Sheria zinazosimamia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambapo zinaelekeza mifuko kulipa mafao ndani ya siku 60 tangu mwanachama anapostaafu. Kwa sasa, mifuko imeboresha mifumo yao na wastaafu wote wanalipwa mafao yao kwa wakati ndani ya siku 60.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shekilindi.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru pia ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri lakini hicho anachokisemaa siku 60 siamini.

Nina swali la kwanza, nini kinachokwamisha, kwa sababu Mheshimiwa Waziri umesema siku 60 ndiyo wanalipwa lakini sivyo ilivyo sasa hivi. Je, ni lini sasa Mheshimiwa Waziri wewe mwenyewe utahakikisha malipo haya kwa wale wananchi wastaafu wanalipwa kwa siku 60?

Swali la pili, ili kuondoa usumbufu huu kwa wastaafu wetu kulipwa mafao hayo. Je, ni lini Serikali itaweka dirisha katika Halmashauri zetu kwa ajili ya kushughulikia wastaafu wetu hawa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Shekilindi, kwanza kwa nini inakuwa saa nyingine wastaafu hawalipwi kwa wakati?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokwishasema kwenye majibu yangu ya msingi, kwamba kwa mujibu wa Sheria ile ya Hifadhi ya Jamii, mtu anapostaafu anatakiwa alipwe mafao yake ndani ya siku 60. Changamoto huwa inakuja pale unapokuta mwajiri hajapeleka ile michango ya wale wastaafu kwa wakati. Kwa hiyo, yule mtumishi anakuwa amekoma utumishi wake lakini sasa anapoanza kufuatilia michango yake anakuta michango ya mwajiri bado haijapelekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, nitumie Bunge lako Tukufu kutoa rai kwa waajiri wote kuhakikisha wanafikisha michango ya watumishi wao kwa wakati katika mifuko ya hifadhi ya jamii ili kuondoa usumbufu pale ambapo mtumishi anakuwa amekoma utumishi wake na anafuatilia mafao yake aweze kuyapata kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye swali la pili kuhusu ni lini Serikali itaweka dirisha katika Halmashauri zetu. Kwa sasa taasisi zetu za *PSSSF* na *NSSF* zinazo ofisi katika kila Mkoa na kila Kanda. Hata hivyo, tunachukua wazo zuri la Mheshimiwa Mbunge la kuweza kuona ni namna gani tutashirikiana na wenzetu wa Ofisi

ya Rais - TAMISEMI la kuwa na ofisi ama dirisha la kutoa taarifa juu ya mafao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa tumeenda kidigitali kwa maana ya mwanachama wa mifuko hii yote miwili ana uwezo wa kuangalia michango yake kupitia mtandao. Anapewa namba yake ya kuweza ku-*log in*, anaingia anaona michango yake na ni kiasi gani ambacho tayari anacho kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Rais, Mheshimiwa Oran Manase.

Na 643

**Mipaka Vijiji vya Kata ya Utengule na Usongwe**

**MHE. ORAN M. NJEZA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itarekebisha mipaka ya Vijiji, Kata ya Utengule na Usongwe ikiwemo Kijiji cha Mbalizi ambacho hakiungani kabisa na Vijiji vingine?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishaji wa maeneo ya utawala katika Mamlaka za Serikali za Mitaa hufanyika kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura 287 na (Mamlaka za Miji) Sura 288 pamoja na Mwongozo wa Uanzishwaji wa Maeneo ya Utawala wa mwaka 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia Sheria hizi na mwongozo uliopo, utaratibu wa uanzishaji au mabadiliko ya mipaka ya vijiji inapaswa kuanza kujadiliwa kwenye Mkutano Mkuu wa Kijiji, Kamati ya Maendeleo ya Kata, Baraza la Madiwani, Kamati ya Ushauri ya Wilaya na Kamati ya Ushauri ya Mkoa ambayo huwasilisha mapendekezo hayo Ofisi ya Rais - TAMISEMI kupitia Katibu Tawala Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema Halmashauri na Mkoa kufuata taratibu hizi na ombi hili liwasilishwe Ofisi ya Rais - TAMISEMI kupitia Katibu Tawala Mkoa kwa hatua zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oran.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali. Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ilikamilisha taratibu zote na taarifa za RCC ninaimani iko katika Ofisi ya TAMISEMI. Sasa kwa vile katika hatua hizo, Kijiji cha Mbalizi ambacho hakipakani na Vijiji vingine vya Kata za Utengule Usongwe, kimezungukwa na Kata za Nsalala ambayo ni tofauti na Kata ya Iwindi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kurekebisha mipaka ya Kijiji cha Mbalizi na kwa vile kina watu zaidi ya 40,000 ili kigawanywe kupata Kata mpya ya Mbalizi, Mtakuja *Pipeline* na Utengule Usongwe?

Swali la pili, kwa vile mwaka huu tuna uchaguzi wa Serikali za Mitaa lakini tuna vitongoji katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ambavyo vina wakazi wengi sana kikiwemo Kitongoji cha Nzunya katika Kata ya Tembela.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuvipandisha hadhi hivi vitongoji ili viendane na sheria za nchi na ziweze kushiriki vizuri katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa uwakilishi mzuri wa wapigakura wake, lakini naomba maswali yake yote mawili niyajibu kwa pamoja:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari Ofisi ya Rais-TAMISEMI imepokea maombi haya na tathmini inaendelea, kwa ajili ya

kubaini uhitaji. Ila sasa, kwa wakati huu kipaumbele cha Serikali ni kuhakikisha na kwa kuzingatia kwamba, pia, Ibara ya 9 (a) (4) ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 kipaumbele cha Serikali kwa wakati huu ni kuhakikisha inaimarisha Serikali za Mitaa, ili ziweze kutimiza wajibu wake. Kwa mantiki hiyo, kwa sasa Serikali inahakikisha kwamba, inaajiri watumishi kwenye maeneo ambayo yana upungufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Serikali inajielekeza zaidi katika kuweka miundombinu muhimu kama vile ofisi, lakini kama vile huduma za afya, shule, miundombinu ya barabara, umeme na maji. Kwa hiyo, naomba nichukue nafasi hii kumuomba Mheshimiwa Mbunge kwamba, waendelee kushirikiana na Serikali kwa maana ya kutizama katika kipaumbele cha kuhakikisha huduma za kijamii na za kiuchumi zinaweza kuwafikia wananchi na wakati ukifika Serikali itafanyia kazi maombi haya ya kuanzisha mamlaka au maeneo mapya ya utawala, lakini kwa wakati huu kipaumbele ni kuhakikisha maeneo ya utawala yaliyopo yanaimarishwa zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Mgogoro wa mpaka kati ya Mkoa wa Singida na Mkoa wa Tabora ni wa muda mrefu sana, lakini uliisha Mwaka 2019. Kilichobaki ni Serikali, kwa maana ya Wizara ya TAMISEMI na Ardhi, kwenda kuweka *beacon* kwenye mpaka ambao ulikubalika. Je, Wizara inasema nini kuhusu hatua hiyo? Kwa nini imechelewa na tunakwenda kwenye uchaguzi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilichukue suala hili. Tutawasiliana na wenzetu wa Wizara ya Ardhi ambao ndio wenye mamlaka kimsingi, ili tuone hatua ambazo zinaweza kuchukuliwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sichalwe.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kwa kuwa, kugawanyika kwa mipaka hii ni mahitaji ya wananchi ambayo yanasababisha wao kupata changamoto. Kwenye Kata ya Chilulumo na Kata ya Mkulwe vinatokea Vijiji vya Sanja, Kaonga pamoja na Chuo ambavyo vinaonekana kwamba, vinapaswa kupata Kata mpya na ni mahitaji makubwa ya wananchi hao na tumeshaanza taratibu kwa ngazi ya chini. Je, kama taarifa hizi zitawafikia au zimekwisha kuwafikia, mnatuhakikishia kwamba, mtatusaidia kupitisha, ili kupata Kata mpya katika vijiji hivyo na viweze kushiriki uchaguzi mwakani, Mwaka 2025?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyotangulia kujibu katika jibu la msingi. Serikali kwa wakati huu inazingatia Ibara ya 9(a)(4) ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 ambayo inataka kuimarishwa kwa Serikali za Mitaa, ili ziweze kutimiza wajibu wao. Kwa hiyo, kama nilivyosema hapo awali, kwa wakati huu kipaumbele cha Serikali ni kuhakikisha inaboresha maeneo ya utawala yaliyopo na siyo kuanzisha maeneo mapya ya utawala, lakini wakati ukifika, Mheshimiwa Mbunge, tathmini itafanywa, ili kubaini uhitaji na uhitaji ukibainika bila shaka maeneo hayo mapya ya utawala yataanzishwa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Yahya Ally Mhata.

Na. 644

**Hitaji la Magari ya Wagonjwa Vituo vya Afya Nanyumbu, Michiga na Mtambaswala**

**MHE. YAHYA A. MHATA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itanunua Magari ya Wagonjwa, kwa ajili ya Vituo vya Afya vya Nanyumbu, Michiga na Mtambaswala?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu imepelekewa magari mawili Novemba 2023, moja la kubeba wagonjwa na jingine la usimamizi shirikishi. Aidha, gari la kubeba wagonjwa lipo Hospitali ya Wilaya na linatumika kufuata wagonjwa wa dharura kwenye Vituo vya afya vya Nanyumbu, Michiga na Mtambaswala.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inakusudia kuongeza gari jingine la kubebea wagonjwa, ili kuwezesha huduma za rufaa za ndani na nje ya Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu. Aidha, Serikali itaendelea kutafuta fedha, kwa ajili ya kununua magari ya kubebea wagonjwa katika Halmashauri zenye upungufu, ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mhata.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina swali moja la nyongeza. Wakati Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipotembelea Wilaya ya Nanyumbu mapema Mwezi wa Tisa, mwaka jana, Waziri mwenye dhamana aliahidi, mbele ya Mheshimiwa Rais, kuipatia Halmashauri hii ya Nayumbu magari matatu muhimu, kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Mtambaswala ambacho kiko kilomita 70 kutoka Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya cha Nanyumbu ambacho kiko kilomita 45 kutoka Makao Makuu ya Wilaya na Kituo cha Afya cha Michiga ambacho kiko kilomita 30 kutoka Makao Makuu ya Wilaya, Mheshimiwa Rais alihakikishiwa na Mheshimiwa Waziri kwamba, magari haya yatapatikana mara baada ya kurudi. Je, ni lini sasa Serikali itatekeleza agizo lake ambalo Mheshimiwa Waziri alilitoa mbele ya Mheshimiwa Rais kwa wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naanza kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa anayoifanya ya uwakilishi kwa wananchi wake, lakini kuhusu swali lake hili la msingi ni kweli, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI alitoa ahadi ya kuongeza gari la kubebea wagonjwa katika Jimbo la Mheshimiwa Mbunge. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge magari kwa wakati huu tayari yameshafika bandarini na kinachoendelea ni taratibu tu za kuyatoa na kufanya usajili, kwa kadiri Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI alivyoahidi. Basi, nakuhakikishia Mheshimiwa Mbunge utapata magari hayo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Samweli.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Waziri wa TAMISEMI alivyotembelea Hanang aliahidi magari mawili na sasa hivi tumepata gari moja tu. Je hilo gari la pili tutalipata lini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge baada ya kipindi hiki cha maswali na majibu tutakaa, ili tuweze kufuatilia ahadi hiyo ni ya lini na tutazame utekelezaji wake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Monni.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kituo cha Afya cha Soya ni cha muda na hakina gari la wagonjwa. Ni lini sasa Serikali itapeleka gari la wagonjwa katika kituo hicho? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu mkubwa sana wa kuwa na magari ya kusafirishia wagonjwa katika vituo vyetu vya kutoa huduma za afya ya msingi imekuwa ikifanya utaratibu wa kununua na kupeleka magari haya. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwa kadiri ya upatikanaji wa haya magari na kwa kuzingatia vipaumbele vya uhitaji, basi gari hili litafikishwa katika jimbo lako, kwa ajili ya kuhudumia kituo ulichokitaja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Almas.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Je, ni lini Serikali itanunua magari, kwa ajili ya vituo vya afya vya Mabama na Upuge?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kadiri ya upatikanaji wa fedha, Serikali itaendelea kuagiza magari haya ya kusafirishia wagonjwa *(ambulance)*, kwa ajili ya kusambaza katika maeneo tofauti-tofauti katika vituo hivi vya kutolea huduma ya afya. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwa kuzingatia vipaumbele na upatikanaji wa fedha Serikali italeta magari haya katika vituo ulivyovitaja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Kamonga.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa, Kituo cha Afya cha Kata ya Makonde ambacho kiko ziwani kinategemewa na kata tano na mawimbi yakitokea ziwani usafiri kwenye maji hauwezekani. Je, ni lini Serikali itapeleka gari, kwa ajili ya kusafirishia wagonjwa wa Kata hizi tano? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikinunua magari haya ya kusafirishia wagonjwa, kwa ajili ya kuyasambaza katika vituo vyetu vya kutolea huduma ya afya ya msingi. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwa kadiri ya fedha zinavyopatikana na magari haya yanavyonunuliwa na kwa kuzingatia vipaumbele, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, ataletewa magari haya, kwa ajili ya kutoa huduma.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Mheshimiwa Jonas Mbunda.

Na. 645

**Ukosefu wa Minara ya Simu Mbinga**

**MHE. JONAS W. MBUNDA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga minara ya simu katika Halmashauri ya Mji wa Mbinga, ili kurahisisha mawasiliano?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Serikali kupitia *UCSAF* inatarajia kufikisha huduma za mawasiliano kwa kupitia mradi wa Tanzania ya Kidijitali *(DTP)* ambapo jimbo la Mbinga Mjini limenufaika kwa kupata minara mitatu. Minara miwili inajengwa na *AIRTEL* katika Kata ya Kitanda ambapo mnara mmoja umejengwa katika kijiji cha Utiri na ujenzi wa mnara wa pili uko katika hatua za mwisho. Vilevile Kampuni ya Simu ya *VODACOM* inatarajia kujenga mnara katika Kijiji cha Ruvuma Chini kilichopo katika Kata ya Mpepai. Baada ya kukamilika kwa minara hii Serikali kupitia *UCSAF* itafanya tathmini ya hali ya mawasiliano katika Halmashauri ya Mji wa Mbinga na kuchukua hatua stahiki kwa maeneo yatakayokuwa hayana mawasiliano.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunda.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza naishukuru Serikali kwa kujenga minara katika Kata ya Kitanda na Kata ya Utiri. Nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza. Nataka nijue ni lini sasa Serikali itakamilisha ujenzi wa Mnara wa Simu katika Kijiji cha Ruvuma Chini, Kata ya Mpepai?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kata za Kikoro na Kagugu zina changamoto kubwa ya mawasiliano. Ni lini Serikali itatenga fedha, kwa ajili ya ujenzi wa minara katika Kata hizo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nakupongeza sana Mheshimiwa Mbunge Mbunda kwa namna unavyoendelea kufanya ufuatiliaji wa minara hii, mawasiliano ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili la Ruvuma Chini mnara huu tunatarajia ukamilike ndani ya wakati wa mkataba na katika kata hizi mbili alizozitaja tayari wataalamu wetu wapo kwenye site wanafanya *survey*. Kufikia Mwezi Disemba maeneo haya uliyoyataja ya Kikoro na Kagugu, Mheshimiwa Mbunda, tunakuja kujenga minara.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mheshimiwa Pondeza, kwa niaba Mheshimiwa Sanga.

Na. 646

**Wanaochukua Mafuta Baada ya Magari Kupata Ajali**

**MHE. FESTO R. SANGA K.n.y. MHE. USSI SALUM PONDEZA** aliuliza:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kwa wananchi wanaochukua mafuta baada ya magari ya kubeba mafuta kupata ajali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Adhabu, Sura ya 16, kama ilivyofanyiwa marejeo Mwaka 2022, Kifungu cha 258 na 265, ni kosa Kisheria kuchukua mali ya mtu mwingine bila idhini ya mwenye mali ama kuwa na dai la haki. Hivyo, kitendo cha kuchukua mafuta baada ya magari ya kubeba mafuta kupata ajali, bila kuruhusiwa na mwenye mali, ni kutenda kosa la wizi. Serikali kupitia Jeshi la Polisi imeendelea kuwachukulia hatua za Kisheria wahalifu wote waliokamatwa kwa kosa hilo na kuwafikisha Mahakamani. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali. Licha ya hatua hizo ambazo Serikali imekuwa ikichukua, lakini matukio haya yamekuwa yakijirudia mara kwa mara na yamekuwa yakileta madhara makubwa. Ni upi mkakati wa Serikali wa kuchukua hatua kali zaidi kwenye matukio ambayo yanasababishwa inapotokea ajali na watu wanachukua mafuta na baadaye yanaleta madhara makubwa kwenye Taifa letu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Festo Sanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ni la Watanzania wote. Naomba nitoe kwa jamii nzima ya Watanzania, Viongozi wa Dini pamoja na wazazi na walezi kuhakikisha kwamba, tunaendelea kutoa elimu kwa familia zetu, ili kuhakikisha kwamba, inapotokea

ajali si jambo jema kukimbilia kwenda kuiba badala ya kwenda kusaidia. Kwa hiyo, natoa wito kwa jamii nzima tushirikiane kuhakikisha kwamba, jambo hili linakomeshwa mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nakuhakikishia Serikali itaendelea kuchukua hatua kali kwa wale wote ambao wanaiba mafuta haya inapotokea ajali. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Ujenzi. Mheshimiwa Stella Manyanya.

Na. 647

**Kukabidhi Majengo ya Mshauri wa Ujenzi kwa Halmashauri ya Nyasa**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakabidhi majengo yaliyotumiwa na Mshauri wa Ujenzi wa Barabara ya Mbinga hadi *Mbamba Bay* kwa Halmashauri ya Nyasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, majengo ya kambi yaliyokuwa yanatumiwa na mhandisi mshauri wa ujenzi wa Barabara ya Mbinga – *Mbamba Bay* yenye urefu wa kilomita 67 yalirudishwa Wizara ya Ujenzi mnamo Tarehe 13 Aprili, 2023. Kwa sasa majengo hayo yanatumika kama nyumba za watumishi, wauguzi na madaktari, wa Hospitali ya Wilaya ya Nyasa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stella.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na shukrani nyingi kwa majengo haya kupelekwa kwenye Hospitali ya Wilaya ya Nyasa, lakini bado kuna jengo moja ambalo ndio kubwa lilikuwa linatumika, kwa ajili ya

masuala ya kiofisi na utawala, wakati huo halikukabidhiwa kwa misingi kwamba, kuna vifaa vimefungiwa humo siku zote hizo bado halijakabidhiwa. Nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba, inarudisha jengo hilo katika Halmashauri ya Nyasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili. Barabara hiyo baada ya kujengwa bado ina changamoto ndogondogo ikiwemo kufyeka nyasi, ili kuhakikisha kwamba, inakuwa inadumu inavyotakiwa. Nini mpango wa Serikali kuvitumia vikundi vidogovidogo, ili kufyeka nyasi katika barabara hiyo kutoka Mbinga mpaka *Mbamba bay*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nashukuru kwa Mheshimiwa Mbunge kuipongeza Serikali kwa kukabidhi hayo majengo kwa Halmashauri. Kuhusu hilo jengo, sisi kama Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Mbunge atambue tu kwamba, mali zote na hayo majengo, zinakuwa baada ya sisi kutumia tunarudisha Wizara ya Fedha. Basi namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, ombi lake limepokelewa na, sisi kama Serikali, tutakaa na wenzetu wa fedha, ili waone namna bora ya kuhakikisha kwamba, hilo jengo wanalikabidhi kwa Halmashauri ya Wilaya, ili liweze kutumika kama Mheshimiwa Mbunge ambavyo anaomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kufyeka nyasi; tuna utaratibu ambao Mameneja wote wa Mikoa huwa wanasimamia barabara na kwa sasa tutatumia vikundi ambavyo ni *labor based* kusafisha hizo barabara. Namuagiza Meneja wa wa *TANROADS* wa Mkoa wa Ruvuma kuhakikisha kwamba, barabara hiyo inawekewa watu ambao wanaisafisha, kwanza kuifanya idumu, lakini pia, kuimarisha usalama wa watumiaji wa barabara hiyo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Paresso.

Na. 648

**Ujenzi wa Barabara ya Karatu – Mang'ola – Matala Hadi Lalago**

**MHE. CECILIA D. PARESSO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya kutoka Karatu – Mang'ola – Matala hadi Lalago kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Karatu – Mang'ola – Matala – Lalago yenye urefu wa kilomita 229 umekamilika. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha, kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Karatu – Mang'ola – Matala hadi Sibiti yenye urefu wa kilomita 156. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, ahadi ya ujenzi wa Barabara hii kwa kiwango cha lami ni ya muda mrefu sana na maneno haya ya upembuzi yakinifu tumeyasikia muda mrefu bila matokeo. Je, kwa nini sasa Serikali isifikirie kuanza tu angalau eneo ambalo linatumika sana la Karatu – Mang'ola lenye urefu wa kilomita takribani 54 kwa kiwango cha lami kwanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hii Barabara ya Karatu – Kilimapunda hadi Mbulu, nafahamu mlishasaini mikataba na wakandarasi na ilikuwa ujenzi wa kiwango cha lami uanze katika mwaka huu wa fedha, lakini mpaka leo hakuna kilichoanza. Ni lini

barabara hii nayo itaanza kwa kiwango cha lami kwa sababu, barabara hii inaunganisha Mkoa wa Manyara na Arusha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba usanifu wa barabara hii ya Karatu – Mang'ola umeshakamilika, tunachofanya ni kutafuta fedha kuijenga. Pia, sisi kama Serikali tunajua kwamba eneo muhimu sana ni Karatu hadi Mang'ola na tumekuwa tukijibu kwamba Serikali inatafuta fedha hizo lakini pia Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kulikuwa na daraja ambalo lilikuwa linasumbua sana Kona ya 'S' ambapo tuliona ilikuwa inakwamisha magari mengi. Sasa hivi tunaijenga ili tuhakikishe kwamba *at least* kwa mwaka mzima barabara hii inapitika hadi eneo la Mang'ola.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Barabara ya Karatu - Kilimapunda kwenda Mbulu tayari tushasaini mikataba; tuko kwenye hatua za mwisho za manunuzi kuona lini mkandarasi ataanza na utaratibu ambao kama alivyosema anaufahamu ni *EPC+F* ambapo tuko kwenye hatua za mwisho za kuongea na hawa wakandarasi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aysharose.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa barabara inayoanzia Kwa Mtoro - Singida hadi Handeni mkataba wake umeshasainiwa toka mwezi Juni 2023, ili kuanza kujengwa kwa kiwango cha lami. Napenda kujua, je ni lini Serikali itaanza kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu swali la awali la Mheshimiwa Paresso, barabara hii pia zile barabara ambazo ziko kwenye utaratibu wa *EPC*. Kwa hiyo, utaratibu wake unafanana na kuanza kwake kwa ujenzi ni kama tulivyoeleza kwenye bajeti wakati tunasoma bajeti yetu ya Wizara, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Flatei.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa kuwa Barabara ya Haydom tumeshasaini mkataba na wewe ulikuwepo. Je, lini mnampelekea mkandarasi aliyeko *site* fedha ya kujenga kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, Wizara ilishapeleka maombi ya mkandarasi Wizara ya Fedha na wenzetu sasa hivi wako kwenye maandalizi ya kuandaa fedha hizo ili mkandarasi aweze kulipwa na aendelee na ujenzi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, Barabara ya Mafinga – Mgololo ni barabara ya kiuchumi. Mkataba tayari ulishasainiwa toka mwaka jana, je, ni lini sasa ujenzi utaanza? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, Barabara ya Mafinga – Mgololo ina kilometa 81, ni kati ya hizi barabara saba ambazo zinatekelezwa kwa utaratibu wa *EPC+F*. Kwa hiyo, utaratibu ni kama barabara nyingine nilizotaja, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gambo.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Tanzania inakwenda kujenga uwanja mkubwa wa *AFCON* na tunahitaji miundombinu ya barabara kuelekea kwenye eneo la uwanja. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara ya njia nne ya kutoka Arusha *Airport* mpaka Kilombero ili kuwarahisishia wananchi kwenda uwanjani kwenye Mashindano ya *AFCON*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ni kweli, na hili suala wenzetu wa Wizara ya Michezo wamekuwa wanalifuatilia kuhakikisha kwamba tunaanza ujenzi wa barabara hiyo, kwa sababu taratibu nyingine za usanifu zimeshakamilika. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inalifahamu hilo na inalichukulia kwa uzito mkubwa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Jesca.

Na. 649

**Kuwahusisha Vijana Waliomaliza JKT na *Block Farming***

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU** aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje kuwahusisha vijana waliomaliza mafunzo ya JKT waliopo katika vikosi na waliohitimu katika Mpango wa *Block Farming*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, udahili wa vijana wa *BBT* unahusisha vijana kati ya miaka 18 hadi 40, katika awamu ya kwanza vijana 120 walioshiriki mafunzo ya JKT walikuwa miongoni mwa vijana 812 wanufaika wa Programu ya *BBT*. Pia, kutokana na

umuhimu wa Mafunzo ya JKT, vijana wote wa *BBT* ambao awali hawakuwa wameshiriki mafunzo ya JKT, wamepata mafunzo hayo kwa kipindi cha miezi miwili kwa lengo la kuwajengea ukakamavu na uzalendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu huo wa kuwa na vijana wenye uzalendo, tarehe 8 Agosti, 2023 Wizara ya Kilimo iliingia makubaliano *(MOU)* na JKT, ambapo JKT watatoa si chini ya 30% ya vijana watakaodahiliwa na 70% watatoka katika nafasi zitakazotangazwa. Hivyo, awamu zinazofuata udahili wa vijana katika Programu ya *BBT* utazingatia makubaliano hayo. Aidha, kwa wale waliokwishaanza wenyewe na kuwa na changamoto ya mikopo, tunawahimiza kuwasiliana na Mfuko wa Pembejeo ambao hutoa mikopo hiyo, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, naomba ufafanuzi zaidi kwenye jibu lako, hapo ulipoanzia; "Aidha, kwa wale waliokwishaanza wenyewe na kuwa na changamoto ya mikopo tunahimiza wawasiliane na Mfuko wa Pembejeo." Sijaelewa *connection* yake na swali langu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ni kwa nini Serikali kupitia Wizara ya Kilimo isione umuhimu kwamba wale vijana wanaopata mafunzo ya *BBT* wawe wanafundishwa na wanakuwa *attached* kule walikotoka kwenye halmashauri zao ili waweze kueneza ule ujuzi kwenye halmashauri badala ya kuwabeba na kuwapeleka kwenye *block farming*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba kujibu

maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jesca, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana kwa kufuatilia mpango huu wa kujenga kesho iliyobora kwa vijana katika sekta ya kilimo. Katika *BBT* kuna maeneo manne ambayo Serikali inayafanyia kazi. Moja, ni hayo ya *block farming* ambalo liliulizwa kwa maana ya mashamba makubwa; sehemu ya pili ya *financing* kwa maana ya mikopo kwa wale ambao wanakuwa wamepata mafunzo hayo; sehemu ya tatu ni ya ugani ambayo nayo pia tunaiangalia; na sehemu ya nne ni ya kuhakikisha maji yanapatikana kwenye mashamba hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuhusiana na ufafanu wa eneo la kwanza ni kwamba kulingana na swali lake kwamba tumefanya makubaliano na JKT, lakini kuna vijana wengine ambao walipita JKT hawatakuwa kwenye huu mpango. Kwa hiyo, tunasema wale ambao watakuwa wamepita *BBT* lakini hawapo kwenye huu mpango ambao tumekubaliana *MOU* na JKT maana yake na wao tunachukulia wameshapata ujuzi. Sasa kwa sababu kwenye mpango huu hawa watapata fedha kwa maana ya ukopeshwaji watakapokuwa wamepita kwenye *block farming* hizi, sasa wale ambao hawako kwenye utaratibu huu maana yake tunawashauri wapate *financing* kupitia Mfuko huu wa Pembejeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na sehemu ya pili, kama nilivyosema ni kwamba tayari tunawaandaa vijana kulima kisasa kwenye mashamba haya ya *block farming*. Wengine ambao watapenda kwenda zaidi ni wale ambao watapata mafunzo ya ziada ya ugani na hawa tutawaelekeza warudi kwenye maeneo waliyotoka kwa wakulima. Pia, hata wale wengine ambao wanaweza kuwa hawajapata mafunzo haya mahususi ya ugani pia tunachukua wazo hili kwamba nao wakipata nafasi sasa badala ya kukaa kwenye mashamba haya ya *block farms* kubwa wanaweza wakarudi wakashirikiana na wakulima kule vijijini walikotoka ili kueneza ule ujuzi walioupata kuwasaidia wakulima wengine, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Ameir Abdallah Ameir.

Na. 650

**Kutumia TEHAMA Kuboresha Kilimo Nchini**

**MHE. ABDUL YUSUF MAALIM K.n.y. MHE. AMEIR ABDALLAH AMEIR** aliuliza:-

Je, ni kwa kiwango gani TEHAMA inatumika kuboresha sekta ya kilimo nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya TEHAMA katika sekta ya kilimo ni mojawapo ya njia muhimu za kuboresha uzalishaji, ufanisi na tija kwa wakulima. Matumizi ya mifumo hiyo yamesaidia kufanya usajili wa taarifa za wakulima na kutumia taarifa na takwimu hizo kutoa huduma nyingine, mathalan utoaji wa mbolea kwa mpango wa ruzuku, kutoa huduma za ugani kupitia Kituo cha Huduma kwa Wateja cha Wizara *(Kilimo Call Centre)* na *Mobile* Kilimo, ambapo wakulima wanapata ushauri wa kitaalamu kwa kujibiwa maswali yao na hivyo kutatua changamoto zinazowakabili na kuboresha uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile TEHAMA imesaidia katika utoaji wa vibali mbalimbali vikiwemo vibali vya kuingiza na kusafirisha mazao na bidhaa za kilimo ndani na nje ya nchi na kufanya malipo kwa wakati lakini imewezesha wakulima kupata taarifa za masoko kwa urahisi na hivyo kuwawezesha kuuza mazao yao kulingana na bei ya soko. Pia, kuwawezesha wakulima kupata taarifa za hali ya hewa kwa wakati, ambazo ni muhimu sana katika kupanga shughuli za kilimo kama vile upandaji na uvunaji, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Ameir.

**MHE. ABDUL YUSUF MAALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa kiasi gani *TARI* (Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania Bara) na *ZARI* (Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar) zinashirikiana katika kutatua changamoto za kilimo kwa pamoja kupitia TEHAMA? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ni tafiti za aina gani mpaka sasa zimefanyika katika teknolojia ya habari na mawasiliano ili kutoa matokeo chanya? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA KILIMO**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nijibu maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia kuhusiana na matumizi ya TEHAMA na hasa ushirikiano wa taasisi zetu za utafiti kwenye kilimo kwa maana ya *TARI* kwa upande wa Tanzania Bara na *ZARI* kwa upande wa Zanzibar. Taasisi zetu, ikiwemo hizi zimekuwa zikishirikiana sana katika maeneo mbalimbali katika utafiti, kupeana na kujengana uwezo kati ya wataalamu kutoka *ZARI* na *TARI*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu maswali hayo kwa pamoja, hivi karibuni mwaka 2022 taasisi hizi zilifanya tafiti kwa ushirikiano katika mazao ya mihogo na mpunga ambapo moja kupitia Wakala wa Kimataifa wa Atomiki waone namna gani tunaweza kupunguza athari ya maradhi ya mihogo kwa maana ya michirizi kahawia ambayo inaathiri sana zao la muhogo ambalo linalimwa Tanzania Bara lakini pia na kule Visiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia katika mpunga (mchele) ambapo wameweza kufanya utafiti ili kuona namna gani ya kuongeza uzalishaji wa mpunga (mchele) ambao unalimwa kati ya Tanzania Bara na kule Visiwani ili kupunguza baadhi ya athari au kuboresha mavuno yanayotoka katika maeneo haya ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo moja, tunashirikiana sana kama Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa taasisi zote kama nilivyosema *TARI* na *ZARI*. Pili, tafiti zote ambazo zinatumia TEHEMA zimefanyika kwa kushirikiana na tutaendelea kuboresha ushirikiano huu kadiri muda unavyoendelea, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malembeka.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilitaka niulize swali kuhusiana na hiyohiyo TEHAMA, katika Halmashauri ya Masasi hususan katika Jimbo la Lulindi kuna maeneo mengi ambayo wakulima wanapata tofauti. Mtu ana ekari 100 lakini ukienda kwenye kompyuta anaonekana hana shamba na mwingine hana shamba lakini ukifika kwenye kompyuta anaonekana ana ekari labda 50. Je, ni lini Serikali itahakiki upya maeneo hayo ili kila mmoja ajue umiliki wake? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** nakushukuru sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia taarifa hizi ambazo wakati mwingine kweli kutokana na changamoto za kiteknolojia kuna wakati inawezekana kweli taarifa za mtu mmoja zinahamia kwa mtu mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tumeanza kuboresha TEHAMA kwenye sekta ya kilimo na maeneo mengine. Changamoto hizi ndogondogo tunaendelea kuzifanyia kazi na

tuendelee kupewa taarifa na nitaonana naye baada ya hapa ili aweze kutupa taarifa mahususi ili wataalamu wetu waweze kufuatilia na kuweza kurekebisha changamoto hiyo, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Nataka tu niwaombe Watu wa Lindi, Pwani, Ruvuma na Mtwara, changamoto iliyojitokeza kama wiki moja iliyopita kwenye Mfumo wa Ugawaji wa Ruzuku ya Pembejeo. Tumeshawaagiza watu wa *eGA* wana-*update* na kuzi-*retrieve data* za mwaka jana na watagawiwa wakulima kutokana na *data base* ya mwaka jana na *update* iliyofanyika mwaka huu itaendelea kufanyiwa *cleaning. (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa maswali yamekwisha. Wageni waliokuwepo Bungeni asubuhi hii; wageni waliokaa Jukwaa la Spika, wageni wa Mheshimiwa Naibu Spika kutoka *Royal Golf Magazine*: Ndugu Amani Hamisi Rajabu - Mkuu wa Utawala, Mauzo na Masoko; Ndugu Mbonile Mwamasangula - Mwasisi wa Jarida la *Royal Golf Magazine*; na Ndugu David Eliya Mwaibanje, Mkurugenzi Mwendeshaji. Wageni hawa vilevile wanashirikiana na Mheshimiwa Abdallah Chikota, Mbunge wetu kutoka Kusini. *(Makofi)*

Pia wapo wageni 15 wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Viongozi wa Chama cha Watu wenye Ualbino Taifa na Viongozi wa Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu: yupo Ndugu Godson Mollel, Mwenyekiti wa Chama cha Watu Wenye Ualbino Taifa; Ndugu Alfred Kapole, Makamu Mwenyekiti; Ndugu Abdillah Omary, Kaimu Katibu Mkuu; Ndugu Saleh Alex, Afisa Programu; Ndugu Lodovic Julius, Mwenyekiti Mkoa wa Dodoma; Ndugu Hadson Sema, Katibu Mkoa wa Dodoma; Ndugu Ignas Rugemalira, Katibu wa Mkoa Kagera; Ndugu Magreth Swai, Mwanachama; na Ndugu Maiko Salali Mwanachama. *(Makofi)*

Pia wapo Ndugu Sabra Nassoro Mbarouk, Mwenyekiti wa Wanawake Zanzibar *Blind Association*; Ndugu Adil Mohamed,

Mratibu wa Zanzibar *Blind Association;* Ndugu Mkongwe Zaidi, Msaidizi wa Zanzibar *Blind Association*; Ndugu Jamila Salum Mbaruku, Msaidizi wa Zanzibar *Blind Association*; Ndugu Kilumba Wakulichombe, Mhazini wa SHIVYAWATA; Ndugu Festo Fute, Kaimu Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu; na Ndugu Rasheed H. Maftah, Mkurugenzi Kitengo cha Watu wenye Ulemavu, Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Pia, wapo wageni wa Waheshimiwa Wabunge: wageni 66 wa Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji: Wenyeviti na Makatibu wa CCM wa Matawi yote ya Jimbo la Ubungo, karibuni. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, Mpiga kura wake kutoka Liwale Mkoa wa Lindi. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Ally Makoa, mpiga kura wake kutoka Jimbo la Kondoa Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Viongozi wa CCM Kata ya Ruzinga kutoka Missenyi Mkoa wa Kagera. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, rafiki zake kutoka Mkoa wa Simiyu. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Angelina Malembeka, marafiki na familia yake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri, familia yake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani, Wajumbe wa Jumuiya ya Wazazi Kata na Mpiga kura wake kutoka Jimbo la Singida Kaskazini. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Viongozi na Wajumbe wa Taasisi ya Tanzania Kizazi Imara *Foundation* kutoka Jijini Tanga. *(Makofi)*

Tunao wageni 10 wa Mheshimiwa Boniphace Getere, Wanafunzi kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo. *(Makofi)*

Tunao wageni 33 wa Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Madiwani kutoka Uyui Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

Wapo wageni 49 wa Mheshimiwa Joseph Kakunda, Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM Wilaya ya Sikonge, Sekretarieti ya CCM Wilaya ya Sikonge na Waheshimiwa Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

Tunao wageni 38 wa Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve, Wajumbe wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake na Kamati ya Utekelezaji ya Wilaya kutoka Mufindi Kusini. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 14 wa Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Wilaya na Sekretarieti. *(Makofi)*

Pia, wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo: tunao wanafunzi wawili na walimu wawili kutoka Shule ya Sekondari Hellen’s ya Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Yupo Mwalimu Emmanuel Charles na Mwalimu Hemedy Shaidu kutoka Shule ya Msingi *Fountain Gate* ya Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi 12 na walimu wanne wa Shule ya Awali na Msingi JC O’ghabann kutoka Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 63 na walimu 4 wa Shule ya Msingi Notra Dame kutoka Njiro Arusha. *(Makofi)*

Tunao pia wanafunzi 38 na walimu 10 kutoka Shule ya Msingi *Destiny* ya Mkuranga Mkoa wa Pwani. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2024 ***(The Finance Bill, 2024)***

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kupeleka Muswada kwenye Kamati ya Bajeti, Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2024 *(The Finance Bill, 2024),* hivi punde umesomwa kwa mara ya kwanza Bungeni, mara baada ya hatua hiyo na kwa mamlaka aliyonayo chini ya Kanuni ya 97 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Spika wa Bunge, anaelekeza Muswada huo ufanyiwe kazi na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa majadiliano yanaendelea, tuna Mbunge ana dharura. Tutaanza na Mheshimiwa Christina Mnzava, ajiandae Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo na Mheshimiwa Cosato Chumi ajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kunipa afya njema na kuweza kusimama katika Bunge lako Tukufu na kutoa mchango wangu katika Bajeti Kuu iliyoko mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia namshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo anaifanya kwetu Watanzania. Tumeona ni jinsi gani ambavyo anaendelea kuongeza bajeti ili maendeleo ya nchi hii yaweze kusonga mbele. Pia, nimpongeze sana Kaka yangu Dkt. Mwigulu Nchemba kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. Kazi ngumu ya kuhakikisha kwamba mapato ya nchi hii yanaendelea kuimarika na kuendelea kusimamaia matumizi katika sekta mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ongezeko kubwa la bajeti. Ukiangalia kwa mwaka wa fedha tunaoumaliza, kwa maana ya 2023/2024, tuliidhinisha hapa takriban shilingi trilioni 44.39 lakini kwa mwaka huu wamekuja na ongezeko la karibu trilioni 5. Kwa kweli hili ni jambo ambalo linaonyesha ni jinsi gani Serikali ya Mama Samia inaendelea kuwajali Watanzania kwa kuendelea kuongeza fedha kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika sekta ya afya, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, sekta hii ilitengewa shilingi trilioni 1.24 hadi Machi zilitolewa takriban shilingi bilioni 838, kwa hiyo, hii ilikuwa karibu asilimia 68 ya fedha ambazo tulikuwa tumezipitisha katika Bunge hili ziliweza kupelekwa kwenye Wizara husika. Hii siyo katika sekta ya afya peke yake, hata sekta na Wizara zingine fedha zimepelekwa kwa kweli kwa mtiririko mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika fedha ambazo ziliidhinishwa na Wizara ya Afya, tumeona zimefanya kazi nyingi sana. Kuna maboma ambayo yamejengwa, katika sekta ya afya kuna zahanati zimejengwa, kuna vituo vya afya vimejengwa, kuna vitendea kazi, vifaatiba vya uchunguzi na ugunduzi vimenunuliwa, takriban Mikoa yote. Kwa kweli hii inaonyesha ni jinsi gani Serikali ya Mama Samia inavyowajali Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sekta hii ya afya napenda niseme kitu kimoja, pamoja na mazuri yote ambayo Mama Samia anafanya, kuna changamoto ambayo mimi naona ni ndogo sana, na Wizara hii ya Fedha ambayo ndiyo inabeba mfuko mzima wa Serikali inaweza ikatatua. Wananchi wa Tanzania hususan katika Mkoa wa Shinyanga, kulikuwa kuna Sera ya Afya ya kuhakikisha kwamba kila kijiji na kila mtaa unakuwa na zahanati na kila Kata inakuwa na kituo cha afya, Sera hiyo haijawahi kufutwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuna wananchi ambao kwa mapenzi na kwa hamasa waliyoipata waliweza kujitolea kujenga maboma, maboma yamefika katika lenta lakini yanaachwa, hii ni kuwavunja nguvu Watanzania, kuwavunja moyo Watanzania ambao walitumia nguvu zao katika kuendeleza maendeleo ya Tanzania yaani wakajitolea kwamba na sisi tuwe sehemu ya maendeleo ya nchi yetu, wamejenga yale maboma, yamefika kwenye lenta mengine yamepauliwa, lakini Serikali inashindwa kutoa fedha kumalizia yale maboma. Nikuombe sana Mheshimiwa Mwigulu, utakapokuja kuhitimisha bajeti yako utuambie, mna mpango gani kwa zile nguvukazi ambazo wananchi wa Tanzania walizitumia kuhakikisha kwamba, wanajenga maboma, wamejenga, mtawasaidia vipi kuhakikisha yale maboma yanakamilika ili na wao wawe sehemu ya mchango ambao Serikali ya Mama Samia inatoa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ningependa kuwapongeza sana Wizara hii ya Fedha kwa jinsi ambavyo mmeweza kuwasaidia watoto wetu na wanawake wa Tanzania, kwa kutoa kodi katika malighafi ya kutengeneza taulo za kike. Kwa kweli, nawashukuru sana. Pamoja na kutoa hiyo kodi ambayo ni asilimia karibu 10 mpaka 25 kwa wazalishaji, naomba sana usimamizi uwepo hasa katika sekta nzima ya viwanda na biashara, kwa sababu ninyi mmetoa kodi lakini wanaokuja kusimamia ule utekelezaji ili wananchi waweze kupata unafuu wa hiyo kodi ambayo Serikali imewaonea huruma inasimamiwa na Wizara ya Viwanda na Biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta kodi imetolewa, kwa sababu siyo mara ya kwanza, Wabunge waliotangulia katika Bunge hili walishasimama hapa hasa wanawake niwapongeze sana, wakaomba hizi pedi, taulo za kike ziweze kupunguziwa kodi, ilitolewa *VAT* ikawa haina *VAT,* lakini wafanyabiashara ambao siyo waaminifu hawakuweza kupunguza bei za taulo za kike. Kwa hiyo, mtumiaji ambaye ni mwananchi wa kawaida ambaye hana uwezo wa kununua pedi kwa gharama kubwa aliendelea kununua pedi kwa gharama ile ile ambayo pamoja na kwamba Serikali imepunguza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana Wizara inayohusika, kama Wizara ya Fedha, kama Serikali ya Mama Samia imeamua kutoa kodi hiyo kwa mali ghafi, kwanza tuangalie tuna viwanda vingapi Tanzania ambavyo vinazalisha? Isiwe kwamba tunapunguza kodi, tunanufaisha watu wengine ambao wanaagiza hizi pedi kutoka nje au wanaangiza *raw materials* kutoka nje hapa wanakuja kufanya *final touches* za hizo bidhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana Wizara inayohusika ihakikishe kwamba inafuatilia, inasimamia lile punguzo la kodi kwa ajili ya malighafi za kutengeneza taulo za kike basi linawanufaisha wananchi ambao ni wa kawaida. Tukitaka kujua ni akina nani wananufaika, tuangalie wananchi ambao wananufaika na huu mpango wa *TASAF*, ni rahisi sana kuwapata wananchi ambao wanastahili, kwa sababu siyo wanawake wote Tanzania au familia zote ambazo hazina uwezo wa kununua hizo taulo za kike, wengine wana uwezo lakini wale ambao wanatoka kaya maskini ndiyo hasa ninaona ni walengwa ambao wanatakiwa wanufaike na hizo taulo za kike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo napenda kulizungumzia, tumeona hapo wakati wanawasilisha taarifa ya nishati, tuliletewa magari hapa ambayo yanatumia gesi, tukaanza kuelimishwa na kuhamasishwa na kuna baadhi ya wananchi wameshaanza kutumia magari ambayo yana mfumo wa gesi. Ningeomba sasa badala ya kupandisha hii bidhaa ya gesi, mmepandisha kama shilingi 300 na kitu, sina kumbukumbu

vizuri, sasa kama mnapandisha, wakati tunahamasisha kutunza mazingira, wakati tunahamasisha matumizi ya gesi na gesi asilia tunayo sisi watanzania huku ndani, ni kwanini tusiweke mazingira mazuri tukapunguza bei ya gesi lakini hata tukapunguza kodi kwenye ile mifumo maana kufunga mfumo wa gesi ndiyo tatizo, ndiyo gharama kubwa lakini gesi haina gharama kubwa zaidi. Ningeomba hili ambalo mmepandisha Mheshimiwa Waziri karibia shilingi 300 na kitu kwa ajili ya gesi ya magari ningeomba muiangalie, muipitie, muweze kupunguza ili wananchi wengi wenye magari waweze kuhamasika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, ningeshauri sasa Serikali tuoneshe mfano. Tunajua tuna safari ndefu, tuna safari nyingi, magari ya Mawaziri, Makatibu Wakuu, Watendaji wa Halmashauri, mna safari za hapa na pale kwa ajili ya kuwahudumia wananchi. Wekeni utaratibu muwe wa kwanza kufunga hiyo mifumo ya gesi ili muweze kutuhamasisha hata sisi Wabunge tuweze kufunga mifumo ya gesi, kwa sababu, kiongozi anaonyesha njia, onesheni njia kwa nyinyi Serikali magari yote yafungwe mfumo wa gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hapo hakikisheni kwamba vinakuwepo vituo vingi. Kama kuna vituo Dar es Salaam, basi na Dodoma viwepo na Mwanza viwepo na Kilimanjaro viwepo ili kila mwananchi aweze kushawishika na kuhamasika kuhakikisha kwamba anatumia mfumo wa gesi katika magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe kabisa anayeumia ni mwananchi wa kawaida, mkiongeza kodi yoyote, mkiongeza kitu chochote, anayeumia ni mlaji wa mwisho kwa sababu ndiye anayelipa kodi kule chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, nimtie moyo endelea kufanya kazi, kazi siyo ndogo na unapofanya kazi nzuri ni lazima utatupiwa mawe. Ukitaka kusifiwa sana jua hufanyi kazi. Ukiona unasifiwa kwa kila kitu jua kwamba haufanyi kazi vizuri, lakini kama kuna mishale jua kwamba anhaa! kumbe majukumu niliyopewa ninayatimiza vizuri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, ninaunga mkono hoja, ninawatakia kila la kheri na Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa naomba kumtambulisha *DC* wa Mtwara, Mheshimiwa Mwanakhamisi Mkunda ambaye yupo *Speaker's Gallery*, karibu. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Gambo, jiandae Mheshimiwa Chumi na Mheshimiwa Chikota pia jiandae.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda nitaomba na mimi nichangie kwenye maeneo matatu ambayo ni kwenye upande wa *service levy*, upande wa madeni ya wazabuni mbalimbali nchini Tanzania na kwenye upande wa *dollarization*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye *service levy*, wafanyabiashara wa sekta ya utalii wamekuwa na changamoto ya usumbufu wa muda mrefu sana kutoka kwenye Halmashauri zetu. Kwanza ni namna ambavyo wanadaiwa zile kodi ni utaratibu ambao haukubaliki. Kuna mfanyabiashara yuko Arusha Mjini anatakiwa alipe *service levy* Halmashauri ya Arusha, anadaiwa Halmashauri za Monduli, Karatu, Ngorongoro na maeneo mengine ambayo anafanya biashara za utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado pia hata sheria yenyewe inataka mtu alipe *service levy* kutokana na *turnover* lakini *nature* ya biashara ya utalii haifanani na biashara nyingine na nitatoa mfano. Kwa mfano, mimi ni *tour operator*, nikimuuzia mgeni nje bidhaa ya utalii Tanzania nauza *package*. Namuuzia *accommodation* lakini sina hoteli, naweza kumuuzia *transportation*, pengine sina magari, na bidhaa nyingine kama *park fees* ambazo ziko Ngorongoro na Serengeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadaye mtalii akishafika Tanzania, mimi wajibu sasa nachukua kile alichonilipa kwenye

*account* yangu, kama alilipa *park fees*, mimi nailipa Ngorongoro na Serengeti. Kama alilipa *accommodation*, labda namlipa Serena au hoteli nyingine. Kama alikuwa anataka kwenda Zanzibar, nimemuwekea kwenye *package* yangu, mimi nalipia pia na malipo yake ya kule Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwisho wa siku tukija kulipa *service levy*, nikilipa Ngorongoro watalipa *service levy*, nikilipa Serengeti, watalipa *service levy*, nikimlipa mtu wa *accommodation*, atalipa *service levy* na mimi pia ambaye nimetumika kama *conduit pipe* ya kupokea zile fedha natakiwa pia nilipe *service levy* kutokana na *turn-over*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ushauri wangu hapa Waziri wa Fedha atusaidie kuwasiliana na wenzetu wa TAMISEMI ili kuhakikisha kwamba mtu anapolipa *service levy* basi…

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimuongezee kidogo, mchanganyo uliopo kwenye hiyo sheria ya *service levy* unawakumba pia wawekezaji wengine wenye hali kama hiyo ya utalii ambao wanawekeza kwenye huduma za jamii kama shule, nao wanatakiwa kulipa kwenye *package* ya ada ambapo kuna chakula ndani yake, kuna malazi na kila kitu. Sasa, unakuta wanakuja kuchajiwa hela kubwa kuliko kile kitu wanachochaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nimuongezee taarifa hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gambo.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa yake ni nzuri lakini naomba isichukue muda wangu wa kuchangia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gambo, taarifa ni sehemu ya Kanuni.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubali lakini ndiyo maana nikasema isichukue muda wangu wa kuchangia.

**NAIBU SPIKA:** Endelea bwana.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tulikuwa tunaomba Wizara ya Fedha na TAMISEMI wakae, waweke utaratibu mzuri zaidi wa kuweza kusimamia chanzo hiki, kwa sababu Halmashauri hizi zinapewa makadirio ya kukusanya fedha, kwa hiyo wanatumia pia hii ni kama fursa ya kwenda kukusanya kila mahali na mwisho wa siku wanai-*disturb* sekta ya utalii ambayo ni sekta nyeti sana katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo langu la pili ni kuhusu madeni. Unajua hii nchi wageni wana thamani zaidi kuliko Watanzania. Leo angalia mikataba yote ya wakandarasi wa nje, mkandarasi wa nje akipewa mkataba lazima kunakuwa kuna *clause* pale inasema kwamba Serikali ikichelewa kumlipa italipa pia na riba. Wengine wanakwenda mpaka kusema kabisa pengine watalipa riba asilimia 3 juu ya riba ambayo inawekwa na wenzetu wa Benki Kuu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, je, kwa huyu mfanyabiashara wa Tanzania ambaye anayefanya kazi kwenye taasisi zetu, kwenye Halmashauri, yeye mbona hawekewi riba? Mwisho wa siku huyu mtu unakuta amekwenda kukopa fedha benki, benki wamemuwekea riba, kadri Serikali inavyochelewa kumlipa anapata hasara na mwisho wa siku unakuta vitu vyao vinapigwa mnada na wanapata hasara kubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba kwanza, Waziri wa Fedha kwenye bajeti yake hii atauambie mpaka sasa hivi kuna madeni kiasi gani ya wazabuni wa ndani katika nchi yetu ya Tanzania? Pia, atuambie je, bajeti hii tunayoipitisha Halmashauri zetu na taasisi za Serikali zimeyatambua madeni hayo na

wametenga fedha za kwenda kuwalipa? Maana bila ya kufanya hivyo, uwezekano wa kuwalipa utakuwa mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa zaidi tunaomba pia tuweke utaratibu hapa kwamba Mtanzania au mtu yeyote anayefanya kazi za ndani tuweke pia na riba ili Serikali ikichelewa kulipa iweke ni madeni ya kipaumbele kama ambavyo wanafanya kwa wenzetu wanaotoka nchi za nje. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika hili tutaangallia hata uwezekano, kabla ya kukubali bajeti yako ipite Bajeti Kuu ya Serikali, tutaomba tupate ufafanuzi wa kutosha kwenye kipengele hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ni kwenye mambo ya *dollarization*. Unajua hii nchi yetu hii, tukiona watu wameongea jambo, tunaamka tunatoa matamko bila kuangalia na ukubwa wa changamoto ya matamko yetu na sekta zenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano kwenye changamoto ya upatikanaji wa dola, hapa nitakupa mfano halisi, leo wenzetu wa Benki Kuu wanasema wana-*control price*. Ukiwauliza leo watakwambia kwamba dola ukitaka kubadilisha ni shilingi 2,680 lakini namuuliza huyu mtu wa Benki Kuu, je, nikienda leo benki nikitaka nibadilishe shilingi nipate dola kwa *rate* hiyo mnayonipa itapatikana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, benki nyingi ukienda leo wanakwambia kwa siku unaweza ukapata dola 500, sasa dola 500 unafanyia nini? Mimi juzi hapa, nakupa mfano hai, nilikuwa na shida ya dola 300,000, nilitumia mwezi mmoja kuweza kupata dola 300,000 ili niweze kununua kitu ambacho nilitaka kununua nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unajiuliza, leo mnasema mna-*control price*. Mkisha-*control*, mtu akienda kule nje akikosa, je uwezo wa benki zetu wa kutoa upo? Na kama haupo, Serikali inakuwa ni sababu ya *black market* katika nchi hii. Leo mnasema dola ni shilingi 2,680 hazipatikani, mtu akikwambia nje inapatikana

dola kwa shilingi 3,000 itabidi ununue kwa sababu kule nje huwezi kuuziwa kitu kwa kutumia fedha yetu ya Kitanzania. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi nadhani kwa sababu, wenzetu wa *IMF* kwenye ripoti yao ya hivi karibuni wameweza kukosoa utaratibu wa Benki Kuu au wa Tanzania kwa ku-*control exchange rate* ya dola yetu kwa sababu, haiko *realistic* kule kwenye *market* na ni kitu ambacho kinaleta changamoto kubwa sana. Kwa hiyo ni vizuri mkaangalia umuhimu wa *free market*, mkaangalia uwezekano wa kuruhusu watu wapate dola kwa utaratibu wa ushindani wa soko kama walivyofanya wenzetu wa Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili. Ushauri wangu ni nini kwenye jambo hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia Taarifa ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwenye Ukurasa wa 35, ametuambia kwamba, hadi Machi 2024, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa Dola za Marekani bilioni 5.3. Kiasi ambacho kinakidhi uagizaji wa bidhaa na kununua kutoka nje kwa miezi 4.4 ambacho kiko juu ya lengo la nchi la muda usiopungua miezi minne.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama lengo la nchi ni muda usiopungua miezi minne, kwa nini hii 0.4 ambayo imepungua kwa sababu, pale ni *lower demand and supply*, kwa nini msiichuke mkaiingiza kwenye benki zetu? Ili Watanzania wakitaka kununua bidhaa nje, wakienda kwenye benki, wakute dola zinapatikana kwa sababu, wenzetu wa Kenya wamefaya hivyo na sasa hivi changamoto hii kwa kiwango kikubwa imeondoka kwenye nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la tatu ni, mnapoenda kwenye Sekta ya Utalii, ni sekta ambayo ni *very sensitive*. Leo ukisema kila kitu kifanywe kwa shilingi, sawa nakubali ni hatua sahihi kabisa, lakini mimi ninayefanya biashara ya utalii napokea dola kutoka nchi za nje. Kama Ngorongoro, Taasisi ya Serikali, wanataka nilipe *park fees* kwa dola, hiyo njia itasaidia sana kupunguza *black market*. Mimi nitapokea dola kutoka nje, nitalipa

*park fees* kwa dola kwenye Taasisi ya Serikali, Serikali itabakiwa na zile dola.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkiruhusu kulipa kwa shilingi, nitapokea kwa dola, nikienda kuangalia Benki Kuu shilingi 2,680 huku nje shilingi 3,000 mtakuwa mnachochea *black market*. Maana yake ni nitachukua zile dola zangu, nitakwenda kununua nje ya mfumo, halafu mwisho wa siku nitakwenda kulipa kwa shilingi na zile dola zenyewe hamtaziona kwa sababu, zitakuwa mikononi mwa watu, lakini zikienda kwenye Taasisi ya Serikali inakuwa ni rahisi zaidi kuziona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nadhani hili suala la *dollarization*, Serikali inatakiwa itulie…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, kengele ya pili.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ishirikishe sekta zote, isichukue maamuzi ya haraka na maamuzi ya jumla. Nashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chumi. Jiandae Mheshimiwa Chikota, jiandae Mheshimiwa Taletale.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya mimi kuchangia pia, katika hoja hii na namshukuru Mungu kwa uzima na afya zetu. Mimi nitakuwa na mambo kadhaa, lakini kwanza naanza na pongezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia, kutumia nafasi hii kuipongeza Serikali na Mheshimiwa Rais kwa mambo ambayo yanafanyika katika Jimbo la Mafinga Mjini. Kwanza sisi, kama watu ambao tunajishukughulisha na kilimo, tunapongeza sana suala la mbolea. Tulishauri hapa Bungeni, kweli Serikali ikaleta ruzuku ya mbolea na baadae kulikuwa na changamoto za hapa na pale, tumeendelea kushauri na maboresho yameendelea kufanyika. Kwa hiyo hili ni jambo linalostahili pongezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia, naishukuru na kuipongeza Serikali katika kufanikisha miradi mbalimbali ya kijamii. Tuna kituo cha afya pale Ifingo, tunashukuru sana kimekamilika na tumepata gari la kubebea wagonjwa *(ambulance)*, tunachosubiri kutoka kwa wenzetu wa TAMISEMI ni gari, kwa ajili ya ufuatiliaji kwa wenzetu wa Idara ya Afya. kituo hiki pamoja na kusaidia watu wa Kinyanambo, lakini pia, kinasaidia watu kutoka hadi Ihalimba, watu wa Kata ya Rungemba na watu wa kutoka Jimbo jirani la Kalenga wanakuja pale kupata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika elimu, tumesogeza elimu kwa kujenga Shule ya Sekondari pale Ndolezi na sasa tunaendelea kwa kushirikiana na wananchi kujenga shule nyingine ya msingi, ili kupunguza umbali wa wale watoto wanaotoka kule Ndolezi kwenda Mafinga au kwenda Mwongozo au kwenda Mkombwe Shule ya Msingi. Kwa hiyo, tunapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia, nawapongeza wananchi wote wa Jimbo la Mafinga Mjini kwa sababu, haya yote tunayofanya tunashirikiana kutoka Kata zote na Vijiji na Mitaa yote kwa sababu na wenyewe pamoja na jitihada na nguvu ya Serikali na nguvu ya halmashauri, lakini yapo maeneo kama wale wa Ndolezi na wale wa Kikombo walitoa nguvu zao kwa kushirikiana na jitihada za Serikali kufanikisha miradi ikamilike. Wale wa Kituo cha Afya cha Lufingo, wale wa Bumilayinga wote tunafanya kazi kwa kushirikiana, lakini pia, yote yanafanikiwa kwa sababu, tunashirikiana na uongozi wa Serikali kwa maana ya Mkuu wa Mkoa, Ndugu yangu Peter Serukamba na uongozi wake wa Mkoa, lakini na Mkuu wetu wa Wilaya Dkt. Linda pamoja na Madiwani, wote tunashirikiana na wataalamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yote yanafanikiwa chini ya usimamizi wa Chama chetu Cha Mapinduzi chini ya *Comrade* Yassin Daudi, *MNEC* wetu Ndugu Asas na Katibu wetu wa Mkoa Ndugu Goma, lakini kwa pale Wilayani tuna Mwenyekiti wetu jembe Ndugu George Magelasa Kavenuke na Katibu wetu Ndugu Clement Bakuli pamoja na viongozi wa ngazi zote za chama. Hawa wote ninawapongeza kwa sababu, tunashirikiana

kuleta maendeleo pamoja na wadau wa maendeleo muhimu sana wenzetu wa *Water for Africa*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wametuchimbia visima virefu vya maji kwenye shule zote za sekondari, kwenye zahanati zote, kwenye hospitali yetu ya Mafinga na kwenye vituo vyetu vyote vya afya vya Ifingo, Ihongole pamoja na kule Bumilayinga. Kwa hiyo, ninawapongeza sana na wadau wengine tunaoshirikiana nao kwa maana ya *TARURA, TANESCO, RUWASA, MAUWASA, TFS* na Shamba la *Saohill* pamoja na JKT Mafinga katika kufanikisha maendeleo ya wananchi wa Mafinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi, sasa ninakuja katika mchango wangu. Jana kuna mtu alichangia hapa na alisema Mheshimiwa Mwigulu pamoja na Mheshimiwa Prof. Mkumbo ni *Singida Boys* na mimi nasema nawa-*consider* wao kama wachezaji wa Yanga Maxi Nzengeli na Pacome Zouzoua kwamba, ule ushirikiano wao umeleta heshima kwa klabu ya Yanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama ingekuwa ni Simba ningesema hawa ni Fabrice Ngoma na Sadio Kanoute. Kwa hiyo, ule ushirikiano umeiwezesha Simba kwenda robo fainali Klabu Bingwa, lakini ushirikiano ule ndani ya Yanga, wa Maxi Nzengeli na Pacome Zouzoua, umeiwezesha Yanga kwenda kuchukua ubingwa na kwenda robo fainali. Sasa ninawaomba ushirikiano huu ambao nimetoa mfano, sasa na ninyi mshirikiane kama Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango kuhakikisha kwamba, uchumi wa nchi na maisha ya Wananchi wa Tanzania yanakuwa ni maisha ambayo yameboreshwa na yanakuwa na *affordability*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ili hayo yafanikiwe, tunapozungumzia bajeti, maana yake ni mapato na matumizi. Sasa yapo mapato unaweza kuyapata kwa kutoka jasho, lazima ufanye uzalishaji, lakini yapo mapato yanaweza kupatikana katika nchi yetu bila kutoka jasho. Ninawaomba Mheshimiwa Waziri, nendeni mkarejee mchango wa Mheshimiwa Kakoso wa mwaka

jana wakati wa bajeti kuhusu namna gani Taifa linaweza likanufaika kutokana na hewa ya ukaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi watu wa Gazeti la Mwananchi waliandaa kongamano la kuzungumzia mambo ya mabadiliko ya tabianchi na kwa namna gani hii changamoto inaweza kugeuzwa kuwa fursa. Inaonekana nchi yetu kwa kutumia misitu tuliyonayo, tunaweza tukapata takribani shilingi trilioni mbili na nusu zikachangia katika Pato la Taifa. Hebu wekezeni nguvu katika jambo hili na kuna dhana inajengeka kwamba, hiyo hewa ya ukaa watapata fedha watu ambao wametunza misitu asilia, lakini mimi naomba muende mbele, hata misitu ya kupandwa, hata chai, hata parachichi, hata mikorosho, unaweza kupata fedha katika suala zima la hewa ya ukaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili. Ili tuweze kupata fedha maana yake ni lazima tuzalishe. Sasa nakuomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Waziri wa Mipango pamoja na Waziri wa Kilimo, kumekuwa na kilio kikubwa katika suala zima la kilimo cha chai. Kule Mufindi wawekezaji waliochukua hawafanyi chochote, wafanyakazi kwa miezi minne hawajalipwa mishahara, ukienda Rungwe kilio hichohicho, ukienda Lupembe kule kwa mwenzangu Mheshimiwa Swalle kilio hicho hicho, ukienda Korogwe, ukienda Lushoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu jamani tuone tunaokoa vipi sekta ya uzalishaji ya chai, ili kuona kupitia chai tunaendeleaje kupata fedha za kigeni kama alivyosema Mheshimiwa Mrisho Gambo. Mwisho wa siku tunahitaji dola, tutapataje dola kama hatujaboresha mazingira ya kuzalisha, tukauza hiyo chai tukapata fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninawaomba hebu tujaribu kuliangalia katika muktadha mzima wa kuongeza mapato ya nchi yetu, lakini, ili haya mambo yaweze kwenda vizuri ni lazima miundombinu wezeshi iwepo. Sisi watu wa Mufindi maisha yetu ni kilimo hicho cha chai, mazao ya misuti na kilimo katika ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakuomba Mheshimiwa Waziri utakapokuja kufanya majumuisho, utueleze hatma ya Barabara ya Mafinga kwenda Mgololo, tumesaini mkataba mwaka jana, Mwezi wa Sita, Tarehe 16, mpaka sasa mkandarasi hajaingia kazini. Ninawaomba, ile barabara ni uchumi sio tu wa Mafinga, Mufindi na Iringa, bali ni uchumi wa Taifa hili kwa sababu, kule kunatoka mazao ya misitu; nguzo, mirunda na mbao zinatoka kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unakuta pale malori, ma-*semi trailers* yame-*park* wiki nzima, hayawezi ku-*move*. Wakati wa mvua umesimamisha uchumi kwa sababu, yale magari yaki-*move,* nilishawahi kusema hapa, yatajaza mafuta, utapata *fuel levy,* Serikali itapata mapato. Kwa hiyo, hata gharama za uzalishaji zinakuwa kubwa, nawaomba sana, Mheshimiwa Waziri tuliangalie hili, lakini katika suala hilohilo ambalo ninalizungumzia tena la uzalishaji, Mheshimiwa Waziri tuliteta na wewe pale nje, sisi watu wa Mufindi ndiyo watu wa kwanza kuanzisha Benki ya Wananchi, ilikuwa inaitwa *Mufindi Community Bank (MUCOBA)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, benki nyingine za wananchi mnazoziona nchi hii, walikuja kujifunza *MUCOBA,* lakini benki hii kutokana na mtikisiko wa kiuchumi wakati fulani tuliyumba kiasi kwamba, ninamshukuru sana Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, na Mzee Yassin Daudi alikuwa Mwenyekiti wa Chama wa Wilaya. Tulikaa wakatusaidia, wenzetu wa Benki ya Zanzibar wakaja na wakaongeza mtaji, lakini *all over a sudden* mwaka jana, Mwaka 2022, *TRA* wamekuja kuchukua katika akaunti ambayo iliwekewa fedha za wananchi za mikopo ya asilimia 10 shilingi 681,000,000. Sasa mimi nashindwa kuelewa Mheshimiwa Waziri, benki ambayo inachechemea inawezaje ikadaiwa fedha kiasi cha shilingi 681,000,000?

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mawasilisho kadhaa, nitayaleta mezani kwako unisaidie, barua imeandikwa kwa Kamishna kuomba jambo hili lifanyiwe kazi. Matokeo yake sasa Benki ya Wananchi wa Zanzibar imeona kwamba, hapa hakuna biashara na imeondoka, lakini Benki hii ya Wananchi wa Mufindi

ilikuwa ni msaada kuondokana na ile mikopo tuliyosema hapa siku moja ni mikopo ya kausha damu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri, hebu iangalie hii benki ambayo ni mkombozi kwa wananchi wa kawaida wa Mufindi, wanachukua mikopo katika gharama nafuu na pasipokutakiwa kuweka dhamana kubwa. Mimi naamini unaliweza jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni la miradi. Nakuomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, sisi tuna mradi, katika Mradi wa Miji 28 Mafinga tupo, lakini mpaka sasa hivi mkandarasi hajalipwa *certificate* nne, kaondoa watu wake *site*. Sasa tulijinadi tukasema kwamba, lazima kufikia Mwaka 2025 mradi utakamilika, sasa imebaki miezi saba, mkandarasi hayupo *site*. Nakuomba, wewe kama Waziri wa Fedha, Fedha zipatikane.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho na Mheshimiwa Rais kwenye hili ninampongeza sana, ameshiriki mikutano yote ya mazingira duniani akiendelea na hii *slogan* yake ya *clean energy,* sasa *clean energy* haipo tu kwenye kupikia. Mheshimiwa Waziri hebu kwanza tufanye *incentives* kwa watu wanaowekeza kwenye masuala mazima ya gesi, watu wanaowekeza kubadilisha magari yatoke mifumo ya mafuta kuwa ya gesi, sisi hapohapo tumekuja kuweka tena tozo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninaomba katika kipindi cha miaka mitano hebu kwanza tusahau, twende na *slogan* ya Mheshimiwa Rais ya *clean energy*. Sasa huku Rais anasema *clean energy,* sisi tunaweka tozo juu yake, hatuta-*achieve* hilo jambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la mwisho. Mheshimiwa Waziri umesema kwamba, mafuta yakipanda, ile ikiwa imeshuka ile bei utakuwa unai-*maintain,* ili fedha iende kwenye barabara...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili hiyo Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, naomba kuhitimisha, naunga mkono hoja. Naomba haya niliyoyasema, hasa hili la *MUCOBA* na Barabara ya Mafinga – Mgololo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha alitilie mkazo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Abdallah Chikota, jiandae Mheshimiwa Taletale. Mheshimiwa Taletale.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia, naipongeza Wizara ya Fedha kwa ujumla. Nampongeza Kaka yangu, huyu ni dokta wa uchumi, kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu. Anafanya vizuri sehemu nyingi, anakosea sehemu moja tu na siku akijua kama hapa anakosea, atahamia kwa mnyama. Kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu unapokuwa Yanga ni makosa makubwa sana, kama hujui, pole sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nampongeza Mheshimiwa Rais, kwa kuitengeneza na kuiunda Wizara ya Mipango, naamini Wizara hii ina watu ambao ni mahiri sana. Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo, huyu alikuwa Mwenyekiti wa Kamati yetu ambayo ilikuwa inasimamia Wizara mbili, lakini pia, Mheshimiwa Rais hakuishia hapo akamleta Naibu wake, babu yangu huyu wa Kisukuma, Mheshimiwa Nyongo, pia, alikuwa Mwenyekiti wa Kamati yetu akisimamia Wizara nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwigulu mmeletewa watu haswa. Huyu Mheshimiwa Nyongo ni mjanja, ni simba kwa hiyo, ujue kabisa mmeletewa watu ambao watakusaidia, mkishikana vizuri tutafika mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naanza na Wizara ya Usafirishaji. Kwanza naipongeza, sasa hivi sisi wakazi wa Morogoro tayari treni inafika, lakini ukiwa unashuka kwenye treni unakwenda kuitafuta barabara ya lami, yani ukiingia hapo unapiga vumbi mpaka basi. Huu ni mtihani, kama tumesema tunataka kwenda kisasa ile treni abiria anakwenda ana vumbi mpaka kwenye macho kwa sababu, tu tumeshindwa kuwasaidia wenzetu wa *TRC*

kutengeneza lami kutoka pale kituo kilipo mpaka wanapoelekea watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, basi wangetengeneza hata kilometa tano au kumi. Sisi wakazi wa Morogoro tukishuka kwenye treni pale, tunachezea vumbi, sijui bodaboda, sijui nini, Mheshimiwa Waziri tuiangalie hii. Dhamira ya Mheshimiwa Rais ni kutufanya tuwe *modern*, dhamira ya Mheshimiwa Rais ni kufanya watu wafurahie usafiri wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunaona leo hii treni inafanya kazi, inafika mpaka Morogoro. Mimi ni mkazi wa Ngerengere, basi tupeni lami hata kilometa tano ilimradi wakati unasogea na bodaboda lile vumbi linakuwa limepungua, triii unaingia. Mheshimiwa Mwigulu, Kaka yangu, haya unayaweza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudi kwenye kilio ambacho juzi nilipata bahati ya kukaa karibu na Mheshimiwa Spika, nikaji-*beep,* namba yangu amei-*save* Bigwa – Kisaki, heee! Nimesimama hapa *over four years*, huu ni mwaka wa nne, nalia na Bigwa – Kisaki mpaka Mheshimiwa Spika akaona abadilishe jina kwenye simu yake ani-*save* Bigwa – Kisaki. Kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu, hapa nitakusifia na hata ukisema ubaki na Yanga yako, nitaibakisha tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuomba, Mheshimiwa Bashungwa tumempa mzigo wa kutusaidia sisi wana-Morogoro vijijini, ile barabara inakwenda kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere. Mheshimiwa Rais akitaka kwenda kukagua bwawa ni lazima mumshushe na helikopta, basi timizeni ahadi ya Mheshimiwa Rais, marehemu, pia, mtimize ahadi ambayo Mheshimiwa Mama Samia ameongeza kilometa 78. Nimeongea juzi na Mheshimiwa Waziri, anasema kila kitu kashamaliza, mpira upo kwako.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia basi, kama Pacome ZouZoua, ehee! Ndugu yangu Mheshimiwa Mwigulu nakuomba kabla haujamaliza hii bajeti usimame utuambie sisi wana-Morogoro Kusini Mashariki unaleta lini hii pesa, kwa ajili ya

mkandarasi aanze kujenga Barabara yetu ya Bigwa – Kisaki. Vilevile Barabara yetu ya Ubena – Zomozi inayopitia Ngerengere kuelekea Mvuha. Hizi barabara zinakwenda kufungua uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wana-Morogoro Kusini Mashariki juzi niliongea wakati tunafanya utekelezaji wa Ilani kwenye Jimbo letu la Morogoro Kusini Mashariki, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wetu kaka yangu Mheshimiwa Adam Malima amekwenda ku-*modernize* kule biashara ya *spice*. Sisi baada ya miaka 10 tunakwenda kuwa wakulima wa kwanza na wakubwa wa *spice* Tanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla, lakini hatuwezi kukua na barabara ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitaka ujue kama tunatokea kwenye kijiji kina mateso leo hii nenda, hakuna barabara. Tumetoka kwenye mvua juzi, mashimo mtoto mdogo anajificha gari linapita juu, huu ni mtihani sana. Nakuomba sana kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu kabla haujamaliza bajeti hii usimame useme, mkandarasi anataka *advance* yake tu shilingi 20,000,000,000 ukimpiga nayo usoni, tunamuona mkandarasi *site* anafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunakuwa sehemu ya kuimba iyena iyena yenye nguvu kwa Mheshimiwa Rais wetu. Asikuongopee mtu, uchumi ni barabara pia. Leo hii, sisi tunatamba kusema tunanywesha juisi na kulisha matunda Mkoa wa Dar es Salaam, Mkoa wa Dodoma na Mkoa wa Iringa kwa barabara ileile mbovu, lakini kesho na keshokutwa mkituletea pesa, mkithamini kama sisi wana-Morogoro Kusini Mashariki na wana-Morogoro Vijijini kwa ujumla tunahitaji ile barabara, mtakuwa mmetunza kura za Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kumshukuru Mheshimiwa Rais, kwetu sisi Morogoro Vijijini na Morogoro Kusini Mashariki, ametuletea Mradi wa Morong'anya wa zaidi ya shilingi 23,000,000,000 na Vituo vya afya kwenye Kata yetu ya Mkulazi, hapakuwahi kuwa na kituo cha afya, ametuletea kituo cha afya, ametuletea zahanati. Kiukweli kabisa mimi leo hii nasema 2025

Mheshimiwa Samia kwanza, mengine baadaye na mimi nijipakulie tu ukoko hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki Kiti nitakukuta nacho, lazima nirudi 2025. Ninarudi kwa sababu ya yale ambayo Mheshimiwa Rais ameyafanya, nitarudi kwa yale ambayo sisi tunaona kabisa ni ndoto, lakini, ili tuamke kabisa tuleteeni barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe hili jambo kidogo kwenye upande wa Wizara ya TAMISEMI, upande wetu wa Kituo chetu cha Afya cha Ngerengere. Wewe ulikuwepo hapa wakati nikikiombea pesa Kituo cha Afya cha Ngerengere miaka miwili iliyopita, hiki kituo tumerithi kwa mkoloni, hatuna kituo cha afya. Leo hii hatuna kituo cha afya na gari tulipewa miaka kumi na tano iliyopita kwa hiyo hatuna kituo cha afya, hatuna hata gari la wagonjwa kwenye Kituo cha Afya cha Ngerengere.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sisi wakazi wa Morogoro Vijijini mtutazame. Umesoma bajeti ambayo tunaona kabisa inakwenda kutafsiri maendeleo, inakwenda kutafsiri ile lugha ambayo Mheshimiwa Rais anasimama kuzungumza, ya mabadiliko ya maendeleo ya nchi. Sasa na sisi tuwe sehemu ya hayo mabadiliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashindwa kuzungumza kwa nguvu kwa sababu kuna sehemu nimepewa vitu najisikia raha. Leo hii sina shida ya maji kwa sababu ya huu Mradi wa Morong'anya. Leo hii Kata yetu ya Mkambarani tumeletewa shilingi bilioni nne kwa sababu ya mradi wa maji *Alhamdulilah*. Hapa nimesimama nalia tu kwa sababu ya barabara, kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu nakuomba nisadie basi yaani hata ukisimama kutaka kumaliza hii bajeti useme neno maana kuondoka na shilingi yako ni kuondoka na shilingi za Wizara zote. Sema neno juu ya hii Barabara ya Bigwa – Kisaki…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Taletale, ahsante.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Chikota. Mheshimiwa Nicholaus Ngassa, Mheshimiwa Tabasam na Mheshimiwa Kaboyoka wajiandae.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kumpongeza Waziri wa Fedha kwa hotuba yake. Nimpongeze pia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa hotuba yake. Vilevile niwapongeze kwa utendaji wao wa kazi; Waziri wa Fedha pamoja na Naibu wake na Waziri wa Mipango pamoja na Naibu wake pia na Watendaji Wakuu wa Wizara hizi mbili kwa kazi nzuri ambazo wamezifanya kwa maandalizi mazuri ya hotuba na ndiyo maana wameleta kitu ambacho kinajadiliwa kwa nguvu zote, kwa sababu kitu ambacho kina matumaini kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utaenda kwenye hotuba hizi zote mbili, nikianza na Hotuba ya Hali ya Uchumi ambayo imewasilishwa na Profesa. Mpango wa Maendeleo umezungumzia ule mradi wa kimkakati, Mradi wa *LNG* na mimi nichukue nafasi hii kipekee kumpongeza Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa nguvu kubwa anayoiweka kuhakikisha kwamba Mradi wa *LNG* unatekelezwa, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu ambao utahusisha vitalu vitatu, kitalu namba moja, mbili na nne ambavyo vipo kwenye kina kirefu utakuwa na manufaa makubwa sana kwa nchi yetu. Kwa hotuba yake Mheshimiwa Waziri amesema kazi ambazo zimepangwa kufanyika katika mwaka huu wa fedha ni kukamilisha majadiliano ya mradi ya mkataba kati ya nchi yetu na wawekezaji. Hivyo, tutakaribia kupata *Host Government Agreement (HGA)*, vilevile mkataba wa ugawaji wa mapato. Kazi nyingine ambayo ameifanya ni kuelimisha wananchi umuhimu na manufaa ya mradi huu, vilevile utoaji wa elimu kuhusu fursa na huduma kwa bidhaa za ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wataalamu wa masuala ya gesi wanasema tuna vyanzo vitano vya mapato mradi huu ukitekelezwa. Chanzo cha kwanza kikubwa ni faida yenyewe ya gesi. Chanzo cha pili tutapata kodi ya mapato, chanzo cha tatu tutapata mrabaha, vilevile tutakuwa na Tozo ya *LNG (LNG fee)* lakini kwa kwetu Tanzania kwa sababu mradi huu unatekeleza kwa ubia na Shirika letu la *TPDC* basi ule ushiriki wa *TPDC* kuna mapato tutayapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hapa tuna vyanzo vitano vya uhakika katika mradi huu. Kwa hiyo niipongeze Wizara kwa shughuli zile ambazo zimepangwa, ushauri wangu ni kwamba shughuli hizi zifanyike kwa weledi kwa sababu hili suala sasa la kuelimisha jamii kuhusu manufaa ya mradi huu lazima tulifanye kwa umakini. Awamu ya kwanza kuna dosari ambazo tulizifanya, tuliwaaminisha Wananchi wa Mtwara na Lindi kwamba itakuwa Singapore na itakuwa Dubai kwa hiyo, wataacha kilimo cha korosho watategemea uchumi wa gesi. Kitu ambacho kilikuwa ni makosa makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba timu ya wataalamu ambao wanaandaa *community engagement* na *communication strategy* wahakikishe wanatumia wanasiasa. Wanatumia wawakilishi wakaelezee nini kitafanyika kwa mradi ule? Na si kuwaambia kwamba jamani Mradi wa *LNG* ukianza basi Lindi itakuwa Singapore kwa hiyo korosho mtaacha kulima hamtalima mpunga hamtalima vitu vingine. Makosa yale tuliyafanya na tusirudie tena kwa sababu awamu za kwanza za hamasa tulitoa matamko kama hayo ambayo sisi kama wanasiasa sasa hivi tunaulizwa maswali mengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba wakati wa uelimishaji, timu ya wataalamu ichanganyike na timu ya wawakilishi na wananchi, Waheshimiwa Madiwani, Waheshimiwa Wabunge kwa maana ya wanasiasa ili waende wakafanye kazi hiyo ya kuelezea kwamba nini kitafanyika mradi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafahamu kwamba tuna Kamati ya Majadiliano ambayo ina watu mahiri sana. Tuna

usimamizi mzuri wa Wizara yetu, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati anafanya kazi kubwa sana kuhakikisha kwamba majadiliano yanakamilika. Tuna timu ya wataalamu wabobezi ambao wanashauri timu ya majadiliano lakini kama alivyosema Mheshimiwa Profesa Muhongo jana majadiliano haya yamechukua muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanauliza sasa kinachojadiliwa ni kitu gani? Tutoke tuwaambie wananchi tumefikia hatua gani? Mazungumzo yamechukua muda mrefu sana. Mazungumzo yenyewe yanafanyika Arusha, Lindi hawajui na Mtwara kwenye kitalu hawajui. Kwa hiyo naomba muda wa majadiliano upunguzwe. Hapo awali sisi tulikuwa mbele ya Msumbiji kwenye utekelezaji wa mradi huu lakini kwa sababu ya muda mrefu sasa hivi Msumbiji wapo mbele zaidi yetu sisi. Kwa hiyo, naomba muda wa majadiliano upunguzwe, vilevile tuhakikishe kwamba kile ambacho tutaendelea kukipata tunakipata katika mradi wetu wa gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la manufaa na huduma za bidhaa ambazo zitakuwa *supplied* na watu wetu wa ndani na hapa nakuomba Waziri uratibu jinsi shughuli zitakavyofanyika. Ukiangalia ule uchumi wa gesi na shughuli itakayofanyika pale wakati wa ujenzi wa mradi tutakuwa na watu wengi sana, lakini baada ya ujenzi kukamilika watu watapungua. Kwa hiyo lazima tuwa-*engage* Watu wa Lindi na Mtwara ni muda tunafikiri wao wanaweza kunufaika zaidi wakati wa ujenzi wa mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile vitu vinavyotakiwa pale vinahitaji mtaji mkubwa sana lakini kuna vitu wakazi wa Mtwara na Lindi wanaweza ku-*supply:* nyanya, kunde na mbogamboga. Ndiyo muda sasa Waziri wa Kilimo kupitia mradi wetu wa *irrigation* (umwagiliaji) kuwekeza kwenye mabonde sasa yalipo Mtwara na Lindi. Tuna Bonde la Kinyope, kuna Ngongowele kule Kilwa na Nachingwea kuna miradi ya umwagiliaji, pia kuna Ndanda kuna mradi wa umwagiliaji. Miradi hiyo sasa ipelekewe fedha ili mradi utakapoanza wananchi wa Liwale wa Ndanda, Nanyamba na

Newala waweze ku-*supply* kwenye mradi. Hapo tutakuwa tumewasaidia wananchi wa maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ushauri wangu mwingine ni kwamba sasa Wizara zingine sasa zitekeleze majukumu yao. Tunajenga mradi mkubwa pale Lindi lakini Mji wa Lindi hauna kiwanja cha ndege, Mji wa Lindi kiwanja chake ni cha vumbi, hivyo hizo gharama za mradi zitakuwa kubwa kwa sababu wawekezaji watakuwa wanaishi Dar es Salaam wanashukia Mtwara wanakwenda na asubuhi wanarudi. Ni muda mwafaka sasa wa kutekeleza mradi wetu wa ujenzi wa Uwanja wa Lindi, muda ni huu ili mradi ule ukikamilika basi utaendana na mradi wetu mkubwa ambao tunaujenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ni muda sasa mwafaka wa kukamilisha Ujenzi wa Bandari ya Lindi ambayo vilevile itatoa huduma wakati mradi huu unatekelezwa. Pia, ni muda mwafaka sasa wa ujenzi wa Barabara ya Mtwara – Mingoyo mpaka Masasi, barabara ambayo ni sehemu ya barabara muhimu sana kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara. Ni muda mwafaka sasa wa kuimarisha hospitali yetu ya Kanda ya Kusini ili chochote kikitokea basi kundi kubwa ambalo litakuwepo pale lipate huduma kwenye hospitali zetu za rufaa zilizopo Mtwara na Lindi, vilevile hospitali yetu ya rufaa ya kanda yetu ya kusini iliyopo pale Mitengo – Mtwara *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni muda mwafaka wa kuhakikisha kwamba huduma zote za msingi, huduma zote za kibingwa zinapatikana katika hospitali yetu ile ya kanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa pili ni kuhusu Hotuba ya Wizara ya Fedha ni kuhusu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, kengele ya pili hiyo…

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nicholaus Ngassa, jiandae Mheshimiwa Tabasam, jiandae Mheshimiwa Kaboyoka, jiandae Mheshimiwa Shanif Jamal Mansoor.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi pia ya kuchangia Bajeti Kuu ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Tarehe 16 mwezi huu wa sita kwa maana ya juzi pale Jimbo la Igunga tulikaa mimi na Waheshimiwa Madiwani pamoja na viongozi wetu wa Kamati ya Siasa ya Wilaya na viongozi wetu wa chama wa kata zote 16 za Jimbo la Igunga. Tulikuwa tunafanya Tathmini ya Utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi na kuangalia namna ambavyo tumetekeleza Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi 2020/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapato ya halmashauri yetu ya Wilaya ya Igunga tukijitahidi sana kukusanya ni shilingi bilioni nne kwa mwaka lakini wakati tunafanya tathmini tulijikuta tumetekeleza miradi ya zaidi ya shilingi bilioni 70. Kwa mantiki hiyo nianze kwa kumshukuru Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Serikali yake ya Awamu ya Sita kwa kutupatia fedha nyingi kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwenye Jimbo letu la Igunga. Kwa shilingi bilioni nne ambayo tunaipata kama halmashauri ninaamini kwamba kama tungekuwa tukitumia fedha zetu peke yake ingetuchukua zaidi ya miaka kumi kufikia ambayo tumeyafikia ndani ya miaka minne. Tunasema, ahsante sana kwa Mheshimiwa Rais, ahsante kwa Serikali hii yetu na ahsante kwa Chama chetu Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niwapongeze kaka zangu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, hawa mimi ni majirani zangu lakini pia ni ndugu zangu. Niwashukuru kwa kazi nzuri na kuendelea kuaminiwa na Mheshimiwa Rais, fanyeni kazi sisi ndugu zenu tunawaombea na Mungu atawabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo matatu ningependa kuyachangia mchana huu ambayo naamini yanaweza yakasaidia kututoa hapa tulipo. Jambo la kwanza ningependa kuchangia ni suala la Mamlaka ya Mapato Tanzania, Mamlaka

yetu ya Mapato inafanya vizuri lakini kuna mambo ambayo yanahitaji kuboreshwa ili tuweze kuhakikisha tunakwenda vizuri katika ukusanyaji wa mapato na kuimarisha undugu na Utanzania kati ya Mamlaka yetu ya Mapato ya Tanzania na wafanyabiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza ni mahusiano kati ya wafanyabiashara na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Utakubaliana nami Mheshimiwa Waziri ana kazi kidogo ya kufanya kuwaasa maafisa wake waongeze mahusiano vizuri kati ya wafanyabiashara lakini pia na Mamlaka yao ya Mapato Tanzania *(TRA)*. Wana-*deal* na watu ambao ni watu wa kawaida sana, sasa wao ni wataalamu na wamesomea hii kazi lakini sasa inabidi waende na *approach* ambayo itawasaidia kuwa na mahusiano mazuri na wafanyabiashara wetu waweze kutoa ushirikiano kubwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania na naamini litasaidia kuongeza hata wigo wa mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi trilioni tunazokusanya kwa sasa ukiwa na mahusiano mazuri kati ya wafanyabiashara na Mamlaka yetu ya Mapato Tanzania naamini tutaongeza wigo mkubwa wa ukusanyaji wa kodi nchini. Pia nimefanya kautafiti kidogo kumekuwa na changamoto; Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Maafisa wako wa *TRA,* wamekuwa hawana mahusiano mazuri sana na Viongozi wa Serikali kwa maana ya Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa. Kuna mazingira unakuta hata wanabishana au kama kuna vikao basi unakuta hata maafisa wako hawatokei kwenye vikao. Tunaomba muwajenge, muwaeleze tunajenga nchi moja tushirikiane katika kuhakikisha tunasonga mbele vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ningependa kulichangia mchana huu ni maendeleo vijijini kwa maana ya *rural development and rural transformation*. Kama Taifa kwa sasa tumefanikiwa sana kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwenye suala la shule za msingi ambapo tumeweza kufikia lile lengo la *universal primary education*. Kama Taifa tumejenga shule za msingi kwenye kila kijiji

mpaka sasa, niamini ni vijiji vichache sana nchini havina shule za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo tumefanikiwa kwa kiwango kikubwa ni suala la umeme vijijini *(rural electrification)*. Katika kutekeleza Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi, tuliahidi kila kijiji kitapata umeme. Tumefanikiwa pia nchini kwa sasa tumekamilisha suala la usambazaji wa umeme vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa zahanati, tumejenga zahanati nyingi sana nchini kwa maana inasaidia wananchi kupata huduma za afya. Pia na huduma za kifedha kuna suala la jambo la *financial inclusion* hapa na lenyewe tumefanikiwa kwa kiwango kikubwa sababu ya miamala ya simu (kutumia mitando ya simu). *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuna maeneo mawili ambayo nimefanyia utafiti ni changamoto ambayo itatusaidia sana kwenda kupiga hatua nyingine katika kuhakikisha tunafanya maendeleo vijijini. Kwa kuwa ukijaribu kuangalia 70% mpaka 80% ya Taifa letu ni vijiji na siyo miji. Sasa kuna eneo la kwanza, eneo la barabara vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya Wabunge wamechangia hapa. Katika kukuza uchumi wa nchi mshipa namba moja ni suala la miundombinu kwa maana ya barabara na ukiangalia *landscape* ya nchi yetu maeneo mengi yana mito midogo midogo ambayo ni mito ya misimu. Sasa tuongeze fedha upande wa *TARURA,* mimi niwashauri Serikali kwa sasa mnatupatia takribani shilingi bilioni mbili kwenye kila jimbo, mkifikisha angalau shilingi bilioni tano kwenye kila jimbo tutafanya maendeleo makubwa sana katika Taifa hili na tutafungua uchumi kwa kiwango kikubwa sana. Hii ndiyo itakuwa eneo moja la kusaidia sana katika mabadiliko na maendeleo ya vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tunasema miundombinu kwa maana ya barabara ndiyo mishipa ya uchumi. Barabara zitajengwa vijijini lakini pia na yale madaraja madogo madogo

ambayo kwenye mito yetu mingi, kwa sababu ukiangalia maeneo yetu mengi yanakuwa na mabonde mabonde tukishaweka haya madaraja madogo madogo na makalavati itatusaidia sana kuwa na barabara zinazopitika kwa mwaka mzima hata misimu ya mvua na itasaidia sana katika kukuza uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ningependa kulielezea Serikali ambalo kwa sasa inabidi tupambane katika kuhakikisha tunalifanikisha ni maji vijijini. Ukifanya utafiti katika vitu vya muhimu ukiacha pumzi jambo linalofuata ni maji. Tunaomba mwongeze nguvu, mwongeze fedha katika eneo la maji ifike hatua vijijini maji yasiwe anasa yaani kila mwananchi awe na maji nyumbani kama ulivyo umeme. Kama hana nyumbani basi yanakuwa karibu ili tuwaepushe wananchi kutokana na adha ya kutoka na matrela ya ng'ombe maji kilometa tano, kumi kwenda kwa ajili ya kupata maji. Serikali tunaomba mliangalie hili na kwenye kupitia mipango (Tume ya Mipango) mliangalie sana suala la upatikanaji wa maji ambalo ninaamini ni moja ya huduma ya msingi sana kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ambalo ningependa kulichangia mchana huu ni Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025/2050. Nikupongeze kaka yangu Mheshimiwa Profesa Kitila mnakwenda vizuri na Tume yako ya Mipango na wataalamu wote ambao mnashirikiana nao, lakini nikushauri katika Dira hii tunayoiandaa sasa hivi kwanza i-*reflect* mahitaji ya vijana. Taifa letu kwa sasa asilimia takribani 60 mpaka 70 ni vijana ambao ni chini ya miaka 45 (miaka 40 mpaka 30 kushuka chini) twende tukatengeze Dira itakayo-*reflect* mahitaji ya hili Taifa la sasa. Twende na mtazamo *(thinking)* ya kisasa ambayo ndivyo mnavyoliona Taifa la utandawazi. Tuangalie mila na desturi zetu, tuangalie mshikamano na umoja wa nchi yetu ambazo ni tunu zetu lakini tuangalie mahitaji ya Taifa tunalokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine la msingi tutengeneze Dira ambayo itatengeneza mazingira ya kuondokana na urasimu nchini. Kwa sababu katika mipango yako na uwekezaji jambo litakalokukwamisha katika nchi hii ni urasimu.

Tumekuwa tukitoa mifano ya mataifa ya jirani kwamba kama mwekezaji anahitaji vibali ndani ya siku mbili, ndani ya siku saba amepata vibali. Kwetu sisi bado tunapigana *mark time,* mwekezaji anakuja miezi miwili, miezi mitatu bado anasumbuliwa na kuhangaishwa. Sasa unaangalia je? Ni nini? Tunamkwamisha nani? Tunalikwamisha Taifa letu. Mwangalie katika Dira ya Maendeleo mnayoitengeneza suala la urasimu mliwekee kabisa mwongozo tuje tuepuke vikwazo vingi katika uwekezaji, kwa sababu suala la uchumi wa nchi uwekezaji ndiyo *indicator* namba moja ambayo itatusaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine tunatakiwa tuongeze wigo wa walipa kodi, *tax base* yetu bado ndogo sana. Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Mipango mfanye jitihada, umizeni vichwa, *think tanks* wako waumize vichwa tuongeze *tax base*. Ni aibu kwa Taifa kutokuwa na walipa kodi zaidi ya milioni tano kwenye Taifa la watu milioni 60 angalau tuanze kusoma kwenye *digits* na milioni kumi na tano, milioni kumi saba za walipa kodi. Tutakuza sana uchumi na tutakusanya matrilioni ya fedha mengi sana kupitia Mamlaka yetu ya Mapato na taasisi zinazokusanya maduhuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu katika Dira ya Maendeleo ya Taifa ningependa kuongelea suala la sekta za uzalishaji. Kwenye sekta za uzalishaji Mheshimiwa Profesa liangalieni hili na tuwe na vipaumbele tuamue kama Taifa tunaamua kuwekeza kwenye nini? Nini kitakuwa kipaumbele kama Taifa kwenye sekta ya uzalishaji? Au tunaamua kwenda na sekta zote tunaamua kwenda na kilimo, ufugaji, madini, viwanda. Kama tunaamua kuweka *priorities* tuangalie yaani Taifa letu lifikie hatua tunajivunia kwamba tuna kitu tunakifanya kama Taifa kimoja ambacho kinatutambulisha duniani lakini pia kinakuza Pato na Uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulichangia katika suala la Dira ya Maendeleo ya Taifa, Mheshimiwa Waziri naomba mliangalie sana tuje na sera ambazo zitaweza kutusaidia kwenye suala la uboreshaji wa makazi ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tuna wananchi ambao wanaishi maisha duni sana huko vijijini, lakini katika dira hii ambayo tunaenda kutengeneza ya kwenda 2050 tuitengeneze na tutakuja na sera ambazo zitasaidia sana kuboresha makazi. Tuhakikishe wananchi wanaishi katika makazi bora na ndiyo namna ambavyo tunatoka kwenye dunia hii sasa, tunatoka kuwa nchi yenye kipato cha chini kwenda kipato cha kati, maana yake hata makazi ya wananchi wetu yawe bora zaidi pia wawe na ustawi ulioimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tabasam, jiandae Mheshimiwa Kaboyoka, jiandae Mheshimiwa Shanif Jamal.

Mheshimiwa Tabasam hayupo. Mheshimiwa Kaboyoka, jiandae Mheshimiwa Shanif Mansoor.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hizi hoja mbili za Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango na Uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kuwapongeza kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya Wizara zote mbili na Mawaziri wote wawili, Naibu Mawaziri wenu na wafanyakazi wote wa Wizara hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri niongee tu kwamba ninavyoangalia bajeti zetu kila mwaka, tukija hapa ni matatizo ya kuambiwa bajeti iliyopitishwa mwaka jana hili na hili halikufanyika, halafu hapo hapo unakuta hata zile barabara ambazo zimewekewa hela zimetengenezwa kidogo, zingine hazijatengenezwa, kunakuwa na wakandarasi ambao wanadai fedha nyingi na mapungufu mengi katika kutekeleza haya tunayopanga. Kwa hiyo, najiuliza hivi tunapanga bajeti kila mwaka ili nini, kama tunayopanga hayatekelezeki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hata ukiangalia ripoti ya *CAG,* nimekuwa Mwenyekiti wa Kamati hii mwaka wa tisa huu na kila mwaka tungepiga *total* ya fedha ambayo inaonekana kwamba haitumiki vizuri tusingehitaji kwenda kukopa. Kwa hiyo, ukiangalia tunakosa *monitoring* na *evaluation system* ambayo inasema haya tunayopitisha hapa yanatekelezwa vizuri? Kama hayatekelezwi vizuri tufanye nini hatua gani ichukuliwe? Kama mwananchi anaona aliahidiwa maji hayafiki, barabara imetengenezwa kidogo, fedha nyingi inaenda kwa wakandarasi, sasa tunapoteza muda wa nini kukaa hapa kupitisha bajeti kila mwaka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nikaangalia tunaposifu wenzetu wa China kwamba wanatengeneza mipango yao vizuri walikuwa nchi maskini hata miaka ile Mwalimu Nyerere akiwapigania hata waingie wawe na wawakilishi wa kudumu kwenye *UN* walikuwa chini sana, mpaka wanatetewa na Tanzania, sasa hivi wapo mbali sana, lakini unaona wenzetu wana *centrally planned economy* ambayo imepangwa vizuri sana, *so much so that* inafuatiliwa na inakuwa *monitored* kwamba, kila kilichopangwa kinatekelezwa kilivyopangwa. Hiyo inaleta unafuu hata kwa Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi namuonea huruma sana mkwe wangu Dkt. Mwigulu Nchemba, kila anayesimama hapa anamuomba barabara yangu haijaisha, hiki na kile hakijaisha. Leo tena tunachangia kama tupo kwenye *sectoral budget,* sasa mimi nachanganyikiwa kwamba hivi tunachangia za kisekta au tunamsaidia Waziri kwamba bajeti yako iendeje, maana yake tunaanza kuomba tena. Sasa unaona kwamba jamani sijui ni mimi nachanganyikiwa au ni nani? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nasema kwamba hebu tuangalie na tujifunze kwa wenzetu, Je, ni *discipline* tunakosa sisi watanzania kwamba, hata mkwe wangu watu wakikufuata wakikupigia magoti kweli hulali, kwa hiyo unasogeza fedha hii tena unapeleka kule. Mwingine kuna matamshi ya viongozi kwa nini hapa hamjaleta maji? Waziri njoo kesho, haya hawa wapate maji kesho, tunakimbia tena. Kwa hiyo, mimi najiuliza hivi mipango yote hii tunafanya inatusaidia nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niombe tu Waziri wetu wa Mipango na Uwekezaji hebu ajaribu kuunda Wizara yake *such a way that,* kwa kweli tutakuwa na *plans* nzuri za *short term, medium term* na *long term* ili hata bajeti ikifanywa wao kazi yao kubwa wana-*monitor*. Kunakuwa na *midterm monitoring* kuona kwamba hiki tulichofanya kinakwendaje ili tu-*arrest the situation* kabla mambo hayajaharibika. Tusingoje mpaka aje CAG kuona hapa tuna mapungufu, hapa fedha imeibiwa. Sasa, huo muda wa kuibiwa fedha ni kwa vile hakufanyiwi *monitoring* na *evaluation* kila wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nasema kwamba tujifunze kwa wenzetu Marekani wana mipango miwili *centrally planned* pia wana ile ya binafsi. Ukienda wenzetu wa Denmark wana *system* ambayo ndiyo kama tulijaribu kuitumia kwamba, tunagatua madaraka. Sasa, mimi nashindwa kuelewa sasa hivi tumesimama wapi, mipango yetu ipo wapi? Maana kila leo unavurugwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mwingine kapata fedha yake nje huko, anakuja anamwambia Waziri wa Fedha nina fedha hii nimeleta nataka kufanya hivi, sasa hata Waziri anachanganyikiwa anaona nifanye nini sasa? Tumepanga mpango huu, kuna haya yanayokuja na hatujui ni mikopo au ni misaada, na hiyo misaada inakuja kwa njia gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu ambacho nimeona tuna tatizo kubwa sana, tunakosa *land masterplan,* sasa tumesema hapa kwamba uti wa mgongo wa nchi yetu ni wakulima ambao wengi ndiyo wameajiriwa huko vijijini. Pia tumeona kila siku kama siyo ng'ombe wameingizwa kwenye mashamba basi usiku ni tembo, bado ndege wa kweleakwelea, bado wafugaji na wakulima wanavyopigana mishale, sasa tunasema haya yote ni ya nini? Halafu tukija kupitisha bajeti ya Wizara hii ya Ardhi tunapitisha sawa sawa na mtu mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nafikiri Waziri wetu wa Mipango na Uwekezaji hebu liangalie hili kwamba, utafanya nini kuwe na *land masterplan* ambayo inaonesha *vividly* kwamba

sasa hapa bwana, na tulisikia juzi watu wamejenga kwenye vijiji chini kuna madini, haya tunafanya nini? Tunayafukia, tunamng'oa yule mwenye nyumba ili uchukue madini yako? Wengine wanasema ukilima bangi ni ya kwako, lakini kwenye madini ni ya Serikali yakiwa nyumbani kwako. Sasa tusiwe na *double standard.* Kwa hiyo, tuseme hivi, tuwe na *masterplans* ambazo zinatusaidia. *Land masterplans is very important* ili hata mipango hii ya kufanya *compensation,* leo tunapanga barabara inapita hapa lazima hawa wavunjiwe nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mlinipa mradi kule wa barabara yetu ya kutoka Ndungu hadi Mkomazi, Mkandarasi yupo *site* lakini fedha ya *compensation* haijapelekwa. Fedha ya *advance* ya Mkandarasi haijapelekwa. Sasa hizi *compensation* kwa nini ziwepo? Zinakuwepo kwa vile hatuna *masterplan* kwamba, hapa itapita barabara, wananchi waishi hapa, mkulima ni hapa, mfugaji usivuke hapa na wewe eneo lako hilo, lakini sasa ni *mixed grill* ambayo hatujui tunakwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni *National Water and Sanitation Masterplan*. Kila anayelia hapa maji. Tunajua maji ni uhai, hii nchi haiwezi kwenda kama hatuna maji, hata tungepata dhahabu majengo na kila kitu. Kama hakuna maji hamna anayeweza ku-*survive*. Kwa hiyo, niombe sana ndugu yangu Prof. Kitila Mkumbo najua unaweza sana, hebu tuangalie hivi vitu vyote tuvisimamie, Wizara yako ni ya mipango *I am sure* muda huu ni mfupi sana na bado una *mobilize resources* na watu. Hii ni Wizara ambayo inatakiwa iwe Wizara Mama ambayo kila Wizara inachukua mipango yake kama ilivyopitishwa na Wizara yako ya Mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo Mawaziri Wakuu na ambao walikuwa Mawaziri wa Fedha ambao bado wanaishi, Mheshimiwa Msuya, walijua mipango huko nyuma ilikuwa inakwendaje, amekuwa Wizara ya Fedha alipokuwa Waziri pale, tukiwa-*consult* hawa wanaweza kutusaidia halafu tuwapeleke vijana wetu nje wakasome. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi vitu siyo vya kubahatisha tu kwamba leo umewekwa unaweka hapa, msaidiane kabisa na Waziri wetu ili tuwe na mipango ambayo ipo *very systematic* halafu *monitoring and evaluation* tusilindane, kama mtu hafanyi kazi basi, siyo leo ameharibu hapa anahamishiwa kesho kule, anaachishwa kazi kesho anakuwa *appointed* kazi ile pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona hata ripoti za CAG hapa wengine ambao tuliona waliwekwa pembeni…

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Kaboyoka, kengele ya pili.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Basi naomba hiyo Wizara yetu ya *Planning* ifanye kazi yake *properly* ya *planning,* ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shanif Jamal Mansoor, jiandae Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei na Mheshimiwa Manyinyi jiandae.

**MHE. SHANIF M. JAMAL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema, niweze kusimama kwenye Bunge lako Tukufu na kuchangia hoja ambayo ipo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Kwimba kwa kunipa ushirikiano mkubwa ili niweze kutimiza wajibu wangu wa kuwaletea maendeleo. Pia niwapongeze wananchi kwa michango mingi wanayotoa kwenye miradi mbalimbali na nisiwasahau Waheshimiwa Madiwani kwa kunipa ushirikiano mzuri niweze kutimiza wajibu wangu, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea miradi mingi ya maendeleo ndani ya Jimbo la Kwimba. Nikianza kutaja moja baada ya nyingine ni miradi mingi sana naomba niseme machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la sekta ya elimu. Ndani ya awamu hii tumeweza kujenga Shule za Msingi tatu. Shule ya Lunene, Mwaluleho na Mwamaya pia Shule za Msingi mpya tatu zimejengwa. Pia, Shule za Sekondari tatu zimejengwa za Hungumalwa, Kilabhoya na Mpamwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye suala la afya tumeweza kujenga Hospitali ya Wilaya mpya, tumepata *ambulance* mpya, vituo vya afya viwili vimejengwa vya Hungumalwa na Kikubiji. Hungumalwa imeshaanza kutoa huduma pia pale tumeletewa *ambulance* nyingine. Kikubiji pia inaanza kutoa huduma mwezi ujao. Pia, tumejenga zahanati mbili ambazo ni Mang'ombe na Sangu na zahanati zote zimeanza kutoa huduma. Kwa kweli kwenye afya tumepiga hatua kubwa namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa msaada mzuri na miradi mingi aliyotuletea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongee kwenye suala la maji. Kwenye maji tuna changamoto. Sisi Wilaya na Jimbo la Kwimba tuna mtandao wa bomba, tunategemea maji kutoka *KASHWASA*. *KASHWASA* ndiyo wanazalisha maji Ihelele Wilaya ya Misungwi, wanatuingizia maji kwenye *tank* letu ya Mhalo. Kutoka Mhalo maji yanasambazwa mpaka kwenda Ngudu Mjini. Tumejenga matenki mawili ya lita milioni mbili Ngudu Mjini. Changamoto tuliyonayo sasa hivi ni kwamba *KASHWASA* hawatuletei maji ya kutosha, tumeanza kuwa na mgao wa maji. Wanatuletea maji tunapata mara moja kwa wiki maana yake Mji wa Ngudu watu wanapata maji mara moja kwa wiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mateso makubwa sana wananchi wanapata kwenye huduma ya maji. Wanasema *KASHWASA* kwa sababu wanapanua wanakwenda mpaka Singida sijui Tabora lakini huku nyuma wanatuacha, wanasema sisi

ni wateja wadogo maana yake hawaoni umuhimu wetu sisi. Ningeomba Wizara ya Maji ifuatilie *KASHWASA,* huduma zao zimeharibika sana. Sasa hivi sisi hatupati maji ya kutosha, mahitaji yetu ni makubwa hawatupatii, wanatupatia mgao. Kwa nini watupatie mgao wakati miundombinu ipo na maji yapo, kwa nini wanashindwa kutusukumia maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba suala la maji liingiliwe na Wizara ya Maji wafuatilie *KASHWASA* kwa nini maji imekuwa ni mgao kwa wananchi wa Ngudu? Tumepata mgao ni mkubwa sana wananchi wanateseka. Tuna hospitali mpya ukija utawahurumia wagonjwa pale, hakuna maji kwenye vyoo, wanenda na madumu, wanajisaidia nje. Kwa kweli hali yetu siyo nzuri, hospitali mpya lakini imechakaa kwa sababu hakuna maji. Kwa kweli, maji ni tatizo kubwa naomba waweze kutusaidia angalau maji yapatikane kwenye Wilaya yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la barabara. Kwenye suala la barabara niwapongeze *TARURA* wakati wa mvua za *El Nino TARURA* kwa kweli wamefanya kazi nzuri, wameweza kuboresha miundombinu iliyoharibika, wameendelea kukarabati na tunaenda vizuri. Tukifika *TANROADS* tuna maombi ya barabara ya lami kutoka Hungumalwa – Ngudu – Bukwimba – Magu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni awamu yangu ya tatu. Miaka 10 mimi naongelea hili suala. Miaka 10 naongelea suala la barabara ya lami wananiambia tumeweka kwenye utaratibu, tukipata fedha tutaanza. Sasa lini watapata fedha miaka 10 nipo hapa naongelea hili suala moja? Hata jana nashukuru Mbunge mwenzangu wa Sumve wa Wilaya yetu ameongelea hili suala ni tatizo. Tumeiomba hii barabara kwa miaka mingi sana tatizo ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tena nitaongelea hili suala limekuwa ni kama kero. Miaka mitatu iliyopita tukaambiwa wanajenga kilomita 10. Mwaka mzima umepiata hakuna kilichojenjwa, tena wakasema kilomita 10. Tumekaa kwenye *Road Board* ya Mkoa wa Mwanza, Mkoa wa Mwanza umeielekeza *TANROADS* kwamba, nendeni mkaanze kujenga hii ndiyo *priority*

ya Mkoa wa Mwanza. Meneja *TANROADS* wa Mkoa wa Mwanza akachukua taarifa hiyo akasema anakwenda kuifanyia kazi, mpaka leo hakuna majibu, zaidi ya *RC* wanne wameshabadilika maagizo ni yaleyale, sitasema Mawaziri wangapi wamebadilika lakini maagizo ni haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka miwili iliyopita Makamu wa Rais alifanya ziara Wilaya ya Kwimba, tulizungumza nae pale Hungumalwa akaagiza kwamba, *TANROADS* mwambieni Waziri mwenye dhamana aje hapa Kwimba aangalie tatizo la barabara hii. Mtu wa *TANROADS* akasema hadharani ndiyo Mkuu nimesikia. Mpaka leo sijamuona Waziri kuja kututembelea kujibu hoja ya Makamu wa Rais, maana yake ni dharau! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala kwa kweli limekuwa ni kero kwa wananchi wetu wa Kwimba, tunaomba mara hii Mheshimiwa Waziri wa Fedha yupo na wao wanasema hawana fedha. Sasa yeye atujibu hata mwenyewe alishaahidi huko nyuma kwamba, kuna fedha ya mradi fulani inafika tutapeleka fedha kwenye mradi huu tunaanza, tunasubiri majibu yake leo. Waziri wa Ujenzi na yeye yupo anatusikiliza hapa Mheshimiwa Bashungwa tunakutegemea utusaidie, utukomboe kwenye suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine tuna barabara ya kutoka Ngudu – Jojiro – Mabuki ni kilomita 21 barabara inayounganisha Wilaya kwenda kwenye Makao Makuu. Ni Wilaya peke yake ambayo haijaunganishwa na lami. Nawashukuru wameanza kilomita tatu angalau mkandarasi yupo barabarani anaanza kujenga lakini tunaomba ipo ndani ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi, hiyo barabara inatakiwa ikamilike. Tuna miaka miwili tunaenda mwaka wa 2025 kwenye uchaguzi, tunasemaje kuhusu utekelzaji wa hiyo ahadi tuliyoitoa kwa wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ningependa kuzungumza ni kwamba kwenye Mfuko wa Jimbo tumeletewa fedha kutoka Februari, tumegawa fedha hazijafika kwenye benki. Wale Watendaji wa Vijiji wanaenda benki wana-*bounce,* wanarudi wanasema Mbunge hakuna fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwezi wa Saba hapa tunanza kwenda Majimboni, tunaendaje huko? Hizo fedha tulishazigawa na hazijafika huko, tunategemea tutapata maswali tutajibu nini? Tunaomba angalau Mheshimiwa Waziri wa Fedha hizi fedha zimefika wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ningependa kuongea la ujumla ni kwamba niwapongeze Serikali kwa mradi wa mwendokasi Dar es Salaam ni mradi ambao ni mzuri sana wanaujenga kwa fedha nyingi sana, milioni ya dola wanazitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kushauri Serikali, hamuwezi mkajenga mradi mkauendesha wenyewe, hizo barabara mmezijenga mimi, ningewashauri watangaze tenda, watanzania ambao wana uwezo wa kuleta mabasi 50 na kuendelea makubwa yanayofanana na ya mwendokasi, mtu awekeze mabasi 50 mapya na kuendelea aje atumie barabara zenu aweke barabara *private*. Mtu akitaka kupanda basi zake atapanda ata-*charge* pesa yake, ili mradi huduma ipatikane. Tumeweka miundombinu Dar es Salaam yote imechafuka kwa sababu ya mwendokasi lakini hakuna mabasi. Barabara zipo tupu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningeshauri sana Serikali isitegemee kununua mabasi itoe kibali wafanyabiashara wa Tanzania wapo, wanunue mabasi 50 na kuendelea, watumie zile barabara kutoa huduma. Sisi tunachotaka ni huduma ipatikane kwa wananchi wa Dar es Salaam, sasa hivi mnajenga barabara lakini hakuna huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina machache hayo ya kusema nashukuru sana, naunga hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, jiandae Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, jiandae Mheshimiwa Abubakari Asenga, jiandae Mheshimiwa Komanya.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Niende moja kwa moja kwenye hoja kwa sababu nikishasimama mimi hiyo saa inakosa *speed governor. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kusema hivi, kuna changamoto moja ambayo lazima tuifahamu kwamba, bajeti yetu siyo kubwa ni ndogo sana, bajeti ya nchi jirani na kwetu Kenya ui-*convert* kwa *Tanzanian Shillings* ni trilioni 77. Bajeti ya Uganda nchi ambayo ni ndogo na kulinganisha na sisi ni trilioni 50 nukta *something* za Tanzania, bajeti yetu ni trilioni 49, kwa hiyo tuko nyuma licha ya kwamba, nchi yetu ni kubwa sana na licha ya kwamba watu wetu ni wengi sana, idadi ya watu ni kubwa, lakini bajeti yetu ni ndogo. Ni ndogo kwa sababu, bajeti inatokana na mapato. Sasa kama mapato hatujakusanya ya kutosha ina maana basi ni lazima tujifunze tujue namna gani tutatumia vizuri, tubane matumizi, ili iweze kutosheleza kwa namna yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, ukichukua uwiano wa bajeti ya wenzetu Wakenya kwa *Tanzanian shillings* kwa uwiano wa mwananchi mmoja mmoja, wastani ni shilingi 1,400,0000. Ukiangalia hii ya Uganda ni shilingi 1,100,000 ya Tanzania ni shilingi 750,000 tu basi, kwa kila mtu wastani wake. Kwa hiyo, shilingi 750,000 ni kidogo sana ukichanganya kila kitu; uendeshaji wa Serikali, huduma za jamii, ukiweka kulipa madeni, yote iko kwenye shilingi laki saba, wastani wa kila mtu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni fedha ndogo na ni lazima tusibweteke kwamba, imeongezeka kwa asilimia 11, asilimia 12, bado inatakiwa iongezeka zaidi, ili iweze ku-*catch up* na ukilinganisha kwa *square kilometre* tulizonazo sisi tunaonekana ni duni sana. Kwa hiyo, ninataka niseme kwamba, hilo ni jambo la ku-*address* na ndiyo sababu ninaamini kwamba, nadharia wanayokujanayo ya kwamba, tutumie vizuri bajeti na hiyo bajeti tuitumie kwa kuweka, ile ambayo mwenzangu amesema ni, *monitoring and evaluation* ifanyike vizuri na kwa *KPIs* hizi zinawekwa, kama kweli zinawekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini *KPIs* haziwezi kufanya kazi kama hatuna mipango ambayo ni *SMART*. *SMART* maana yake ni *Specific, Measurable, Attainable, Realistic and Time Bound* na ina *Time Bound*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano ukiangalia hii wanasema Barabara ya Handeni – Kiberashi – Kiteto – Mtoro mpaka Singida ni Barabara ya kilometa 433. Sasa kama hujaiwekea *specific target* kwamba, Mwaka huu 2024/2025 kwenye hii pengine tutajenga kilometa 50 na mtu aone kwamba, anaweza akazifikia na ukazitengea fedha, hatutafika mbali. Utamwekea mtu *KPI* ya namna gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, *KPI* haiwezi kufanyika bila kuwa na mipango ambayo ni *smart* na *smart* ni *framework* ambayo inatumika kila mahali. Ninaamini kwamba, watu wetu wa Tume ya Mipango wataendelea kuangalia hilo suala na kuhakikisha kwamba, kila barabara ikiainishwa basi tunajua mwaka huu itajengwa kiasi gani na siyo kuainisha tu, toka mimi niingie hapa Bungeni ziko kwenye mpango. Hazijaisha na hatuambiwi zimejengwa kiasi gani, lakini zinajirudia tu, hazitakaa ziishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwenye suala la mpango. Mimi nasema ukweli ni kwamba, kwa hali ilivyo tete kwenye Soko la Kifedha na Mitaji ya Kimataifa sasa hivi, kukopa ni kama ku-*commit suicide* kwa sababu, riba ni kubwa sana zinafika mpaka asilimia 12, asilimia 13 kwa dola, siyo kwa shilingi. Hiyo ni riba kubwa sana, siyo wakati mzuri wa kukopa kwa hiyo, lazima sasa tujue kwamba, pengine tunge-*focus* kumalizia hii miradi ambayo imeshaanza na ambayo inatakiwa sasa itupeleke kwenye Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 tukiwa tunasema kwamba, angalu tumefanya kidogo kwenye ile miradi ambayo tulipewa na tukaenda kuitangaza huko kwenye majimbo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ninataka nizungumzie ni hili ambalo wenzetu wamezungumza, la uhaba wa dola. Mimi ni mtaalamu wa mambo ya fedha kwa hiyo, nisipolizungumzia nitakuwa sijatenda haki. Ukweli ni kwamba, kuna

njia mbili, njia tatu za kukabiliana na uhaba wa bidhaa yoyote na dola ni bidhaa tu, wala siyo kitu cha ajabu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ni kwamba, una-*control,* unafanya *exchange control*. Ukifanya *Exchange Control* maana yake una-*allocate administratively,* tena una-*allocate* ile dola iliyopatikana kwa ile mitaji ambayo unaona ni *priority*, ile mingine basi haipati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hiyo ni *distortive* kwa sababu ni kwamba, kuna wengine ambao wangetumia ile dola kwa tija zaidi kwa sababu, wana miradi mizuri zaidi kuliko hii ambayo wewe unafikiria ni mizuri. Kwa hiyo, *Administrative Allocation* au hizo *Exchange Controls* ambazo zilikuwepo tukaondokana nazo miaka hii ya 1990, siyo njia sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, njia nyingine ni hiyo ambayo wenzetu wote hapa tunasema tuongeze uzalishaji wa huduma na bidhaa za kuuza nje, lakini hiyo ni *structural measure*. Yaani unachukua *the structural policies,* hasa za kibajeti, ili kuibua au *rather* ku-*debottleneck production problems* kwenye sekta zetu, kama ni ruzuku kwenye mbolea na kadhalika, lakini hiyo inachukua muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ni lazima isaidiwe na *incentive* ya kibei na bei maana yake ni kwamba, dola inauzwa kwa shilingi chache sana. Bei ya dola ni ndogo mno hapa kwetu ndiyo sababu inakuwa adimu, kila mtu anataka dola. Mtu ana-*import,* ananunua dola kwa bei chee, halafu ikifika hapa ina maana kwamba, hata hizi *products* zetu hapa ndani haziwezi ku-*compete* na *imported goods* kwa sababu ya dola iko *mispriced. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi ninafikiria hiyo *question* ya *debottlenecked supply is okay,* lakini *it will take some time*. *Meanwhile* ni lazima tukubali tutumie *demand management tool,* ambayo ndiyo hiyo *exchange rate,* kuiruhusu na ninashukuru kwamba, Benki Kuu imefanya, imeruhusu na imepunguza kidogo makali, msererko huo wa *around 11 percent*. Tunashukuru Wizara

imeweza kufanya hilo, lakini unaona kwamba, bado iko kwenye *equilibrium*. Hatujawa kwenye *equilibrium exchange rate so far* na ndiyo sababu, unaona kabisa dola zile hazipatikani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitoa mfano huu juzi, Jumamosi, nikasema kwamba, pale kwa wenzetu majirani, wao waliruhusu *exchange rate* ika-*overshoot* ikafika 160 kutoka *around 90*. Sasa, baada ya muda kwa vile waliiruhusu ikafanya *adjustment* yenyewe, imerudi sasa imeanza ku-*appreciate* inarudi kule ilikokuwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hii ya kwetu ingeruhusiwa, ingekwenda kule halafu *exporters* wakaona faida zaidi kwa hiyo, wangeamua kuzalisha na kuuza nje zaidi kwa ushindani mzuri. Kwa hiyo, *gradually* ile *supply* ina-*pick up* na inapo-*pick up* basi ina-*equilibrate* na *exchange rate* inashuka ina-*appreciate* tena, inarudi pengine inaweza kuwa shilingi 2,300 siwezi kusema.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nasema kwamba, bila kutumia hiyo ushindani wa uchumi wetu haupo. Kwa sababu, tunashindanisha uchumi na uchumi na kitu kimoja kinachoshindanisha ni *productivity* na *efficiency* na kingine ni *exchange rate*. Ndiyo kitu kinacholeta uwiano kwenye uchumi na ndiyo uchumi shindani. Kama uchumi ni shindani na wewe unaubana hautafika mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, narudi kwenye suala zima la ukusanyanji wa mapato ya *TANAPA, Ngorongoro* na *TAWA*. Sasa sisi tunaona kwamba, pengine ni vizuri kwa sababu, hawa wanafanya biashara kusema kweli, wanafanya biashara siyo *TANAPA* wanacheza. Wanafanya biashara na siyo watu wa kusubiri kwamba, wapate migao kama hii inayotoka Hazina kwenda kwenye Wizara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninafikiri kwamba, ili waweze kuwajibika *internationally,* waweze kuwajibika kwa kufuata *accounting standards* za Kimataifa, tuweze kuwapima na waweze kupewa malengo. Msajili wa Hazina anasema anajua,

anawawekea malengo na ufuatiliaji na bado haohao wana bodi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninafikiri kwamba, tumuombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha ajaribu kuliangalia hili jambo, arudishe ukusanyaji wa mapato ya haya mashirika ya kibiashara yarudi kwenye mahali pake. Ni pale ambapo wanakusanya na *usually* mapato yanaendana na *expenditures* na baadaye kunakuwa na *surplus*, *then surplus can go away out there*. Kama inakuwa ni ngumu sana kufanya yote kwa mpigo, amefanya kwa *TPA* kwa hiyo, tunaomba tena afanye na...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Dkt. Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** …mojawapo halafu baadaye aende *gradually,* lakini siyo lazima afanye yote kwa mpigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho niseme kwamba...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kimei, ahsante.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tabasamu amerudi. Ataanza yeye halafu atakuja Mheshimiwa Manyinyi.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Mimi ninaanza mchango wangu katika eneo la kubana matumizi. Ni kwamba, kwa miradi yetu yote tuliyonayo katika nchi hii na bajeti yetu hii ya shilingi trilioni 49, kama hatuwezi kubana matumizi, yaani Serikali haiwezi kubana matumizi, bado ni hatari kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba, sehemu ya kwanza ya kubana matumizi ilikuwa ni kuhakikisha magari yetu yote ya

Serikali yanatumia gesi, yafungwe mitambo ya gesi. Hawa wenzetu, kupitia *TEMESA*, wafanye kazi hiyo au wataalamu wapelekwe India ambako sisi tulikwenda kujifunza jambo hilo tukaliona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakitoka na *knowledge* hiyo wakaja nayo Tanzania, kwa kupitia mikoa yetu sisi ya Tanzania, kote kule watakuwepo mafundi watakaofanya kazi hii kwa gharama nafuu, ili magari yetu ya Serikali yaanze kutumia mfumo huo wa gesi. Halafu na magari yetu sisi, ya watu binafsi, yaanze kutumia mfumo wa gesi, tutaokoa sana matumizi katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakupa mfano mmoja tu; ni kwamba kama unajenga nyumba wewe mwenyewe tu binafsi, wewe ni mjenzi unajenga nyumba yako ya kuishi lakini unataka ule vizuri, unataka kula kuku, unataka kula nyama na unajenga nyumba, hiyo nyumba haiwezi kwisha. Kwa sababu, kuna wakati ni lazima upunguze gharama, upunguze matumizi, gharama ya familia kwa sababu, unafanya kazi ya ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo hii sisi tuna miradi mikubwa, miradi ya reli, miradi ya meli, miradi ya barabara na bado tumekutana tena na Kimbunga Hidaya kikatuletea mvua kubwa, lakini bado tunatembelea magari ya gharama kubwa, kitu ambacho ni hatari kubwa sana kwa nchi. Katika eneo hilo mimi ninashauri, kwanza tunayo magari mabovu katika halmashauri, tunayo magari mabovu Serikalini; mimi ninamshauri Waziri wa Fedha kwa kumtumia Mfilisi wa Serikali, haya magari yote yanatakiwa kuuzwa kwa sababu, hizo ni pesa. Zipo mpaka meli ambazo zimechakaa, zipo feri zimechakaa, ukienda kila maeneo vyombo vya Serikali vimekaa ni lazima vile ambavyo vimepitwa na muda wake viondoke. Ninafikiri huo ndiyo utakaokuwa ni mpango wa kwanza wa kubana matumizi ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine ambayo sisi tunataka kusaidia kuishauri Serikali ni namna ya kupata vyanzo vipya vya mapato. Chanzo cha mapato ambacho kinatumika na

Serikali kwa sasa hivi cha kuongeza kodi bado ni hatari kubwa sana kwa maisha ya wananchi. Yako maeneo ambayo kodi ingeingia kwa ndani, inafichwa tu ndani ambako mwananchi anakutana nayo haoni kama amelipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yako maeneo ambayo yamependekezwa, mimi ninaunga mkono kabisa. Yamependekezwa katika mafuta, hayo yote mimi sipingani na Wizara ya Fedha. Ni kwamba, ni lazima tukusanye, lazima tupate kodi tuendeshe nchi yetu. Tujiondoe katika mikopo mikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ambacho ninataka kumshauri Mheshimiwa Waziri ni, je, kinachokusanywa kinaingia katika mfuko wa Serikali? Hiyo ndiyo alama ya kujiuliza. Ni kwamba wananchi wanalipa kodi, kule kwenye Halmashauri kule wananchi wanalipa ushuru, je, huo ushuru wote unaingia katika Mfuko wa Hazina au Mfuko wa Halmashauri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa huko ndiko kunakotakiwa kuangaliwa kwa kiwango kikubwa. Ni kwamba tukiangalia wakusanyaji, hizo *control number* zinazotolewa, je, zinaingia moja kwa moja Serikalini? Kwa sababu, sasa hivi kila mnavyokua na teknolojia inavyopanda na watu ndiyo wanatengeneza mifumo. Wanakuwa katika majumba yao, ikitolewa *control number* haiingii katika *control number* ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni jambo linalotakiwa kuchunguzwa sana. Watu wetu wa usalama, watu wetu wa fedha, basi walichunguze sana jambo hili kwa sababu, minong'ono na manung'uniko iko kule. Tunaona kwenye nchi za wenzetu, hawa watu wa namna hiyo wanaokaa na *laptop* wanaingilia mifumo ya fedha ya Serikali, kwenye nchi nyingine wapo, wanakamatwa wanapelekwa Mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna watu ambao wanasafiri, wanaweza wakasafiri hata kwenye ndege. Akaanza kuangalia kwenye *laptop* yake, yeye anakwenda kukaa kwenye kiti anaangalia ni sehemu gani kuna dola katika begi, inampa

*alarm*. Sasa, kama imefikia hatua hiyo, basi na sisi ni lazima tuwe makini sana katika mifumo ya ukusanyaji wa fedha. Hapo tunaweza tukafaulu sana katika mapato yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba, barabara zimeharibika. Miundombinu inatakiwa kurekebishwa kuanzia kwenye vijiji na kwenye miji yetu, lakini pamoja na miundombinu kuharibika mpaka barabara ambazo ni *trunker* na zenyewe zote zimeharibika. Ni kwamba, ni lazima tuhakikishe tunapata chanzo cha kutengeneza hizi barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kusaidiwa na mjomba, sisi Watanzania ni lazima tujifunge mkanda tutengeneze barabara zetu. Ndugu zangu Mheshimiwa Rais anaumiza kichwa sana, ni wapi atapata pesa, kwa ajili ya kutusaidia sisi Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ambacho ninapendekeza mimi ni kwamba, maeneo yote ambayo yanakuwa ni chanzo cha kupata pesa, basi kila mtu ni lazima afunge mkanda. Pesa zikusanywe kule na Mheshimiwa Waziri wa Fedha akutane na makundi yote maalumu. Makundi yote yanayofanya biashara, makundi ya machinga, makundi ya wajasiriamali na makundi ya wafanyabiashara wakubwa, basi tukae kujadiliana ni maeneo yapi ambayo sisi tunaweza tukapata chanzo cha kupata pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ninataka nilizungumzie hapa ni suala la mikopo. Ili tuweze kutengeneza uchumi wa nchi yetu tunamuomba sana Waziri wa Fedha ahakikishe riba zinapungua katika benki zetu, hakuna jinsi nyingine. Kwa hali ambayo tunataka tupate walipakodi wengi ni kwamba, ni lazima tupunguze masharti ya fedha Benki Kuu, ili wakopaji wawe wengi halafu tuweze kutengeneza uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu, nchi hii ule mfumo kwamba, kuna wafanyakazi na wakulima halafu kundi la wafanyabiashara likatolewa, basi huyo mkulima ataumia na huyo mfanyakazi ataumia. Kwa hiyo, hayo ni maeneo ambayo tuone ni

namna gani wafanyabiashara wanaweza wakatafutiwa fursa, ili waweze kulipa kodi, waweze kufanya biashara na walipe kodi kwa ulaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo ninataka kuzungumza hapa ni kuhusiana na faini. Faini iliyopendekezwa tunamuomba sana Waziri wa Fedha, ni kubwa mno, labda wafanyabiashara wanakwenda kufunga kabisa maduka yao. Kwa sababu, usipotoa risiti ukapigwa faini ya shilingi milioni 15, duka lina mtaji wa shilingi milioni 7 inamaanisha kwamba, tayari wewe unatakiwa uende tena, yaani unalikimbia duka tu. Ni kwamba, watu watakimbia maduka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliona Mwaka 1997 lilipokuja tu suala la *VAT* zaidi ya maduka 7,000 yalifungwa na watu wakahamia Malawi, wakahamia Zambia. Tukabakia sisi kukaa kwa sababu, tunaipenda nchi yetu. Sasa kwa hii faini itakayoanza Tarehe Moja, faini ya shilingi milioni 15, Mheshimiwa Waziri wa Fedha tunawaomba sana. Jamani Waheshimiwa Wabunge, kama kweli tutaipitisha hii faini ya shilingi milioni 15, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana, lakini suala la hii faini ninaogopa sana kuunga mkono hoja kwenye hii faini kwa sababu, hata mimi nitakuwa ni miongoni mwa watu watakaojeruhiwa. Kwa sababu, risiti tunatoa, lakini unajikuta mtu mmoja una maduka sita sasa kwa hiyo, inamaanisha kwamba, watu wataishia gerezani. Mfanyakazi wako asipotoa risiti na wewe sasa hivi uko hapa Dodoma, Bungeni, tayari unaingia katika matatizo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mheshimiwa Asenga jiandae. Mheshimiwa Komanya jiandae, Mheshimiwa Mheshimiwa Bulaya jiandae. *(Makofi)*

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, ili na mimi niweze kuchangia kwenye hii Hotuba ya Wizara ya Mipango pamoja na Wizara ya Fedha. Awali ya yote ninachukua nafasi hii, kwanza kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi yake nzuri ambayo ameendelea kuifanya na ninyi mkiwa kama wasaidizi wake katika kuwahudumia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mchango wangu kwa leo utagusa pande zote mbili na ningependa nianze na Mheshimiwa Prof. Mkumbo, Waziri wa Mipango. Kwetu sisi, kama Wabunge, maadamu kazi yetu ni kushauri mimi ninapenda nishauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii kwenye upande wa nishati tunayo ambayo tunatumia kwenye upande wa kuzalisha umeme, tunatumia gesi lakini vilevile tunatumia maji. Sasa kwenye upande wa maji maana yake ukichukua Bwawa la Julius Nyerere, ukachukua Mtera, ukachukua Kihansi na vyanzo vingine vyote vya maji naamini kwamba kabla ya kufika mwisho wa mwaka huu tutakuwa tunazalisha *Megawatt* zisizopungua 2,500 kwenye upande wa maji peke yake lakini mahitaji yetu au matumizi yetu mpaka kufika mwisho wa mwaka huu tutakuwa tunaelekea labda sana sana *Megawatt* 2,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa maneno mengine Mheshimiwa Waziri, ni kwamba upande wa gesi ni kwamba tunaweza kuiondoa kwenye upande wa uzalishaji wa umeme kwa sababu uki-*compare* katika hivyo vyanzo viwili maji ni nafuu zaidi kuliko gesi. Kama hivyo ndivyo sasa hii gesi hebu tuitafutie mahali ambapo tutaona inaweza ikatusaidia. Leo Mheshimiwa Waziri, ukiangalia pale Dar es Salaam, Mtwara na Lindi tunayo *chance* nzuri ya kutumia gesi kama *power* ya kuendeshea magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hivyo ndivyo kazi yetu kubwa ambayo tulipaswa kufanya sasa hivi ni kuwahamasisha wananchi wa hiyo mikoa mitatu kwa kuhakikisha kwamba kwanza tunawawekea vivutio vya kuwafanya waweze ku-*convert* magari

yao yaweze kutumia gesi. Hiyo ni pamoja na kuondoa ushuru wote ambao unatumika kwenye ile *conversion* ya *gas to power*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo watu wengi zaidi watatumia gesi na kwa sababu tunayo maji ya kutosha basi tunaweza kupata, magari ya hiyo mikoa mitatu yapo tayari sasa wengi zaidi wanaweza kuingia kwa kutumia gesi. Kwa kufanya hivyo maana yake ni kwamba kwanza itatusaidia sasa kupunguza matumizi ya mafuta ya *diesel* pamoja na *petrol.* Kama tutapunguza mafuta ya *diesel* na *petrol* maana yake ni kwamba badala ya kutumia fedha nyingi za kigeni kwa ajili ya *importation* ya *diesel* na *petrol* tutakuwa na gesi ambayo tunatumia fedha za kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya muda sasa leo maana ni kwamba nasema hilo kwa sababu Mheshimiwa Waziri, umesema leo unashauri kuongeza ushuru kwenye gesi wakati gesi yenyewe ambayo tunaongeza ushuru tunategemea ni gesi ambayo ni vituo vitatu peke yake ndiyo vilivyopo; kile cha Ubungo, kile cha *Airport* na pale *TAZARA*. Sasa leo vituo vitatu tunavitungia sheria ya kusema kwamba tuweze kuvi-*charge* matokeo yake ni kwamba hata wale ambao tungewavutia wengi wakaingia humo baadaye mwaka kesho sasa tukaanza kuwatoza tukapata fedha za kutosha matokeo yake ni kwamba hawatafanya ile *conversion* kwa sababu gari moja dogo siyo chini ya shilingi milioni mbili kuli-*convert*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mtu anajaribu ku-*weigh* aangalie gharama za ku-*convert* halafu wakati huo *diesel* pamoja na gesi vinalingana matokeo yake ni kwamba hawataenda huko wataendelea kubaki kwenye *diesel* na *petrol* halafu tutaendelea kuwakosa na huku maji tunayo na tuna umeme wa kutosha na gesi ipo. Kwa hiyo matokeo yake ni kwamba tutaendelea kutumia fedha za kigeni kwa ajili ya *importation* ya *diesel* na mafuta ya *petrol*. Kwa hiyo huo ni ushauri wangu kwenye upande huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande mwingine hili ni kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Wote tunatambua kwa nchi kama zetu hizi changa tatizo kubwa tulilonalo ni tatizo la ajira, kwa hiyo

watu wetu wanahitaji wapate ajira zaidi. Leo ukizungumza ajira, tutapata ajira kwenye upande wa kilimo lakini tutapata ajira kwenye upande wa viwanda. Kwa hiyo lazima bajeti yetu ielekezwe upande huo tuone namna gani kilimo kinaweza kikachochea katika watu wetu kupata ajira lakini vilevile pamoja na viwanda ili tuweze kupata hizi fedha za kigeni na tuache kuwa wategemezi zaidi kwa kila wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hivyo ndivyo, ndiyo maana leo tunashukuru kwamba tunavyo viwanda vingi kama viwanda vya *cement*. Leo tumefika mahali mpaka viwanda vya sukari na vyenyewe vimekuwa vingi. Jana Mheshimiwa Waziri, niliweza kugusia kidogo kwamba leo tunapozungumza kwa mfano mimi nakumbuka siku moja tulikaa na watu wa *CTI* wakaweza kusema, mwaka juzi kulikuwa na upungufu wa sukari kwa tani 30,000. Mwaka jana upungufu uliyojitokeza ulitokana na *El Nino*, mwaka huu kwa mujibu wao *CTI* wanasema wanatarajia kuwa na tani zisizopungua 520,000 mpaka 550,000. Mahitaji yetu ni 480,000 mpaka 500,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hivyo ndivyo kumbe sasa hata hivi viwanda vyetu navyo sasa vimefika mahali ambavyo tunajitosheleza kwa sukari lakini vilevile tunaelekea sasa ku-*export* ili tupate fedha za kigeni. Kama hivyo ndivyo sasa ushauri wangu kwa hapo nini kifanyike, maana ulileta hapa Muswada wa *NFRA* kuweza kuagiza sukari. Mimi nikasema hivi, badala ya *NFRA* kuagiza sukari wao tuwape tu kazi moja. Kwanza, Mheshimiwa Waziri, tukienda kwenye hali halisi kazi tu ya kununua mazao ya wakulima mashambani yale mahindi imewashinda.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunafika mahali tunasema hebu tuwaongezee na kazi yaku-*import* ambapo tusipoangalia ni kwamba hata hivyo viwanda tulivyonavyo tutaendelea kuviua na ushahidi Mheshimiwa Waziri upo wazi kwamba kwa mwaka huu peke yake tulisema kwamba *gap sugar* ni kati ya tani 60,000 mpaka 100,000 lakini tumetoa vibali vya tani 410,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tukisema kwamba *NFRA* tuendelee kuwapa kazi hiyo matokeo yake hata hivi viwanda

ambavyo tulipaswa kuvilinda tutashindwa kuvilinda. Tukishindwa kuvilinda na vikafa maana yake ajira kwa wale watu wetu tumeua lakini hata fedha za kigeni ambazo tulikuwa tunazinusuru basi tena tutaanza kurudi kule kule kwenye ile habari ya ulanguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nilichokuwa nakiomba au naishauri Serikali kwamba kama tunadhani wale watu wenye viwanda wana tatizo la *cartel*, ujanja wa kufanya ni mmoja tu na kama tunadhani *NFRA* wanao uwezo wa ku-*import* sukari, wale wenye viwanda wafanye kazi moja; wazalishe na ile sukari yote wanunue *NFRA* na *NFRA* wasimamie namna yaku-*distribute*. Kwa kufanya hivyo hata kama kuna *gap* linabaki, lile *gap* lililopungua basi *NFRA* waweze kupata nafasi yaku-*import*. Tofauti na hapo mimi naamini kuna siku moja mtakuja kuniambia baada ya viwanda vyetu kuwa vimekufa tunarudi kule kule tulipotoka. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nadhani hilo nilidhani niweze kulishauri kama tutaona ni jema basi tunaweza kulifuata na...

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo tunadhani kwamba tutakuwa tumeendelea kulinda viwanda vyetu na hata viwanda vingine. Hii ndiyo itakayotufikisha mahali tukapunguza tatizo la ajira kwa ajili ya watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ni hivi viwanda vyetu vya *SIDO*. Viwanda vya *SIDO*...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Manyinyi, kengele ya pili hiyo.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Karibu Mheshimiwa Asenga, Mheshimiwa Komanya na Mheshimiwa Bulaya wajiandae.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii ya mimi kuchangia pia Bajeti Kuu ya Wizara ya Fedha na Mipango. Nami naanza kwa kumuomba Mwenyezi Mungu atujaalie, atusaidie kutuepusha na majanga katika nchi yetu ili mipango yetu mizuri iliyosomwa na mawaziri wetu na mipango yetu mizuri tuliyonayo iweze kutimia maana yake majanga nayo huwa yanavuruga sana bajeti za Serikali na bajeti za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nimesimama hapa na mimi naanza kuchangia kwa kushukuru Serikali ya Awamu ya Sita ya Chama cha Mapinduzi chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na mawaziri wetu wote ikiwemo Mheshimiwa Waziri wa Fedha chini ya Mheshimiwa Dkt. Mwigulu kwa sababu yale yote makubwa na mazuri tunayosema tumeyafanya na tunawaambia wananchi wetu leo kwa vyovyote zile fedha lazima zitakuwa zimepita Wizara ya Fedha zikaja kwenye halmashauri zetu na zikaja kwenye mikoa yetu ndiyo maana tukapata maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa tathmini yangu kwa kule kwetu Kilombero tuna asilimia zaidi ya 80 ya kutekeleza mambo makubwa ambayo Chama cha Mapinduzi iliahidi na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, amesimamia kutupatia fedha hizo. Kwa uchache kidogo nataka ku-*mention* mambo makubwa tuliahidi, tuliomba tupeni dhamana wananchi tunavyoenda kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa wananchi wanavyotaka kuhukumu Chama cha Mapinduzi na kuhukumu Serikali yetu katika uchaguzi lazima wazingatie mambo yale ambayo tumeyaahidi na tumeyatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza na Mheshimiwa Waziri wa Fedha yupo hapa ana barabara. Mimi nilikuwa sijui kama Wizara ya Fedha nayo ina barabara zake lakini barabara yangu ya lami ya Ifakara - Kidatu ipo chini ya Wizara ya Fedha, chini ya Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na Naibu wake pale

wanasimamia kama *contracting authority* wa barabara ile kilometa 67 sasa hivi imebakia kama kilometa moja kukamilika. Nasisitiza Mheshimiwa Waziri nimekuomba mara kadhaa ukakague barabara hii na Daraja kubwa la Ruaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ni uchumi mkubwa sana wa Kilombero na Mkoa wa Morogoro. Tunavyotaka kujenga uchumi kufungua Mkoa wa Morogoro kutokea Lindi kupitia Mahenge, kwenda Songea kupitia Malinyi na kwenda Njombe kupitia Mlimba barabara hii ilikuwa ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata Hospitali ya Wilaya katika miaka hii mitatu, minne ambayo tunaelekea kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Tumepata miradi ya maji shilingi bilioni 45. Zile fedha anazofanya kule kwenye miradi ya miji 28 lazima zimepita Wizara ya Fedha. Kushirikiana na madiwani na viongozi wa vijiji tumejenga zahanati 12, sekondari za *O level* 12 na *advance* sekondari tano. Sasa hivi tuna mkandarasi wa lami ya Ifakara - Mlimba na yupo *site* na tunaomba barabara ya Ifakara kwenda Malinyi ianze kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema Daraja la Ruaha karibu ya shilingi bilioni 10 linajengwa na linakamilika. Tumepata shilingi bilioni 500 kujenga kiwanda kipya cha sukari ambacho wakulima walikuwa wanalalamika miwa yao inabaki. Tunatarajia kupata *substation* na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mheshimiwa Doto Biteko, alikuwa pale juzi. Ameenda kuzindua mradi wa *substation* shilingi bilioni 23 tumepata kupitia Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Tumepata Mahakama mpya ya Wilaya, tumepata Stendi mpya ya Wilaya, tumepata Soko jipya la Wilaya na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, alikuwa pale juzi amethibitisha hayo ninayoyasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi hapa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi amenipa shilingi milioni 802 tumeshaanza na *OCD* na Mheshimiwa *DC* Dunstan Kiyobya, Kamati ya Usalama Wilaya ya Kilombero inasimamia ujenzi wa kituo kipya cha polisi cha wilaya, nani kama Dkt. Samia Suluhu Hassan? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejenga vituo viwili vya afya na tumejenga soko la samaki. Sasa hivi tumepewa fedha kupitia Wizara ya Nishati na *TANESCO* tunaboresha tuta la Ifakara kuondoa yale mafuriko ambayo mlikuwa mnatucheka nayo. Mheshimiwa Waziri, nakuomba tu kwamba fedha zile za tuta hazitoshi mtuongezee ili tuweze kujaza maji mengi katika Bwawa la Mwalimu Nyerere muweze kuzalisha umeme wa kutosha na tumepata lami za mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo hayo mazuri kuna changamoto nataka nizielezee kwa ufupi kabla sijaingia ndani ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri. Kila Mbunge hapa amesema na mimi nataka kusisitiza. Sisi tumepata mafuriko inawezekana tukawa namba moja nchi hii kwa ubovu wa barabara za mitaa. Tunamuomba sana Mheshimiwa Waziri, katika vipaumbele vya kwanza vya kupeleka fedha pelekea fedha *TARURA* waboreshe barabara za mitaa. Hali ya Jimbo la Kilombero Halmashauri ya mji wa Ifakara ni mbovu sana na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, alikuwa pale ameona, sisi mji wa Ifakara karibu wote ulipata maji. Kwa hiyo barabara zote zina mashimo na makalavati yameharibika tunaomba sana utusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mafuriko hayo wakulima wameathirika kiasi kikubwa sana (wakulima wa mua na wakulima wa mpunga). Tunaomba Serikali muangalie namna ya kupeleka mbegu na mbolea katika msimu ujao wa kilimo na namna gani ya kuwapa pole wakulima hawa. Sasa hivi mkulima anavuna gunia la mpunga shilingi 70,000; bei bado ndogo. Kama Serikali inanunua mazao mengine na hii *NFRA* inunue pia mpunga ili ikuze bei kidogo wale walanguzi waweze kupandisha bei kumpa mkulima bei ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna changamoto ya kusambaza umeme katika vitongoji. Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati amenipa vitongoji 15 lakini kazi ni bado. Tunaomba kufufuliwa kwa kiwanda cha *Mang'ula Mechanical & Machine Tools*. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, nimekuomba mara kadhaa, pale kuna nyumba kibao zipo Serikali imechukua kwa muwekezaji

imerudisha Serikalini. Kiwanda cha *Mechanical & Machine Tools* na vifaa vyake vyote vinaharibika tu pale havifanyiwi usafi. Tembeleeni pale; Mheshimiwa Waziri wa Fedha unavyotembelea barabara ya Ifakara Kidatu tembelea na kile kiwanda. Fufueni kile kiwanda kama mlivyofufua *Kilimanjaro Machine Tools* ili wananchi wetu wapate ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho katika changamoto ni bei ya sukari. Sisi pamoja na ukulima wetu wa miwa, sukari ikiadimika kama mwaka jana hatukuvuna mua kwa sababu ya mafuriko (mua umelowa hauvuniki) sukari imekuwa haba, kiwanda kimezalisha chini ya uwezo. Tumekaa kila sehemu tunapita Kilombero inazalisha sukari inawezekana namba moja kwenye nchi hii, hakuna mkakati wowote au mpango wowote kwa wananchi wa pale Kilombero kuuziwa sukari kwa bei rahisi. Tunanunua sukari shilingi 6,000 au 5,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana tunamlaumu Mheshimiwa Waziri Bashe leo kwa hatua alizochukua. Mimi nipo kwenye mkutano wa hadhara wa biashara na *DC* na Kamati ya Usalama, wananchi wanalalamikia sukari bei 6,000 kwa nini na sisi tunalima miwa? Ndiyo Mheshimiwa Waziri Bashe, anapiga simu *live* kwamba Kamati ya Usalama ya Kilombero iende ikafungue kiwanda ndiyo tunapata sukari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nasisitiza sana ni kwamba kama dhahabu yetu nyeupe ya sukari ni muhimu sana Serikali ikawa na mipango wakati inaadimika tukaipata kwa bei rahisi. Ukiniuliza mimi leo kipaumbele changu cha kwanza tuzalishe sukari ndani ya nchi yetu na ndiyo maana Serikali imekubali katika *25 percent* ya Kiwanda cha Illovo kukubaliana na muwekezaji kuwekeza shilingi bilioni 500 ili kiwanda kijengwe upya. Kiwanda kile kitatumia miwa ya wananchi ya kutosha na kitawezesha nchi yetu kujitegemea katika sukari; hicho ni kipaumbele changu cha kwanza lakini la pili; inapotokea changamoto kama msimu uliopita basi tupate sukari kwa bei rahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yako Mheshimiwa Waziri, nataka kusisitiza hapa na kusema nimeona umezungumzia

mambo ya uwekezaji na miradi mikubwa kama ya reli. Sisi Kilombero na Morogoro tuna mpango wetu wa reli ya Kidatu kuunganisha na Kilosa na wataalamu wametuambia reli hii mkiiunganisha itatusaidia kuweka kontena Bandari ya Dar es Salaam ikaenda mpaka Johannesburg South Africa; hichi ni kiungio muhimu sana cha uchumi. Nimeona kwenye kamati na nimeona kwenye bajeti kwamba mtatoa fedha hizo, Mheshimiwa Waziri tunakuomba reli ya Kilosa - Kidatu ipatiwe fedha. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwsiha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asenga, kengele ya pili hiyo.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Komanya, wajiandae Mheshimiwa Bulaya na Mheshimiwa Mkenge. Mheshimiwa Komanya.

Mheshimiwa Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Bajeti Kuu. Mimi naanza kumnukuu Mheshimiwa Rais alipokuwa akipokea gawio, ya kutoridhishwa na mwenendo wa ufanisi wa mifuko ya hifadhi ya jamii. Vilevile, akasema makosa ya wengine na akasema ikiwepo na Serikali tusiwaonee watumishi wa umma. Pia, amezungumzia uwekezaji usio na tija kwenye maeneo mbalimbali kupitia fedha za mifuko ya hifadhi ya jamii. Nashukuru mwenyewe ameliona, wengine tuliongea humu zaidi ya miaka sita hatukusikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru Kamati ya Bajeti kupitia ukurasa wake wa 87 wamezungumzia uwekezaji usio na tija na kuathiri mifuko. Hii ndiyo inasababisha leo watumishi wa nchi hii wanapunguziwa mafao yao kwa mkupuo. Tuliongea hapa tangu 2018 mnaleta sheria si kwa ajili ya kulinda mifuko, mnaleta sheria baada ya kujua mifuko ipo hohehahe na mnataka kuwadhulumu watumishi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 101 unasema eti umerudisha kikokotoo 40% yaani kama zawadi 40%. Watu waliokuwa wakichukua mafao kwa mkupuo kwa 50% na walikuwa wakiendelea kulipwa pensheni za kila mwezi kwa miaka 15, nyinyi vyote hivyo mmepunguza halafu mnasema eti lengo ni kuwasaidia watumishi wa umma wa nchi hii kwa pesa zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuangalie kiini, kiini mmeenda kuwekeza kwenye miradi isiyolipa na miradi ile inatengeneza hasara. Mimi nilitegemea mtasema mtaenda kulipa fidia kwenye zile pesa ambazo watu wameenda kuwekeza muweke kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii. Nilitegemea mtasema Serikali mnadaiwa zaidi ya shilingi trilioni mbili sasa hivi zile za *P1999* muwalipe ili waweze kufanya kazi zao vizuri na wataweza hata kujipangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunaweza kuwalipa zaidi hata ya 60% kama ambavyo wanafanya wengine. Halafu leo eti mnarudi mnasema 40% yaani kana kwamba mmefanya jambo kubwa. Leo mngekuwa ile mifuko ipo *stable* msingechukua pesa kwenda kuwekeza kiholela, leo ile mifuko ilikuwa ina uwezo wa kumlipa mtumishi hata 60% mafao kwa mkupuo na ilikuwa ina uwezo wa kumlipa kwa kila mwezi mfululizo hata miaka 18.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya umekuja umesema mnasimamisha eti mtalipa mpaka 2030, sasa 2029 mnalipa ninyi kama nani? Tumetunga Sheria 2018 imetaja wazi mwenye mamlaka ya kulipa wastaafu ni Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Ukienda kwenye Sheria ya mwaka 2018 kwa upande *PSSSF* Sheria Kifungu cha 6(3) kinaeleza mamlaka ya kulipa wanayo Mifuko. Ukienda *NSSF* kwenye Sheria ya mwaka 2018 Kifungu cha 3(2) kinaeleza wenye mamlaka ya kulipa mafao ni wastaafu yaani mnataka mvunje sheria kuficha makosa yenu! *Solution* siyo kuvunja sheria, *solution* ni kushughulika na kiini cha kuenda kulipa madeni, kushughulika na kiini kwenda kulipa fidia kwenye maeneo ambayo mmewekeza miradi isiyolipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu unasema eti unaleta 40% unalipa kwa *formula* ipi? ya 1 ya 580? Wenyewe hawataki, wanataka irudi *formula* ya 1 ya 540 kama ilivyo mwanzo. Hapa hakuna mnachomsaidia mtumishi hapa na wamenuna na wanasema achene kuwatisha Wawakilishi wao, haya mambo mnakaa wenyewe mnajifungia mnaamua bila kuwashirikisha, ndiyo maana leo mnaenda kuchukua mamlaka siyo yenu. Hizi pesa mnazosema mnalipa pelekeni wenyewe kwenye Mifuko walipe, walipeni madeni fanyeni Mifuko iwe *stable* ili siku moja watumishi wa nchi hii wanaoifanyia kazi kwa jasho na damu waamue leo tunachukua mafao yetu kwa mkupuo asilimia 70, inashindikana nini kama Mifuko ipo imara? Hilo nalisisitiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine nilikuwa nataka kuzungumzia hebu mkija kujibu hapa mtuambie hebu vipi hukusu *mortgage*? Maana mliiwekea kwenye Sheria, Kifungu cha Sheria Kifungu Namba 42 cha Sheria ya 2018 maana ile ilikuwa danganya toto. Wakati mnawa-*lobby* wakubali na asilimia 33 inatekelezeka? Maana najua Kanuni tayari za mwaka 2024, *GN*. tayari imeshatoka namba 140 tangu tarehe 8 Machi, 2024 kiko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mliwaambia tutawapa asilimia 33 halafu mtakuwa mna uwezo wa kwenda kukopa kupitia pesheni zenu muweze kujenga nyumba ili hata mkipata kidogo muwe na uafueni mna maeneo ya kuishi. Hizi hela zingine mtazitumia kuandaa Maisha! Leo hakuna mtu pale anaye ruhusiwa kwenda kukopa. Kwanza, watakopa lakini vilevile riba, haya mtu ambaye anapata milioni 17 anaenda kukopa nusu ya hapo atajenga nyumba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jamani hawa Wafanyakazi siyo watoto wadogo, wana familia ni kwamba tu hawawezi kuandamana wanaandamana kwenye mioyo. Tunapitisha trilioni 49 hapa halafu mnategemea waende kuzisimamia watu ambao wana manung'uniko, watu wanaodhulumiwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, tumekuwa tukitoza tozo kwenye mafuta ya petroli na gesi ili

ziende kwenye Mfuko wa Maji, Mfuko wa Nishati Vijijini, Mfuko wa Barabara. Kwa miaka mitatu mfululizo pesa hizi hazijaenda na hizi ni pesa mahsusi za kazi mahsusi zipo kwenye *ring fence* kisheria, kutopeleka pesa hizi ni kuvunja Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa hivi kwenye Mfuko wa Maji, hazijaenda bilioni 285, nishati vijijini hazijaenda bilioni 267, Mfuko wa Barabara hazijaenda bilioni 598, fedha ambazo hajizaenda kwa miaka mitatu mfululizo trilioni moja na bilioni mia tatu arobaini na saba. Sasa mnategemea barabara vijijini zitapitika? Mnategemea miradi ya maji kwenye Majimbo yetu itakamilika? Mnategemea miradi ya umeme itakamilika miaka mitatu mfululizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria inavunjwa, pesa zipo kwenye uzio hazipaswi kutumika kwa matumizi mengine yoyote, yoyote yale. Tunatoza tozo kwenye mafuta na gesi mafuta ya petroli na *diesel* ili watu waende wakaone maendeleo kwenye haya maeneo ninayoyasema. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bulaya, kuna taarifa.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilipanga nimjibu wakati wa kuhitimisha ile hoja ya kwanza ya mafao ataona matamko ya wapokeaji wenyewe, lakini taarifa tulizonazo ni kwamba wamefurahishwa sana na hatua ya Serikali iliyofanya. Nilichosimama kutaka kumpa taarifa anasema fedha hazijaenda, hili ni jambo limenishtua fedha hazijaenda wapi? Fedha za Mifuko zipo kwenye Mifuko hazijaenda wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za mifuko zipo kwenye mifuko na zinatumika kufuatana na mahitaji, Mheshimiwa Mbunge asichanganye fedha zinazotumika kwenye *maintenance* na fedha zinazotumika kwenye barabara mpya. Kwa hiyo, fedha za Mifuko zipo kwenye Mifuko. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Bulaya, muda wako umekwisha. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, anaingia Mheshimiwa Mkenge, jiandae Mheshimiwa Magessa, jiandae Mheshimiwa Abdul-Hafar. Mheshimiwa Mkenge hayupo? Mheshimiwa Magessa, ajiandae Mheshimiwa Abdul-Hafar.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii nzuri ya kuchangia kwenye bajeti kuu ya Serikali na Mpango wa bajeti kwa mwaka huu. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa sababu ya kutupatia fursa hii ya kujadili bajeti kwa ajili ya watanzania takribani milioni 61 kwa ajili ya mwaka huu unaofuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwapongeza Mawaziri wote wawili, nawapongeza vilevile wataalam na Makatibu Wakuu wote na Katibu Mtendaji Mkuu wa Tume ya Mipango kuendelea kufanya kazi nzuri ambayo tuliitarajia kuiona wakati tunapoenda kwenye bajeti ya mwaka huu wa fedha unaokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa ninasoma taarifa hii ukurasa namba 11 ukanionesha wazi kwamba, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika mradi mkubwa wa *SGR lot one* imekamilika, *SGR* hiyo imetekelezwa kwa *lot one* mpaka asilimia 83.55. *Lot two* imekwenda asilimia 57.57 lakini ilikutwa kwenye asilimia hizo na sasa imekamilika. Kwa hiyo, ninachokiona hapa ni kwamba, lile neno Kazi Inaendelea linaonekana kwenye bajeti hizi, kwa sababu pale *lot one* ilipokutwa sasa imekamilika inaweza kuanza kutumika lakini *lot two* ilipokutwa imekamilika inaweza kuanza kutumika. Maana yake nampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa matokeo mazuri ya kwanza hayo ya *SGR lot one* na *lot two. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo *lot* nyingine zinazofuata ambazo nazo zinakwenda kwenye utekelezaji, kila moja ipo katika kiwango chake tofauti tofauti mpaka *lot* saba. Kuna uboreshaji wa bandari kina kufikia mita 15.5 na upana wa mita 200 ambayo

kazi hii nayo inatarajiwa kuendelea ili meli zetu kubwa ziweze kutua katika bandari hiyo ya Dar es Salaam ambayo tunatarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile bandari yetu kavu ya Kwala imefikia sasa takribani asilimia 96 hii yote ni kazi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ninayasema haya ili ninapo mpongeza isionekane ninampongeza tu kwenye *plain surface*. Nampongeza kwa sababu ya vile ambavyo vimetokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uwanja wa ndege wa Msalato kwenye miundombinu umefika takribani asilimia 56.9 lakini kwenye upande wa majengo sasa tumefikia asilimia 22. 56, maana yake kuna kazi inaendelea hapa, inawezekana tunaishi Dodoma lakini hatujaenda Msalato kuona kinachoendelea hiyo yote ni kazi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika sekta ya ujenzi tumeona kazi kubwa zinaendelea kwenye ujenzi wa barabara na maeneo mengine ambayo nisingeweza kuyataja yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti hii ukiangalia kwenye bajeti iliyopita ukiangalia kwenye sekta ya nishati utagundua wazi kwamba, Bwawa la Nyerere lilipochukuliwa mara ya kwanza Mheshimiwa Rais anaingia madarakani lilikuwa asilimia 37 na sasa limefika asilimia 97.43 na tayari tumeshafanya majaribio na Megawati 235 zinafanya kazi kwenye mtambo namba tisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu na ushauri kwa Serikali hapa ni kufanya ile mitambo mingine kuanzia mtambo namba moja mpaka nane iingizwe sasa ili tuweze kupata hizi megawati 2,115 zote na hizo *interface substations* iliyopo Lemugul kule Arusha na nyingine zinayojengwa huku kwenye *Southern Regions* ziweze kufanya kazi ili tuuze umeme au tu-*import* umeme kutoka kwa wenzetu tunapokuwa na matatizo ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *REA* nimeona wazi kwamba, kuna takribani vijiji 11,973 vimeunganishwa ambavyo ni takribani asilimia 97 tumeshaviingiza, nchini hii imeshakuwa na umeme kwa kiwango hicho. Vitongoji takribani 32,827 kati ya Vitongoji 64,359

vimepata umeme, hapa vilevile nitoe ushauri kwa sababu karibu asilimia 50 ya vitongoji havijapata umeme tuendelee kujikita kuona tunapata wapi fedha kuhakikisha kwamba, vitongoji vyote vinapata umeme kwa sababu umeme sasa siyo anasa tena kila Mtanzania ana uhitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye maji nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kule tu Jimboni Busanda kuna mradi wa takribani bilioni 6.2 umefikisha maji kutoa Njia ya Korongo kuja pale Mji Mdogo wa Katoro, matarajio ya maji kupatikana yalikuwa ni changamoto lakini maji yamefika na sasa yanaanza kutumika tupo kwenye ugawaji sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna miradi mingine mbalimbali Jimboni kwangu ambayo inaendelea kuwepo kusambaza maji Nyarugusu takribani milioni 700 imekwenda pale kufanya hiyo kazi na maeneo mengine mengi. Yote haya nimeyasema kwa sababu nataka tuoneshe kwamba yapo mambo makubwa yanafanyika kwa bajeti zilizopita na bajeti ya mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye elimu, nilisikia Mbunge mmoja nasema hapa wiki iliyopita tulipigiwa simu kuhakikishiwa wazi kwamba sasa fedha imekwenda kwa ajili ya ujengaji wa sekondari za *SEQUIP*. Mimi nimepigiwa simu nikaambiwa sekondari mpya inatakiwa kujengwa kwenye Kata ya Nyamigota kwenye Kijiji cha Chibingo na pesa ina kwenda wiki hii. Kwa hiyo, ninaamini kesho ni Ijumaa lakini ninaamini kazi huko itakuwa imeanza, hii yote ni kazi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuende kwenye bajeti hii ambayo sasa tunaenda kushughulika nayo ambayo imetuonesha vipaumbele kadhaa. Ukiangalia maeneo ya mpango yana hoja gani? Yanasema yanataka kuchochea uchumi shindani na shirikishi. Hapa hoja kubwa ni kwamba, lazima wananchi wengi washirikishwe kwenye uchumi wa nchi hii na hapa ndipo tunaenda kuwaona wakulima wengi ambao hawajashiriki kwenye kilimo hawachangii pato la nchi hii, matokeo yake mapato yetu yanakuwa kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo, ina nafasi kubwa ya kufanya mchango huu uwe mkubwa kwamba, wale wananchi ambao ni asilimia 66 wakiwezeshwa kupitia skimu za umwagiliaji hii kazi inawezekana kuona tuna mchango mkubwa na mapato yakaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya sana ni kwamba, kwenye maeneo kwa mfano ninayotoka mimi bado hata upembuzi yakinifu uliosema mwaka jana haujafanyika. Kwa hiyo, ninaamini wale wananchi wangu wanachangia kidogo sana kwenye Pato la Taifa kwenye kilimo, lakini na maeneo mengine inawezekana ikawa hivyo. Kwa hiyo, niwaombe sana Wizara ya Kilimo, wahakikishe kwamba wale watu wengi asilimia zaidi ya 66 wapate hizo skimu za umwagiliaji na wawezeshwe ili kuweza kupata mchango mkubwa wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na kwa watoa huduma kukuza bidhaa na uwekezaji na kuchochea maendeleo ya watu na kuzalisha rasilimali watu. Hapa watu wengi wamesema juu ya ajira na sipendi niparudie sana. Kazi kubwa ambayo tumeiona kwenye *section 10* Ukurasa namba sita ni kukamilisha miradi ya kielelezo na miradi ya kimkakati ambayo nimekwisha isema. Kwa hiyo, ninaamini kabisa hii trilioni 49.35 inakwenda kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja tu ni kwamba tumekuwa tunasema kila wakati lakini tunapokwenda kwenye utekelezaji tunakutana na changamoto kwamba pamoja na utekelezaji mzuri unaoenda kufanyika kuna maeneo mengi yanakuwa hayakuguswa. Ukiangalia tumepata ukisoma kwenye *page six section* 12, utagundua imeelezwa wazi kwamba, umewekwa uwekezaji mkubwa kwenye uthibiti wa matumizi mabaya ya Serikali. Maana yake nidhamu ya fedha inaenda kuwa nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda hapo hapo ukaenda mbele utekelezaji wa bajeti iliyopita utagundua fedha iliyotoka mpaka Aprili ni asilimia 80.5 fedha ambayo haitatoka ni asilimia 19.7. Sasa hoja yangu ni nini, kuna miradi ambayo haijaanza kabisa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Magessa kengele ya pili hiyo.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni waliopo Bungeni mchana huu, wageni waliokaa Jukwaa la Spika ambao ni wageni 16 wa Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Wenyeviti wa Kamati ya Usalama Barabarani, Mikoa ya Tanzania Bara wakiongozwa na Ndugu Idd Azzan aliyekuwa Mbunge na Mwenyekiti wa Kamati ya Usalama Barabarani. *(Makofi)*

Wengine ni Ndugu Rajabu Buriku - Mbeya, Ndugu Abdukadri - Moshi, Ndugu Amos Kandonya - Simiyu, Ndugu Jane Jenesi Izira - Singida, Ndugu Edward Nyaulingo - Geita, Ndugu Nassor Mansour - Mtwara, Ndugu Rashidi Hamudi - Tanga, Ndugu Hamudi Nassoro - Tabora, Ndugu Nawidi Mula - Pwani, Ndugu Emmaneul Mollel - Manyara, Ndugu Wiston Kabatenga - Kagera, Ndugu Lucas Mashauri - Ilala, Ndugu Majale Kanunda - Simiyu, Ndugu Mohamed Khalifa - Kilimanjaro na Ndugu Jafari Mchangueni - Rufiji. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni 70 wa Mheshimiwa Profesa Mkumbo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ambao ni Wenyeviti na Makatibu wa CCM wa Matawi yote ya Jimbo la Ubungo. Karibuni. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Profesa Alois Ndakidemi, mpiga kura wake kutoka Kibosho, Mkoa wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, rafiki zake kutoka Ilemela, Jijini Mwanza. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, Wachungaji na Askofu kutoka Kanisa la *Cavalry Assemblies* of God la Jijini Dar es Salaam.  Karibuni. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Boniphace Butondo amba oni binamu zake na watoto wao kutoka Lugana Mkoa wa Shinyanga na Wachungaji kutoka Kishapu, Igunga, Shinyanga, Tabora na Arusha. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Neema Mwandabila ambao ni wadogo zake kutoka Mkoa wa Mbeya. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo, wanafunzi 90 na walimu 11 Shule ya Sekondari *Haradali Winners* kutoka Jijini Arusha, karibuni. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wageni watano ambao ni wafanyakazi wa Kairuki *Hospital* kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni 10 familia ya Mzee Joseph Kiendi Mtungwa kutoka Mkoa wa Mara.

Wanafunzi 110 na walimu 10 kutoka Shule ya *Morogoro Baptist Pre and Primary School,* karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Abdul-Hafar Juma, ajiandae Mheshimiwa Aloyce Kwezi.

**MHE. ABDUL-HAFAR IDRISSA JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia katika hoja tuliyonayo mbele yetu. Mimi ninaomba nianze kwanza kwa kuipongeza Serikali kwa mambo mazuri yanayoendelea kupangwa na mambo mazuri yanayoendelea kutendeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu Serikali ya Awamu ya Sita iingie madarakani na Chama cha Mapinduzi kuendelea kuongeza Taifa letu, yote yaliyokuwa yameahidiwa wakati wa kampeni na yote ambayo yameandikwa katika Ilani ya Chama chetu yameendelea kutendeka na hayo dhamira yake ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora na ndiyo dhamira ya CCM na Serikali yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeendelea kulijenga Bwawa la Mwalimu Nyerere na tayari tumeona linatoa huduma kwa wananchi. Tuliahidi katika Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Mama Mheshimiwa Dkt. Samia amefanikisha na Serikali yake imesaidia hilo. Tuliahidi treni itatoa huduma, treni imeshaanza kutoa huduma kwa hiyo, tunaendelea kuipongeza Serikali kwa yale yote yanayoendelea kutendeka. Ni nini ambacho ningependa kuchangia katika bajeti yetu hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti imependekeza kuweka tozo ama kodi katika gesi inayotumika katika magari. Moja ya sehemu ambayo tunatumia fedha nyingi sana za kigeni, kama Taifa, ni katika kuagiza mafuta tena yanayotumika katika magari. Mheshimiwa Waziri hapa ametangaza amesema, kama tukifanikiwa kupitisha hiki ambacho tunaendelea kukijadili, basi baada ya kuanza kutumika kwake hakutakuwa na matumizi ya dola. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapendelea pasitumike dola katika matumizi ya kawaida, lakini kiuhalisia hata sisi sote tuliopo humu ndani tukitoka tu baada ya kuahirisha Bunge tutenda kutumia dola kwa sababu, tutapanda katika magari na magari haya yanatumia mafuta na mafuta haya tunayaagiza kwa kutumia dola za kimarekani. Fedha nyingi sana tunazitumia katika kuagiza mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza jitihada za kuhakikisha tunapunguza matumizi ya dola kwa kuongeza uzalishaji wa ndani katika mambo mbalimbali, mfano viwanda vya sukari, napongeza. Mfano, tunashadihisha sasa tuanze kutumia na kuzalisha mafuta ndani, lakini hatujaongeza nguvu katika kuacha kutumia mafuta ya *petrol* na *diesel* kwenye magari yetu na tumeweka kabisa tozo katika hili. Wenzangu wamesema na mimi narudia kusema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi nzima hii ya Tanzania ina vituo vitatu tu ambavyo vinatoa huduma ya gesi kwa magari ambayo yanatumia gesi. Mimi nadhani kama tukiamua kuweka tozo, kama tukiamua kuweka kodi, isiwe kodi inayokwenda kutumika

kama kodi nyingine zote. Kodi hii iwekewe mfuko maalumu wa kusaidia uwezekano wa wawekezaji kuwekeza katika vituo vya gesi, ili gesi ipatikane zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya sababu ambayo inasababisha vituo vya mafuta ya *petrol* na diesel kuwa vingi kuliko vituo vya gesi ni gharama ya uwekezaji. Gharama ya uwekezaji kuwekeza kituo cha kutoa huduma ya gesi ni kubwa sana kuliko vituo vya mafuta. Mimi nadhani kama tuliweza kutoa bilioni 100 kila mwezi kusaidia kupunguza bei ya mafuta, kama kodi hii tukiiweka na tutafute fedha nyingine kuhakikisha unapatikana urahisi wa kuwekeza vituo vya gesi, tukifanya hivyo tutapunguza matumizi ya dola katika kununua mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya dola yamesababisha dola ipande na kupanda kwa dola kumeathiri watu wengi sana. Sisi Wazanzibar tunapenda sana sikukuu, kule kwetu tunyime kila kitu usitunyime sikukuu; hivi leo tunavyozungumza nadhani ni Eid ya nne kule Zanzibar na baadhi ya wananchi wangu wameniambia wanataka kutoka wakasherehekee Eid. Kwa hiyo, sisi tunapenda sana sikukuu, lakini wananchi wamelalamikia ongezeko la bei ya kuwanunulia watoto nguo za sikukuu. Nguo iliyonunuliwa mfungo mosi, nguo ile ile katika mfungo tatu imepanda, tatizo ni dola tu imepanda. Pamoja na kupanda kwa gharama za usafirishaji baharini, lakini dola imepanda. Tunafanya nini kuhakikisha mafuta haiwi sababu ya kutumia dola zetu na tuzitumie katika mambo mengine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninashauri kama tutakubaliana humu ni lazima hiyo tozo ama hiyo kodi iwepo, isiende katika mfuko wa matumizi ya kikawaida, iwe ni fedha maalumu katika kusaidia upatikanaji wa vituo vya gesi na urahisi kwa wawekezaji, ili wananchi watumie gesi katika magari yao. Miongoni mwa mapato yasiyo ya kodi yanatokana na Shirika letu la Ndege la *ATCL*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niipongeze Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya Mheshimiwa Dkt. Mama Samia, kwa kuhakikisha ndege zinaendelea kuwepo,

ndege zinaendelea kupatikana na zimekuwa msaada, lakini ndege zinafanya biashara. Kumpata mteja kwa mara ya kwanza katika biashara ni jambo linalowezekana. Pamoja na usimamizi mzuri sana, kazi ngumu sana katika biashara ni kumfanya mteja arejee huduma yako. Sasa wahudumu wa kike na wakiume wa ndani ya ndege nadhani wanavutia, mambo ni mazuri, lakini kwa upande wa *ATCL* angalieni wahudumu wenu wanaokutana na abiria iwe wakati wa ku-*check* au iwe wakati wa kununua tiketi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kununua tiketi hakuna matatizo sana, pana matatizo katika nyakati za ku-*check*. Abiria ndiyo bosi wa *ATCL* sio Mkurugenzi wa *ATCL*, sasahivi bado watu wanakimbilia huduma za *ATCL* kwa sababu, hakuna mbadala, siku watakayopata mbadala wataacha kutumia *ATCL;* baadhi ya wahudumu wenu ndio wanaosababisha. Sasa waangalieni wahudumu wenu katika zile *counter* za ku-*check*, wana-*treat* vipi wateja? Wanasaidia vipi wateja? Wanawapa wateja mbadala upi wa huduma pale wanapokuwa wamechelewa kwa sababu, hii ni biashara na tunategemea fedha, ili bajeti hii tunayotaka kuipitisha sehemu ya fedha hizo tunazitegemea katika Shirika la Ndege? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipongeze Mamlaka ya Mapato Tanzania, *TRA,* kwa namna ambavyo wamekuwa wanajitahidi kuendeleza mahusiano. Siku moja nilikwenda Mamlaka ya Mapato, *TRA,* Temeke na sikupenda kujitambulisha kama Mbunge nikasema ngoja nipate huduma za kawaida na wananchi wenzangu. Mbele ya Bunge hili naomba nimpongeze sana Meneja wa *TRA* wa Mkoa wa Kodi wa Temeke, sikumbuki sana jina lake, lakini anaitwa Masau Malima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilivyofika nilikuta watu wengi katika foleni. Miongoni mwa watu waliokwenda kuomba msaada ni mtu ambaye alikuwa anatakiwa kulipa kodi ya shilingi 18,000; amekwenda anaomba msaada wa Meneja wa Mkoa na alitenga muda akamsikiliza mwananchi yule. Mwananchi aliondoka amefurahi na ninaamini Taifa letu limepata kodi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niipongeze *TRA* kwa kuendelea kujenga mahusiano na walipakodi. Waendelee kufanya hivyo na hapa nimemtaja huyu maalumu, awe mfano na chachu kwa wengine, ili tuendelee kulijenga taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nashukuru sana. Naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Aloyce Kwezi, jiandae Mheshimiwa. Tuanze na Mheshimiwa Kwezi kwanza.

**MHE. ALOYCE A. KWEZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba na mimi nichukuwe nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pili kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mapenzi yake mema kwa sisi wananchi wa Tanzania. Pia, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Waziri wa Fedha pamoja na timu yake yote kwa kazi nzuri za kuhakikisha tunaijenga Tanzania kwa umoja na kuhakikisha maendeleo ya Tanzania yanawafikia Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimesimama hapa, kwa nini nimeanza na shukrani?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeanza na shukrani kwa sababu, kwanza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, pesa zilizokuja katika maeneo yetu ni nyingi sana, haijawahi kutokea. Mbili, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa sababu, ni hivi karibuni tu kule Kaliua sisi tunahifadhi misitu vizuri sana, wameweza kutupatia fedha karibu shilingi bilioni 16, fedha ya kaboni, wanasema ya ukaa. Mheshimiwa Jaffo nakushukuru sana na Wananchi wa Kaliua wanakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba fedha ambazo mmezibajeti na kuzileta Kaliua mzisimamie vizuri sana, ili manufaa yale yaweze kutokea katika Jimbo la Kaliua. Jambo la pili ambalo naishukuru Serikali ni kuhakikisha kwamba, sasa Wakulima wa Mkoa wa Tabora, Wakulima wa Kaliua, lile ombi ambalo tulikuwa tunaomba siku zote, mmeonesha usikivu mkubwa sana, ni

kutupatia ruzuku ya mbolea. Ruzuku kwenye tumbaku *(NPK)* tulikuwa hatuna, lakini mwaka huu wakulima wa Jimbo la Kaliua, Wakulima wa Mkoa wa Tabora, tunakwenda kunufaika na mbolea za ruzuku. Pamoja na kwamba Mheshimiwa Bashe hayupo, lakini tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri inayofanywa na Serikali hii ya Awamu ya Sita, tunashukuru sana kwa jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina ombi. Mwaka jana Mwezi wa Tisa sisi Mheshimiwa Rais alituondolea vijiji ambavyo vilikuwa hifadhi, karibu vijiji kumi na sita na baada ya kuviondoa tulipata changamoto ya barabara. Tulikuja kwako na tukapata fedha ambapo Mtendaji Mkuu wa *TARURA* alipitisha pamoja na Waziri wa TAMISEMI. Sasa mezani kwako bado kuna ombi la shilingi bilioni tatu, ili kuhakikisha vijiji hivyo tunafungua barabara zake zote. Nakuomba Mheshimiwa Waziri, fedha hizo uweze kuziruhusu, ili sisi wananchi wa Kaliua tuweze kujenga miundombinu ambayo ilikuwa ni sehemu ya hifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo ninamuomba Waziri wa Maliasili ni kuhusiana na vijiji vyetu viwili, Kijiji cha Usinga na Kijiji cha Ukumbi Kakoko. Walikuja Mawaziri awamu ya mwisho; awamu ya kwanza timu ya kwanza ilikuja ikaruhusu kwamba, Mheshimiwa kawaonea huruma wananchi waishi. Nataka niweke kumbukumbu vizuri kwamba, vile vijiji viwili vya Ukumbi Kakoko na Usinga vipo pale kuanzia Mwaka 1973, ni vijiji ambavyo vimesajiliwa TAMISEMI. Kwa mapendekezo ambayo mlikujanayo muelewe kwamba, ni vijiji halali na vinatawaliwa na Sheria ya Ardhi, Sheria Namba 5 ya 1999.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwamba, wale wananchi mlikuwa mnasema habari ya kifuta jasho; hakuna cha kifuta jasho pale, wananchi watakuwa wanastahili malipo halali, lakini mimi sioni kama kuna tija. Tumekuwa na tabia ya kuwaondoa wananchi bila sababu za msingi kwenye maeneo ambayo wameishi, kwenye maeneo ambayo wazazi wao na wazee wao wamezikwa. Hebu tuangalie utaratibu mzuri wa kwenda na jambo hili na ninawaomba Wizara ya Maliasili, ninamuomba Waziri

wa Ardhi, tulishazungumza, jambo lile liangalieni vizuri, ili wanavijiji waendelee na kazi zao kama kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo ninaomba ni ile miji 28 ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia ametoa fedha, Serikali ya Awamu ya Sita imetoa fedha, wanufaika wa Mradi wa Maji wa Ziwa Viktoria ni pamoja na Kaliua. Kwanza nawapongeza watu wa maji wa Tabora kwa kazi nzuri kwa sababu, ule mradi unaopeleka maji Skonge, unaopeleka maji Urambo, unaopeleka maji Kaliua upo asilimia 40, lakini ninawaomba kwa sababu, sasahivi wamemalizia tanki la lita milioni mbili. Mimi ninaomba waanze kusambaza mabomba katika Kata zote za Jimbo la Kaliua ambazo zinapitiwa na ule mradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba ule unaisha mwakani Mwezi wa Saba. Nawaomba, kama upo uwezekano wa kumaliza mradi mkubwa kama huu mapema itakuwa ni manufaa makubwa sana kwa wananchi. Mimi nina changamoto, nimefurahishwa kwa sababu, najua Waziri wa Nishati na Naibu Waziri Mkuu wetu yupo na ni makini, nadhani sasa Kaliua tunaongoza kwa kukatika katika umeme wakati mradi mkubwa wa Mwalimu Nyerere umeingiza umeme kwenye gridi ya Taifa, sisi kule bado shida ni kubwa sana. Mimi nakuomba Waziri wa Nishati, hebu fuatilia sana kuna shida gani Kaliua? Yaani umeme kwa siku unakatika zaidi ya mara 20, ni meseji kuanzia asubuhi mpaka jioni, naomba sana ulifuatilie jambo hili, ili tuelewe kuna nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi natambua kuna mradi pale unau-*push* toka umeingia. Nakupongeza umesababisha ule Mradi wa Uhuru pale umekwenda kwa kasi sana, lakini sisi tunachohitaji ni umeme. Yaani hizi *process* zote wananchi hawazihitaji, wanahitaji matokeo, matokeo ni uwepo wa umeme. Watu wanahitaji kuangalia mpira, watu wanahitaji kufanya mambo mbalimbali kwenye mitandao, umeme hamna, wanahitaji mambo ya kuchomelea na mambo mengine. Nakuomba Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu tusaidie sana Kaliua, ili twende pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine ambalo ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Rais ni, wiki hii nimepata taarifa sisi tunapelekewa fedha Kaliua, ametuongezea sekondari tatu, namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Sasa katika Kata ya Ushokola tunakwenda kuongeza sekondari mbili, sekondari ya kwanza inakwenda kujengwa kwenye Kijiji kinaitwa Sanja Ndugu na sekondari ya pili inakwenda kujengwa kwenye kijiji kinaitwa Ibara Upina na katika Kata ya Ingwisi sekondari inakwenda kujengwa Mahalaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais anapofanya majukumu yake mazuri kama haya, Serikali yake inapofanya mambo mazuri kama haya, mimi nasimama kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Kaliua kumshukuru sana kwa mapenzi yake ya dhati. Miradi inayoendelea katika Jimbo la Kaliua ni mizuri sana, ni miradi ambayo tunaitegemea na kwa hilo tu Mheshimiwa Waziri wa Fedha naendelea kusisitiza, lile dokezo lipo mezani kwako. Tafadhali sana, shilingi bilioni tatu, chondechonde kabisa na ikiwezekana hata ukituma meseji muda huu wakaanza kuitoa, ili mimi nikifika kwenye ziara zangu za Mwezi wa Saba napita tu kuangalia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo lingine. Wilaya ya Kaliua kwa sababu ni miongoni mwa zile Wilaya zilizokuwa mpya, nakuomba Mheshimiwa Waziri, tunajenga Ofisi ya *TRA,* ahsante sana, lakini *TRA* inakwenda kwa kusuasua. Naomba ulifuatilie jambo hili, ili Ofisi ya *TRA* katika Jimbo la Kaliua ikamilike haraka iwezekanavyo, ili wananchi waendelee kupata huduma kwa ufanisi na kwa ubora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kumalizia na kusisitiza hapa, namuomba sana Waziri wa Ujenzi, Kaliua ni miongoni mwa Wilaya ambazo zinachangia sana mapato ya ndani katika Taifa, lakini barabara kubwa ambayo inatuathiri kwa sasa ni kutoka Mpanda – Kaliua – Kahama. Sisi tukipata korido ya barabara hii yote inayotokea Mpanda kwa ndugu yangu Mheshimiwa Kapufi anayepiga makofi hapo, ikapita kwangu, ikapita kwa Mheshimiwa Rehema Ulyankulu, ikaenda

Ushetu, ikaingia kwa kaka yangu Mheshimiwa Kishimba, ile korido kiuchumi sisi itakuwa imetuinua sana. Ile Kaliua ni kama *hub* kwa sababu, ndiyo maana kuna njiapanda hata za reli na ukiangalia hata reli tunaendelea kujenga sasahivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana narudi kusisitiza kwamba, barabara ile ni muhimu sana kiuchumi. Inawezekana msiamini, lakini ninachowaambia ni ukikuta Wilaya kama Kaliua inakuwa na wananchi karibu 768,000 hivi kweli tunajadiliana jambo kama hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wale wote wanahitaji huduma kubwa, ukiunganisha na hao tunaongelea watu zaidi ya milioni tatu. Nawaomba ndugu zangu, barabara hii tuipe msukumo wa pekee ni barabara ambayo imekuwepo kwenye Ilani ya uchanguzi kwa mihula mitatu ya nyuma yote imekuwepo pale. Kwa hiyo, nawaomba sana, pelekeni fedha, tuwekeeni wafadhili, ili barabara hii iweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, naendelea kupongeza jambo moja la kuhusiana na kikokotoo, lakini Waziri wa Utumishi sio mbaya sana. Hatua mliyoifanya ya kutusikiliza ni nzuri, lakini *if possible* endeleeni kuangalia, kuwapa nafuu hawa watumishi. Watumishi wengi wa umma kwa sababu, mishahara, na ninajiuliza hivi kwa nini siku hizi hela haikai sana? Mnaweza mkajifunza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema kwamba, naunga mkono bajeti kuu. Nashukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa wageni waliopo Bungeni mchana huu, wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni 56 wa Mheshimiwa Maryprisca Mahundi, Naibu Waziri wa Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Hiki ni kikundi cha wanawake kilichojikita katika utunzaji wa mazingira na kuinua wanawake kiuchumi, *Morogoro Women Voice Connection,* karibuni *(Makofi)*

Mheshimiwa Kuchauka muda uliobaki utakutosha?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** *(Hapa hakutumia kipaza sauti)*.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa awamu yetu ya asubuhi, wakati wa jioni leo tutaanza na Mheshimiwa Mohamedi Kuchauka, Mheshimiwa Dkt. Kikoyo, Mheshimiwa Ahmed Shabiby na Mheshimiwa Joseph Kamonga.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.55 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

**na**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Tunaanza na Mheshimiwa Mohamed Kuchauka, Mheshimiwa Dkt. Kikoyo na Mheshimiwa Ahmed Shabiby, ajiandae.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi jioni hii ya leo na mimi niweze kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwenye hii bajeti kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mimi nitajikita sana kwenye ushauri lakini awali ya yote tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai wa kuweza kukutana jioni hii. Vilevile, nipeleke shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hasa kwa maono yake ya kutenganisha Wizara hizi mbili, Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza ushauri wangu kwenye Wizara ya Mipango. Mheshimiwa Rais alipotenganisha Wizara hizi mategemeo yake makubwa aliyotaka kuyaona ni kuona bajeti zetu au bajeti hii ya kwetu inakwenda na mipango ambayo nchi yetu imejiwekea. Bajeti ambayo inakwenda kutekeleza mpango na siyo kutekeleza tu mpango, ni mpango endelevu na mpango wenye tija. Kama Taifa hatuna tatizo la kupanga mipango. Tatizo letu ni mipango yetu inatupeleka wapi, tunaimalizaje na tunaitekelezaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo shida kwenye utekelezaji wa mipango. Tumekuwa wapangaji wazuri sana na wakati mwingine ziko nchi zinakuja kukopa namna tunavyopanga mipango yetu lakini shida ni kwamba tunatekelezaje. Nitoe mfano, tunao mpango wa pale Dar es Salaam wa ujenzi wa barabara zile za *BRT*. Barabara ya Kimara imeisha miaka 10 sasa, kwenye mipango yetu kwa namna tulivyoipanga na tukipima leo tumefanikiwa kwa kiwango gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ukiniuliza nitakwambia tumefeli kwa sababu leo pale mabasi hayatoshi na msongamano ni ule ule. Tulitegemea kupunguza daladala, ndiyo kwanza zinaongezeka. Kwa hiyo, pale mimi naweza nikasema kwamba tumefeli. Pamoja na kufeli kule bado tunaendelea na mipango mingine, tumejenga Mbagala. Mbagala sasa hivi imeisha ina mwaka lakini hakuna basi hata moja. Pia kama haitoshi

tumeenda Gongo la Mboto, ambayo kesho au kesho kutwa itaisha. Sasa ukiwauliza wanakwambia magari yako kwenye manunuzi. Tulivyokuwa tunapanga, tulikuwa hatujui kwamba mradi huu unakwenda kukamilika lini ili uendane na uletaji wa mabasi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, pale tumepanga lakini hatuku-*foresee* kwamba tunakwenda kufanya nini. Leo ukiniambia mimi kwamba magari ya *BRT* yanakuja yako kwenye manunuzi siwezi kuelewa kwa sababu mradi ule, zile fedha ziko pale. Ile barabara imeisha ina mwaka, fedha za walipa kodi ziko pale zimelala hazina kazi na tumeanza kulipa. Mategemeo yetu ni kwamba sasa zingeanza ku-*generate* fedha pale ili kuanza kulipa lakini tunaanza kulipa au tutakuja kulipa wakati fedha zimelala pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi huo huo nauona kwenye *SGR*. Leo tumeshafika Morogoro na kesho tunaingia Dodoma lakini tumejipangaje kuhusu uendeshaji wa hiyo reli na kwa nini tunafika mahali ili tuweze kutekeleza mpango ambao tumeuanza miaka miwili iliyopita, *sustainability* yake ni mpaka tuje tubadilishe sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kitangulie? Tubadilishe sheria au tuanze mradi? Mwaka jana tu ndio tumebadilisha Sheria ya *PPP,* kwamba ndiyo tumegundua kwamba kumbe hii reli kuendesha kama Serikali hatutaweza tunahitaji watu wa kuwekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali ambayo ndiyo yenye mradi wake mpaka leo mabehewa yako kwenye manunuzi, hawa *PPP* ambapo jana ndio tumeweka sheria ina maana wachukue muda na wao kuomba. Waombe, waingie mikataba, wakishapata hiyo mikataba ndipo waagize mabehewa itakuwa ni miaka miwili, mitatu au minne. Reli imeisha lakini watu wako kwenye manunuzi. Ina maana kwamba tulivyopanga hatukujua kwamba kama Serikali kazi yao ni kutengeneza njia ili wawekezaji waje watumie hiyo njia lakini mpaka juzi ndio tumekuja kubadilisha sheria hapa, ndio tunakumbuka kwamba kumbe ili hii reli iweze

kwenda *effectively* lazima tuite *PPP*. Ndio tumebadilisha sheria tumekwenda na *PPP*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii yote ni kwa sababu tunakwenda na mipango ambayo haiko sawasawa. Mimi niwashauri Waheshimiwa Wabunge wenzangu. Mimi nafikiri Waheshimiwa Wabunge tubadilike kidogo, Serikali inapokuja na mipango na sisi tujiridhishe. Kitendo cha Bunge kupokea mpango wa Serikali tukaupitisha juu juu bila kujua undani wake halafu unakuja unatuletea matatizo kama haya ya kubadilisha sheria nafikiri hatutakuwa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima mipango hii ya Serikalini inapokuja, sisi kama Wabunge tusimame tuiangalie *sustainability* yake, ufanisi wake, utekelezaji wake na miundombinu yake ya utekelezaji itakwendaje lakini kama sisi tutakuwa tunapitisha tu maadamu Serikali wameleta mipango yao na sisi tukakubaliana mwendelee. Matokeo yake ndio wanakuja kesho kutwa yake tubadilishe sheria ndiyo mipango iweze kutekelezeka ndiyo mipango iweze kutekelezeka, hii haiwezi kuwa sawa, atuisaidii nchi hii. Kwanza, tunapoteza fedha za walipakodi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwingine ni kwenye huu Mradi wa *EPC+F*...

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa, Taarifa, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiswaga, Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumuunga mkono mchangiaji, anachangia vizuri sana lakini anavyosema kwamba Waheshimiwa Wabunge tupitishe bila kujua na sisi tuko hapa ndio tunatoa mawazo yetu, si utoe mawazo kwa namna ambayo unaona Serikali iende. Ndiyo

tunachotakiwa kufanya. Kaka naomba usilishushe hivyo Bunge, changia unachotaka Serikali ifanye au iboreshe katika mipango.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kuchauka, unaipokea hiyo Taarifa?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea taarifa yake. Nilichotaka kusema ni kwamba, *EPC+F* ilianzia kwenye Kamati ya Miundombinu. Kabla haijafika Bungeni inaanza kwenye Kamati na hata ile mipango ya *BRT* ilianza kwenye Kamati vilevile Mipango ya *SGR* ilianza kwenye Kamati. Leo tumesaini mikataba ya *SGR,* tumesaini mpaka vipande sita, imepitia kwenye Kamati lakini ukiuliza behewa tunazo? Unaenda kuambiwa kwamba bado ziko kwenye manunuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niliposema Bunge kwa maana ya Kamati zetu zinapoletewa hizi taarifa tuzisimamie vizuri. Leo tunazungumza hapa Bungeni na tunashauri lakini tunaposhauri jambo hili tayari limeshaharibika. Ili ionekane Bunge linafanya kazi vizuri, tuyasimamie haya kabla hayajaingia humu ndani ili yasiharibike. Leo hili likiharibika, linaharibika mikononi mwetu. Mbagala imekaa haina kazi, hamna magari na hii Barabara ya Kimara mpaka leo haina magari, barabara hizi zinaharibu matairi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za watu ziko pale, zimeshaharibika lakini zimekuja kuharibika mwishoni. Hili jambo haliwezi kuwa sawa. Lazima tunapoletewa mipango hii na sisi tujiridhishe kwamba mipango hii kama haitekelezeki basi tuikatae. Hicho ndicho ambacho nilikuwa nataka nikiseme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoa mfano wa pili hapa huu wa *EPC+F* tuliaminishwa wapo matajiri wanakuja kujenga hizi barabara kwa muda mfupi. Badala ya sisi kutumia miaka 20 kujenga barabara saba, hawa watatumia miaka mitatu minne barabara zimeisha lakini kinachoonekana hapa, hawa watu wenyewe wametudanganya bado hawana uwezo ndiyo maana Serikali inasema bado tunaenda kwenye majadiliano. Tunajadiliana tuwawezeshe wapate fedha waje watujengee.

Ndiyo majibu yaliyopatikana hapo kwenye hotuba ya kisekta lakini je, hawa watu hawakuja kwenye Kamati na hawajajiridhisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini sisi kama Waheshimiwa Wabunge hatukuwaambia hebu mtuletee hao matajiri tuwaone; tuwahoji tuone uwezo wao. Jambo hili lisingekuwa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, tuna mambo mengine kama ya kisera, kama kuna sera ambazo tunaona hazitekelezeki Mheshimiwa Waziri wa Mipango tuzifute. Tuna sera ya kuunganisha mikoa yote kwa barabara za lami. Sera hii sasa inakwenda zaidi ya miaka 25 leo, bado hatuna uwezo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Mkoa wa Lindi na Morogoro haijaunganishwa, jana Mheshimiwa Mbunge mwenzangu hapa amesema Kigoma nako hakujaunganishwa. Sasa kama hivyo vitu havitekelezeki kwa nini vibaki kwenye vitabu? Kwa hiyo, tuvifute. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbona tulipohitaji kwamba kila kata iwe na kituo cha afya, tukaona kwamba haiwezekani kwamba kila kata iwe na kituo cha afya. Tukasema tunakuja na vituo vya kimkakati. Kwa hiyo, tukafuta ile ya kwamba kila kata iwe na kituo cha afya na hii nayo tufute. Kwa nini ibaki kwenye makaratasi na miaka inakwenda, mikoa hii haitaki kuunganishwa. Inafika mahali watu wengine wanaona kama wametengwa... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa muda. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Kikoyo, Mheshimiwa Ahmed Shabiby na Mheshimiwa Joseph Kamonga wajiandae.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia bajeti hii. Mimi nianze kuipongeza Serikali yetu, Mheshimiwa Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan na watendaji wote wakuu wa Serikali hii inayoongozwa na Mama Samia Suluhu Hassan. Vilevile, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri ambao hoja yao iko mbele yetu *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma mpango na ninampongeza Mheshimiwa Waziri kwa vipaumbele ambavyo ameviweka. Nimeangalia vitatu vya mwanzo ambavyo kimsingi ni vipaumbele vya kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele namba moja anaongelea kuchochea uchumi shindani, shirikishi na kuhakikisha kwamba Watanzania wanashiriki kwenye uchumi wao. Nadhani kipaumbele hiki kama tutakifanya vizuri, ndiyo kipaumbele ambacho kitashirikisha Watanzania kimiliki uchumi lakini pamoja na kushiriki kwenye kumiliki uchumi hata kuongeza wigo wa walipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili wanaongelea kuimarisha uwezo wa uzalishaji na cha tatu kukuza biashara na uwekezaji. Kwenye hiki cha tatu, kwenye Jimbo langu la Muleba pale tuna wafanyabiashara ambao wanaongeza mnyororo wa biashara kwenye zao la kahawa. Tuna viwanda kama vitatu pale, naomba nivitaje, tuna *Johansen Company Limited, Atadals Groups* na *Hakika Cofee*. Naiomba Serikali iwaangalie watu ambao wamewekeza kwenye kuongeza mnyororo wa thamani kwenye mazao ya kilimo. Hawa watu wanahangaika kutafuta mikopo, kuimarisha na kuboresha kilimo chetu lakini hawapati usaidizi wa haraka haraka na wa moja kwa moja hasa inapokuja kwenye suala la mikopo. Hawa ndio tunaweza kuwatarajia kesho na kesho kutwa kulipa kodi na kuzalisha na kuwafanya wawe kampuni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kutengeneza mabilionea kama Serikali haishiriki moja kwa moja katika kuwatengeneza hawa mabilionea. Serikali ina wajibu mkubwa kuwawezesha

hawa wafanyabiashara na wajasiriamali kuhakikisha kwamba wanakua kutoka kwenye hatua za mwanzo na kwenda kutengeneza kampuni kubwa ambayo mwisho yatakuja kulipa kodi kubwa kwa ajili ya kuongeza Pato la Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwenye hotuba yake aliyoitoa juzi, kwenye *paragraph* yake ya 58 ya hotuba yake aliongelea suala la kikokotoo. Naishukuru Serikali kwa kusikiliza kilio cha wafanyakazi ambao wamestaafu na wale wanaotarajia kustaafu. Kweli kilikuwa ni tatizo kubwa na niishukuru Serikali imeangalia kundi kubwa la wafanyakazi hasa wale polisi, kwenye idara ya afya, magereza na uhamiaji; ni taasisi au mashirika ambayo yanaajiri watu wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona sasa kutoka kwenye 33% kwenda 40% ni mwanzo mzuri lakini naomba niishauri Serikali yangu tusiishie pale. Naomba mwaka ujao turudi kule tulikotoka kwenye 50% ili kuwawezesha Watanzania wanaolitumikia Taifa lao kwa jasho usiku na mchana, wanapostaafu wapate mafao yao yanayotosheleza kukimu maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *paragraph* ya 83 ya Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliongelea suala la ajali za barabarani. Mheshimiwa Waziri alitaja takwimu kwamba kwa kipindi cha miaka mitano (2019 – 2024) zilitokea ajali za barabarani 10,093 lakini hizo ajali zilisababisha vifo 7,639 na majeruhi 12,663. Hili ni janga la kitaifa. Ukiangalia takwimu za dunia kila mwaka ajali zinaondoa takriban watu milioni 1.2 duniani kote na nusu za hizo ajali zinatokea kwenye nchi zinazoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia takwimu kwa ajali zilizotokea Tanzania zina athari kubwa kwenye bajeti ya Wizara yetu hii ambayo tunaijadili leo. Ingawa Mheshimiwa Waziri hakutuambia zina athari gani lakini ukiangalia takwimu hasa sisi ambao tumetoka kwenye usafirishaji, kwenye bajeti za nchi zinazoendelea hizi ajali zinakula asilimia tatu ya bajeti nzima ya mataifa yanayoendelea. Kwa maana hiyo kwenye bajeti tunayoijadili hapa kama kama *trend* ya ajali itaendelea hivi kama ilivyo, tutatumia zaidi ya shilingi trilioni 1.4 kuwatibia watu au

wahanga wa ajali kwenye hospitali zetu na kwenye nyumba zetu. Kwa hiyo, tunalo jukumu kama Taifa kuhakikisha kwamba tunazuia kutokea kwa ajali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru leo asubuhi niliona makamanda wetu wa Kikosi cha Usalama Barabarani na Kamati ya Usalama Barabarani. Tunalo jukumu na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani nakuona uko hapa, kuhakikisha kwamba tunatafuta mwarobaini wa hizi ajali ili kuokoa pesa ambayo tunaitumia kuwatibia wahanga wa ajali pamoja na ulemavu unaotokana na ajali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali yangu kwenye hili, watu wengi wanakufa na wanakufa siyo kwa sababu wamepata ajali, wanakufa kwa sababu mfumo wa kisheria tulionao ni mbovu. Mtu anapopata ajali ili shirika la bima limhudumie lazima jambo liende Mahakamani na mnajua mlolongo wa Mahakama zetu na watu wengi wanashindwa kutibiwa kwa sababu wengine hawana bima na Serikali haina mbadala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali yangu kwenye hili, ianzishe mfuko wa kuwahudumia wahanga wa ajali ili ajali inapotokea tusisubiri mtu aende Mahakamani ili apate huduma. Mtu anapopata ajali watu wengine kutokana na umaskini, ukoo unaanza kuchangishana ili wampeleke mtu hospitalini. Tunawapoteza watu wakati mwingine kwa sababu ya umaskini wa familia wanazotoka au kwa sababu ya mipango yetu ambayo haiakisi uharaka wa hizi ajali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali yangu tuanzishe mfuko wa kuwahudumia wahanga wa ajali pindi inapotokea tusisubiri Mahakama itoe hukumu, tuwahudumie mara moja hata wale ambao hawana bima na wale wanaotoka kwenye familia maskini. Mfuko huo uchangiwe na mashirika yote ya bima ili mtu akipata tiba, shirika la bima likimlipa zile pesa tulizozitumia kumtibia kutoka kwenye mfuko wa kuwahudumia wahanga wa ajali zikatwe kwenye mafao yako ya bima zirudi kwenye huo mfuko na huo mfuko uweze kuwa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuna malalamiko makubwa sana kwenye viwanda vya maji, Mheshimiwa Waziri wa Fedha naomba unisikilize. Watoa huduma au wawekezaji kwenye sekta ya maji wanayo malalamiko makubwa kwamba wanachajiwa *excise duty* kwenye *working capital* na hii wanasema inawaletea umaskini kwa sababu pale ambapo hawakutengeneza faida bado Serikali inaendelea kumtoza kodi kutoka kwenye mtaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii naomba tuliangalie kwa umakini vinginevyo viwanda vyetu vya uzalishaji maji vinaweza vikafilisika na tuangalie *trend* ya kufunga biashara kwenye sekta hii ya maji, wanasema ni mzigo mkubwa kwao nashauri tuliangalie na tulifanyie kazi kama lina athari kubwa kwenye viwanda hivi badala ya kuvifunga viendelee kutoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na hayo machache naunga mkono hoja ya bajeti yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Kikoyo, tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Kamonga, Mheshimiwa Jacqueline Msongozi ajiandae.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwamba leo nachangia hotuba ya bajeti kwa mara ya nne na Ludewa ikiwa inashuhudia maendeleo makubwa sana, kwa hiyo ninawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Ludewa kwa kuniamini, kunipa heshima hii na kuendelea kunishauri na kuniamini niweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Daktari Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea fedha nyingi za maendeleo Ludewa, kwa kweli kila mmoja ameshuhudia kasi kubwa ya maendeleo ila kuna changamoto chache ambazo wananchi wanaomba zifanyiwe kazi na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ni miezi zaidi ya miwili sasa tokea meli ile inayofanya safari zake MV – Mbeya, kutoka Mbeya kwenda mpaka Nyasa haifanyikazi kutokana na mafuriko, maji yalijaa sana wakawa wanashindwa kuendelea kufanya safari zao kwa sababu abiria mpaka kuifikia meli ilikuwa tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ludewa kuna Kata nane za wananchi ambao wana changamoto kubwa za barabara wanategemea usafiri wa meli. Kwa hiyo, niombe sana Wizara husika ikiwezekana watumie bandari ya muda pale eneo la Matema ili huduma ziweze kuendelea kwa sababu Uchumi wa wananchi unaathirika sana kwa kukosekana kwa usafiri wa uhakika wa meli katika Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwamba matumizi ya Serikali yameongezeka sana kwa mika hii ya karibuni na idadi ya watu pia imeongezeka. Tukianza kuangalia kwa mfano, kuna zoezi la kupeleka umeme vijiji vyote nchini linahitaji mapato mengi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna zoezi la usambazaji wa maji nchini linahitaji fedha nyingi, kuna kujenga barabara za vijijini ili tuweze kusafirisha mazao ya wananchi kutoa sehemu moja kwenda sehemu nyingine, inahitaji mapato mengi sana ya Serikali. Ukiangalia tokea miaka hii ya 1990 kuja huku mbele misaada misaada imepungua sana, tafiti zinaonyesha kwamba misaada imepungua kwa zaidi ya asilimia 50, kwa hiyo ili Serikali iweze kupata fedha kugharamia shughuli zote hizi pamoja na shughuli za elimu, shughuli za afya ni sharti kwamba ikusanye kodi ya kutosha ama ichukue mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kodi ningeshauri sana Serikali ijitahidi sana kuongeza mapato ingawa Bunge lilifanya kazi yake kupitisha ile sheria, leo Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo yupo tumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kumteua, sasa sekta yake hii ya mipango inatakiwa iwe mbele iweze kumsaidia sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwenye kubuni vyanzo vipya vya mapato. Tukianza kuangalia kwa Watanzania Waheshimiwa Wabunge

wengi wamesema hapa kwamba walipa kodi ni wachache sana kwa hiyo wanakamuliwa hao hao kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Serikali inawajibu mkubwa sana wa kuhakikisha kwamba inaongeza idadi ya walipa kodi na inaongeza vyanzo vipya vya kukusanya kodi. Vilevile takwimu zinaonyesha kwamba sekta isiyo rasmi ni kubwa sana hapa nchini na kusababisha Serikali kukosa mapato mengi sana. Serikali inatakiwa iweke vivutio ambavyo vitawafanya wale watu ambao wapo kwenye sekta isiyo rasmi waweze kuingia kwenye sekta amabyo ni rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itatusaidia sana kuongeza kiwango cha mapato ya ndani, kodi yetu inayokusanywa iendane na hali ya uchumi. Hata tunavyoangalia wastani wake, uwiano kati ya kodi na Pato la Taifa tukisimamia vizuri sekta isiyo rasmi na ikarasimishwa watu wakajisajili wakaingia kwenye sekta rasmi tutaongeza wigo kwa kiwango kikubwa sana cha walipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawezaje kuweka sekta hii ambayo siyo rasmi iwe rasmi. Eneo la kwanza ambalo tunaweza tukaangalia ningependa kuishauri Serikali kwanza zile taratibu za usajili mtu akitaka sijui leseni ya biashara, akitaka kibali cha kujisajili biashara yake tupunguze urasimu, kipatikane kwa urahisi kama inawezekana ikapatikana Halmashauri basi kipatikane Halmashauri. Zile leseni za biashara kungekuwa na uwezekano ikitolewa mara moja ndiyo basi kuwe na njia nyingine ya uhakiki kama huyu bwana anaendelea na biashara au amefunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri kama inatoa kila mwaka kewa lengo la kumkamata yule ili alipe mapato basi ilitakiwa tuweke utaratibu mwingine ambao ni mwepesi, hata kama kuna mifumo nayo itakuwa nzuri sana. Vilevile yale malipo zile tozo tozo, ada, malipo kwa mtu anayetaka kusajili biashara yake mimi ningeshauri vingeondolewa na zile gharama kwa mtu anayeanza biashara kwa mara ya kwanza kumwambia nenda *TRA* kachukue *tin number* kabla hajaanza biashara anaambiwa

akalipe kodi ya makadirio vitu kama hivi vinakwamisha watu wengi sana katika kuingia kwenye mfumo rasmi wa biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungetafuta namna fulani ikiwezekana hivi vitu, mtu akitaka kuanza biashara mara ya kwanza asilazimike kuanza kulipa mapato, aruhusiwe aanze, aingizwe kwenye mfumo na baadaye jinsi anavyozidi kufanya biashara tutajikuta tumesajili watu wengi sana kwenye mfumo wa kulipa kodi, kwa hiyo tutapunguza watu kwenye sekta isiyo rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna maeneo mengine ambayo tunaweza tukayaangalia, kwa mfano watu kama *TBS*, watu kama *BRELA* wangeongeza ofisi zao mpaka huko Mikoani, sijui wale kwa ajili ya kusajili jina la biashara, unakuta watu wengi wanafanya biashara zisizo rasmi. Maeneo haya tukiyaangalia tukarasimisha biashara, tukapima ardhi ya nchi hii vya kutosha na kusajili kwenye mifumo, tunaongeza sana wigo wa walipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika ile kodi ya majengo watu wa Vyuo Vikuu vya Ardhi kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi na Halmashauri wana teknolojia ile wanaweza wakaenda kwa kutumia mfumo ya *GIS* wakasajili nyumba zote kwenye mifumo na wakazifanyia uthamini watu wakalipa kodi kulingana na thamani ya jengo ile itasimamia hata haki na itawewezesha watu wengi zaidi kulipa kodi bila usumbufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa ulipaji uwe rahisi kuwa kuna kodi nyingi huko ambazo zinaweza zikaongeza mapato ya Serikali, tukifanya haya naamini tutaongeza wigo wa kodi kwa kiwango kikubwa sana, hata mimi Mheshimiwa Mbunge wa Ludewa nikija nikasema barabara zangu zimeharibika sana na mvua itakuwa ni rahisi kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuweza kutoa fedha kwa ajili ya matengezo ya dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka Ludewa kwenda Ibumi kule kumeathirika sana, daraja la Mto ketewaka lilikatika pale, Mlima Kimelembe ardhi iliporomoka sana, hata tunavyoomba fedha sisi

Wabunge wakati mwingine unakutana na mtihani. Mkandarasi wa kutoka pale Itoni kwenda Lusitu ninavyomwambia Mheshimiwa Bashungwa kwamba ameondoka *site* wa sababu ya changamoto ya malipo inakuwa ni rahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwetu Njombe muda wa kufanya kazi ni mfupi sana kutokana na kuwa na kipindi kirefu cha mvua, sasa wananchi wanaomba msimu huu ambapo mvua zimekata zitarejea mwezi Oktoba wakandarasi wasikutane na vikwazo vya malipo. Huu ndiyo muda wao ambao wanaweza wakafanya kazi vizuri na kukamilisha ile miradi ya ujenzi ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana eneo hili liweze kutatuliwa ili lisiathiri shughuli za wananchi. Kuna muda kama mwezi mkandarasi haonekani barabarani na anazungumzia ana changamoto ya malipo. Hali kadhalika zile barabara za *TARURA* na zenyewe tunaomba ziweze kupewa fedha haraka ili msimu huu ambapo wanaweza wakafanya kazi wafanye kazi ili kukuza uchumi wa wananchi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, ni kengele ya kwanza?

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *ok* kama ni kengele ya pili niseme naunga mkono hoja kwa asilimia 100, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Kamonga. Nilimtaja Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, Mheshimiwa *Engineer* Ezra na Mheshimiwa Robert Chacha Maboto ajiandae. Mheshimiwa Jacqueline, Mheshimiwa *Engineer* Ezra hayupo pia Mheshimiwa Robert Chacha Maboto.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata fursa jioni hii ya leo ili niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa fursa hii jioni hii ya leo kwa kuniwezesha kunipa afya ili na mimi niweze kusema machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili napenda nimshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya katika Jimbo letu la Bunda Mjini ambapo tumepata miradi mbalimbali kwa ajili ya wananchi wetu. Tumepata vituo vya afya, tumepata zahanati, tumepata barabara za mitaa na mradi mkubwa wa *TACTIC* ambao wananchi wa Jimbo la Bunda Mjini wanausubiri kwa hamu kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendelea kufanya mambo makubwa katika Taifa letu. Sisi kama Wabunge tumeendelea kushuhudia mipango mikubwa ambayo imeendelea kufanywa na Serikali yetu kama vile ambavyo ameendelea kukamilisha miradi mikubwa ya kimkakati ambayo inajengwa na Taifa ambayo sisi kama Waheshimiwa Wabunge tunaishuhudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kushauri Wizara ya Fedha. Mimi pamoja na nafasi yangu ya Ubunge lakini mimi ni mfanyabiashara na biashara zangu nimefanya hapa hapa nchini pamoja na changamoto zote kubwa zilizopo. Napenda kumshauri pia Mheshimiwa Waziri kwamba nchi yetu ina vyanzo vingi sana vya mapato na hasa mamlaka kubwa ambayo imepewa nguvu za kusimamia ukusanyaji wa kodi katika Taifa hili ni Mamlaka ya Mapato Tanzania - *TRA*. Hawa kabla ya kufanya kazi hii naamini kuna mafunzo mbalimbali ambayo wanayapitia yanawafanya waweze kuelewa ni namna gani wanaweza kuwa-*handle* wafanyabiashara, lakini hizi mamlaka zingine za halmashauri zinakuwa ni tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo unaenda kwenye Halmashauri au mtu wa Halmashauri anakuja kwenye duka la mfanyabiashara ni mkusanya taka tu, amechukua *tender* ya ukusanyaji taka katika Halmashauri ile lakini huyo mkandarasi ambaye amechukua *tender* katika Halmashauri hiyo, anaweza kuwa na uwezo wa kwenda kufunga biashara ya mfanyabiashara kwa sababu tu ya kutokulipa hela ya taka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saa zingine huyo mfanyabiashara anayefungiwa biashara yake kwa sababu ya kutokulipa fedha za taka katika biashara yake haoni ni sehemu gani ambayo anazalisha takataka, lakini tu kwa sababu sheria zinatutaka kulipa yule mtu analipa, lakini unakuta hao watu wanakwenda wanafunga biashara za wafanyabiashara. Kwa mfano, *service levy, service levy* saa zingine taasisi inataka kulipa *service levy* inaomba *control number* kwa Maafisa Biashara lakini kutoa ile *control number* inawachukua muda mrefu sana, saa zingine hata miezi mitatu saa zingine mpaka wafanyabiashara wanaamua kujitengenezea wao wenyewe *control number* zao ili walipe fedha zile za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu nje na hapo yale madeni yanachukua muda mrefu na unapokuja kuletewa hesabu unakuta madeni yale yamekuwa makubwa. Mheshimiwa Waziri kwa sababu leo mpango huu tunaoujadili hapa ndiyo utakaofanya bajeti zingine zote za Wizara zote tulizozijadili na kuzipitisha ziweze kutekelezeka, zitatekelezeka baada ya kuwa tumepata makusanyo ambayo yanaridhisha au katika kiwango kile ambacho Serikali imejipangia kwa mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri usipotengeneza miundombinu mizuri kwa wafanyabiashara wako wa Taifa lako, utawafanya namna ya kukusanya kodi katika Taifa hili itakuwa ni kazi moja ngumu. Kuna mlolongo mwingi sana wa tozo na kodi mbalimbali, kwa mfano kuna *service levy*, kuna ushuru wa mabango, na huu ushuru wa mabango Mheshimiwa Waziri hapo nyuma umekuwa umepelekwa *TRA* na *TRA* walikuwa wanakusanya vizuri zaidi hata kuliko hivi ilivyo sasa, kwa sababu

*TRA* walikuwa wanajua namna gani ya kuweza kukusanya kodi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na huo ushuru wa ada ya taka, zimamoto, *OSHA*, leseni, kodi ya zuio, kodi ya mapato ile ambayo saa zingine mfanyabiashara anakuja kupigiwa hesabu baada ya kukamilisha mwaka hesabu ya mwisho anatozwa ile ya asilimia 30 ya faidi aliyoipata kwa mwaka. Hizi kodi zote Mheshimiwa Waziri karibia zipo zaidi ya 10 hapa ninavyoziona, hizi kodi ingewezekana zingetafutwa zile kodi ambazo zinaweza kubebana Pamoja, zikawekwa pamoja halafu zikakusanywa kwa sehemu moja kuliko kuwa na mlolongo mwingi wa kodi nyingi ambazo zinakuwa kero kwa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara ndiyo zao letu tunalolitegemea kama Serikali ili wafanyebiashara tuweze kukusanya kodi kutoka kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kuna hili jambo la faini la shilingi milioni 15,000,000 kwa mfanyabiashara yule atakayeuza halafu akashindwa kutoa risiti, aidha mnunuzi yle aliyenunua bidhaa kutoka dukani halafu akashindwa kuomba risiti akikutwa hapo mlangoni apigwe faini milioni 15. Lakini ukiangalia mazingira ya wafanyabiashara wetu katika Taifa letu ni mazingira magumu, halafu na mitaji yenyewe hawana na mitaji yenyewe waliyonayo hiyo kidogo wameikopa benki. Sasa leo ukikuta mtu ameenda dukani saa zingine akakuta mtandao haupo hata namna ya kutoa risiti haiwezekani, halafu akaondoka bila risiti akakutwa hapo mlangoni, akapigwa faini ya shilingi milioni 15, huku kibanda chake cha biashara kina mtaji wa shilingi milioni mbili, hili jambo naamini kwamba Waziri pamoja na Serikali ni vizuri mkaliangalia kwa sababu hili likipelekwa kwa wananchi na wafanyabiashara wetu walio wengi wao watashindwa, kwa sababu utakuwa unampiga faini ya shilingi milioni 15 inayozidi uwezo biashara yake anayoisimamia jambo ambalo kwa hali ya kawaida tu halitawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningeiomba Wizara ya Fedha jambo hili ilirudie vizuri kulitizama nje ya hapo wafanyabiashara

walio wengi watapigwa faini halafu tutakuja hapa Serikali itakuwa inataja madeni mengi na makubwa ambayo inawadai watu na wale watu uwezo wa kuyalipa yale madeni hawana. Mimi nikafikiri ni vizuri tukawadai watu madeni ambayo wanao uwezo pia wa kuyalipa, tunadai matrilioni ya matrilioni ya shilingi kwa wafanyabiashara ambazo ni kodi ambazo wamekusanya saa nyingine halafu wameshindwa kuzipeleka Serikalini lakini uwezo saa zingine mtu tunamdai labda miaka mitano au tunafanya naye kesi miaka mitano, inaisha miaka mitano uwezo wa kulipa zile fedha hana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni la wananchi wangu wa Kata ya Nyatwali ambao wamefanyiwa tathmini kwenye maeneo yao toka mwaka jana na mpaka leo wanasubiri fidia ya kulipwa fedha zao, ili waondoke kwenye yale maeneo. Mheshimiwa Waziri unaelewa wale wananchi walikuwa hawana mpango wa kuhama kutoka kwenye lile eneo, isipokuwa Serikali imelitaka kwa manufaa makubwa zaidi na wananchi wale wamekubali na sasa wanachosubiri ni malipo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hii leo tunavyozungumza hapa wananchi wa Kata ya Nyatwali wanataka kusikia kauli yako juu ya malipo yao, ni lini watalipwa fedha hizi kwa sababu, sasa hivi pale wanapoishi, wanaishi katika adha kubwa. Wamepata mafuriko pale kipindi cha masika, nyumba zimeanguka, zimeezuliwa na upepo, lakini namna ya kuzirudisha zile nyumba haiwezekani kwa sababu, tayari walishafanyiwa tathmini wakamaliza kwa hiyo, wapo njia panda, wapo katikati hawajui waende mbele, hawajui warudi nyuma. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, nakuomba utakapokuwa unakuja kuhitimisha bajeti yako hapa kwenye Wizara hii ya Fedha uwaambie wananchi wa Kata ya Nyatwali kwamba, zile fedha zao wanalipwa lini kwa sababu, muda wote akili zao zote zinategemea kupata kauli yako, ili wao waweze kujua wanaanzia wapi wanamalizia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, tunaendelea na Mheshimiwa Muharami Mkenge.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya. Hakika kila mwaka tunashuhudia bajeti ya Serikali ikipanda, hii ni kutokana na sekta nyingi zilizomo katika nchi kupatiwa pesa nyingi, kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Waziri wa Mipango, Naibu Waziri Mheshimiwa Chande na wafanyakazi wote wa Wizara kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. Mimi napenda sana leo nijielekeze katika kutoa pongezi kwa mafanikio yaliyopatikana katika Serikali hii kwa bajeti ya Mwaka 2023/2024 pamoja na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nikianza kwa upande wa Kilimo. Tunaishukuru Serikali, kwenye bajeti iliyopita miradi mingi ya kilimo imefanyika na tumeona kabisa wameongeza ukubwa wa karibu hekta 543,306 zenye thamani ya shilingi trilioni moja na kuanza ujenzi wa mabwawa 14. Haya ni mafanikio makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya afya Serikali imejitahidi kiasi cha kutosha na kwa kweli, tunajivunia, hakuna sehemu yoyote katika nchi hii ambayo imekosa mradi wa afya. Mimi mwenyewe binafsi pale kwangu Bagamoyo nimepatiwa pesa karibu shilingi milioni 900, kwa ajili ya ukarabati wa hospitali kongwe ya Bagamoyo ambayo ipo toka Mwaka 1957. Haya ni mafanikio makubwa sana ya Serikali yetu. Vile vile, nimepatiwa pesa karibu shilingi milioni 300, kwa ajili ya jengo jipya la *EMD* pamoja na vifaa tiba ambavyo vimeletwa. Kwa kweli, mambo ni mazuri katika sekta ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya elimu, halikadhalika, mafanikio ni makubwa sana. Mimi kwa kipindi kifupi nimekuwa

Mbunge wa Bagamoyo, lakini kuna shule karibu nne mpya za sekondari. Haya ni mafanikio makubwa sana kwa Serikali. Shule za msingi karibu tano mpya kwa hiyo, Serikali inajitahidi sana katika kutumia bajeti yake katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya mawasiliano. Naishukuru Serikali, sasahivi sehemu nyingi ambako kulikuwa hakuna mitandao, mitandao inafanya kazi. Hata wanavijiji wenzangu kutoka sehemu za Makurunge, Fukayosi na Kijiji cha Mkenge walikuwa na tatizo kubwa la miundombinu, sasahivi wanapata mtandao kama kawaida. Haya ni mafanikio makubwa sana ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi labda nirudi katika Bajeti ya Mwaka huu 2024/2025. Naipongeza Serikali kwa bajeti kubwa ambayo inakadiriwa kuwa karibu shilingi trilioni 49, lakini kuna mambo mengi mazuri. Kwa kweli, wananchi wameifurahia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mimi nataka nizungumzie mkakati wa kuongeza kodi ya mapato ambao Serikali wameuonesha. Kuna Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya Mapato, Sura Namba 438, ambayo wenzangu wote wameizungumzia na sio vibaya tukairudia kwa kuona kwamba, hili jambo kwa kweli, bado halijakaa vizuri. Sura Namba 438, Kifungu 86(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi kimesema kwa kuweka ukomo wa faini ya juu ya kosa la kutokutoa risiti kwa kiasi cha *currency* 1,000 sawa na shilingi milioni 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kwa Watanzania, mimi nafikiri Watanzania wengi watafunga maduka yao, biashara zao nyingi zitafungwa. Leo hii mwananchi anayetoka katika Kijiji cha Mkenge, ambaye hajui maana ya hii *EFD* risiti anaweza akaenda katika duka akakamatwa kwamba, kwa nini hakuchukua risiti na mwenye duka akakamatwa. Hii naona kwamba, Mheshimiwa Waziri, hebu jaribuni kuiangalia kwa kweli, bado tunahitaji ukusanyaji wa kodi ufanyike, lakini kwa faini kama hizi sidhani kama kutakuwa na afya katika jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nishauri kitu kimoja katika suala la ukusanyaji wa kodi. Kwa kweli, suala la ukusanyaji wa kodi ni suala la muhimu sana katika nchi. Ninaiomba sana Serikali, sasahivi kifike kipindi Mameneja wa *TRA* katika Mikoa yote wawe walimu wa masomo ya kodi katika shule za msingi na shule za sekondari, ili kizazi chetu kione umuhimu wa kulipa kodi. Sasa hivi watu wengi tuliopo hatuoni umuhimu wa kulipa kodi, vizazi vyetu tusivirithishe hii hali ya kutokulipa kodi. Itolewe elimu maalum kwa wanafunzi wa shule za msingi na shule za sekondari, waambiwe umuhimu wa kulipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanafunzi aambiwe kabisa hili darasa unalosoma ni kodi ya Serikali. Haya madawati unayokalia haya ni kodi ya Serikali. Kwa hiyo, itafutwe njia yoyote ya kutoa elimu kwa vizazi vyetu vya chini, ili huko badae tusijetukapata tabu ya kulalamika katika ukusanyaji wa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa mapendekezo yake. Ninampongeza katika Sura Namba 148, Kipengele cha 18, kuliondolea na kulipa msamaha wa kodi Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania, ili liweze kufanya majukumu yake vizuri. Mheshimiwa Waziri, kwa hili nakupongeza sana. Kwa kweli, ilikuwa ni changamoto na janga kubwa, watu walikuwa wakihangaika kutoa vifaa vyao bila mafanikio. Ninakupongeza sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine ambalo nataka kuligusia hapa. Katika Sheria ya Sukari, Namba Sita. Hapa wanazungumza kwamba, *NFRA* kununua sukari, kuwezesha Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* kununu sukari, kuratibu na kuhifadhi pengo la sukari kwenye hifadhi ya chakula ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka niseme kitu kimoja. Kama sikosei mwaka jana au mwaka juzi kuliletwa hoja binafsi hapa Bungeni kwamba, *NFRA* imeshindwa kununua mahindi ya wananchi, ilikuwa haina pesa kabisa. Mheshimiwa Rais akaingilia kati, pesa zikatolewa, mahindi yakanunuliwa. Leo hii mnataka kuipa mzigo tena *NFRA* wa kuingia katika kununua na kuhifadhi

sukari, hii pesa inatoka wapi? Ni wapi *NFRA* wanaipata wakati mahindi ya wakulima bado hayajapata soko? Kwa nini kwanza wasiingie katika mahindi halafu badae huko, kama mambo yao ya kipato yakiwa mazuri au bajeti yao ikiwa nzuri, ndio waingie katika kununua sukari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa mimi naona kidogo kama kuna changamoto ambayo itakuja kujitokeza mbele ya safari. *NFRA* wakipewa mamlaka ya kununua sukari inawezekana wakatokea watu wakaenda wakapata vibali kwa jina la *NFRA* na wakaenda kununua sukari ikaja kuwa *disturbance* kubwa kwa wazalishaji wetu wa sukari hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napenda kuchukua nafasi kuongea kwamba, hapa pana tatizo kidogo, hebu tuliangalie vizuri kwa sababu, haiwezekani wazungumze kwamba, wazalishaji wa sukari wanaficha sukari kwa hiyo, *NFRA* wanunue sukari, ili kuwadhibiti. Hii sio sahihi kwa sababu, mzalishaji wa sukari hafichi sukari, bali anayeficha sukari ni *distributor* anayeuza sukari. Hivi mpaka leo Serikali imeshindwa kuhakikisha kwamba, inawadhibiti hao wanaoficha sukari katika maghala mpaka wachukue maamuzi kwamba, *NFRA* ndio wanunue sukari? Mimi naona kweli, hii haijakaa sawa, kama wameshindwa kununua mahindi wataweza kununua sukari kweli? Hapa ni kuingiza Serikali katika mtihani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine katika hicho kipengele cha pili, kutoza shilingi hamsini kwa kilo ya mabaki ya uzalishaji wa sukari *(by product)*. Mimi hapa ninapenda nipate ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, sukari ina *by product* nyingi, sukari ina *molasses,* sukari ina *ethanol,* sukari inatoa *by product* ya *bagasse,* sasa ni kipi hapa ambacho mnakwenda kukichaji shilingi hamsini katika hii *by product?* Tunataka kukijua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *otherwise* mkisema mnachaji *by product* zote kwa shilingi hamsini kwa kilo, hii itasababisha matatizo kwa wafanyabiashara, itasababisha matatizo kwa wenye viwanda. Leo, kesho na keshokutwa wenye viwanda watashindwa kuwalipa wafanyakazi mishahara vizuri kwa sababu

tu kodi zimeongezeka. Hebu iangaliwe kwa sababu, kitu kama *bagasse* ambayo inazalishwa tani nyingi sana katika uzalishaji wa sukari haitumiki sana. Kitu kama *molasses* soko lake sio kubwa sana, labda hapa muangalie ni kitu gani katika hivi mtakwenda kuchaji shilingi hamsini kwa kilo, lakini sio kwenda kuchaji shilingi hamsini *by product* zote ambazo zinaweza kuzalishwa katika sukari. Mheshimiwa Waziri, hii haijakaa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, napenda kuishukuru Serikali kwa kazi kubwa inayoifanya. Mheshimiwa Waziri pale kwangu Bagamoyo pana bandari ambayo inakusanya pesa nyingi, inakusanya mapato mengi kwa Serikali, lakini Bandari ya Bagamoyo imesahaulika sana. Hakuna kinachoendelea kwa maana ya ujenzi, hakuna kinachoendelea kwa maana ya miundombinu, kila mwaka bajeti inapangwa, lakini bado hali haijakaa sawa. Hebu ikumbuke ile bandari ijengwe vizuri, ili iweze kuinua kipato kwa Serikali kwa sababu, inakusanya mapato mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ukienda pale Meneja wa *TRA* anakaa katika kontena. Meneja wa *TRA* ambaye pengine anakusanya karibu shilingi bilioni mbili kwa mwezi anakaa katika kontena kwa kweli, hali hii haipendezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuweka mkakati au mpango wa kuja kujenga bandari ya uvuvi Bagamoyo. Hiyo nimeiona katika bajeti na katika mipango, lakini sasa nataka niseme kitu kimoja, Bagamoyo kuna chuo cha uvuvi pale Mbegani. Kile chuo kina hatihati ya kuondolewa kutokana na kuchukuliwa kwa bandari, lakini chuo kile kinatakiwa kiwepo Bagamoyo, ili kwenda sambamba na hiyo bandari ya uvuvi ambayo inatarajiwa kujengwa. Chuo kile bado kina eneo la karibu ekari 400 ambazo zipo pale, hazina kazi kwa hiyo, Serikali ifikirie itakapoamua kujenga Bandari ya Uvuvi Bagamoyo, basi na chuo kile kiendelee kuwa palepale, kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa vijana wetu, ili waweze kuingia katika sekta ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii kuwapongeza tena Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri

na Wizara yote kwa ujumla kwa kazi kubwa wanayoifanya. Pia, ninampongeza Mheshimiwa Rais anatupambania sana, majimbo yetu mengi yako vizuri, miradi mingi ya maendeleo ipo, hatuna shaka kabisa na tunamwombea kila la heri. Mheshimiwa Rais, bajeti ya Mwaka 2025 tutakuwa tumefanya mambo makubwa zaidi kuliko hapa tulipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Muharami. Tunaendelea na Mheshimiwa Elibariki Kingu, atafuatia Mheshimiwa Ahmed Shabiby.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa mmoja wa wachangiaji jioni, lakini kabla sijaanza mchango wangu ambao nitauelekeza katika maeneo makubwa matatu, kama ushauri kwa Serikali na kama maoni yangu nikiwa kama Mbunge muwakilishi kabisa wa wananchi wa Singida Magharibi, ukweli lazima tuuseme. Umuhimu wa kusema ukweli ni kuweza kulisaidia Taifa liweze kuwa na mtazamo ambao ni sahihi kutoka mtazamo ambao sio sahihi ambao unaweza ukajengwa katika mazingira tu ya kijamii, kiuchumi ama mazingira mengine ya kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezunguka Nchi ya Kenya kwa mwaka huu, nimekwenda Uganda na nimekwenda Rwanda. Nataka niseme kwa dhati ya moyo wangu kwamba, *standard* za kuulinda uchumi wa Tanzania zinazofanywa kwa makusudi na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Waziri wake wa Fedha, kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, kama hautembei unaweza usielewe haya ninayoyasema. *Standard* za kuulinda uchumi kwa Afrika Mashariki kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, wewe na Serikali yako na Rais wetu mnalitendea haki sana Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia jambo zima la *inflation* toka dunia imetoka katika misukosuko ya *Covid-19,* angalia *inflation* katika Nchi ya Rwanda, angalia *inflation* katika Nchi ya

Uganda na Kenya kwa *statistics*. Tanzania tunafanya *the best* katika ukanda wa Afrika Mashariki na ukanda wa Nchi za *SADC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati ya moyo wangu na mimi niko *proud* na Waziri wa Fedha. Kwanza huenda kwa sababu tu nitasema, mtasema huyu anamsemea kwa sababu ni ndugu yake wa Singida. Mimi nazunguka duniani, mmenipa nafasi ya kuwa mwakilishi kwenye Bunge la Dunia, ninazunguka dunia yote. Viwango vya namna uchumi wa Tanzania unavyokwenda Mheshimiwa Waziri shikamoo, unajitahidi sana kaka yangu kuliweka Taifa katika misingi ambayo imewapunguzia *economic shock* Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia baadhi ya wachangiaji wamezungumza wamesema…

**MBUNGE FULANI:** Eti, rudia.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ananiambia nirudie. Nimesema kwamba, juhudi ambazo zinafanywa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Wizara hii ya Fedha imesababisha kupunguza *economic shock* kubwa ambayo ingeweza kuleta *frustration* kwenye nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza wachangiaji, kaka yangu ametoka kuchangia hivi karibuni, hii *Finance Bill* mnayoileta mwaka huu, nawaambia mimi nitakuwa Mbunge wa kwanza kuiunga mkono kwa sababu kubwa zifuatazo, haiwezekani kama Taifa tukawa tumewapa *monopoly* watu wachache kuagiza sukari. Wamepewa *monopoly* na Serikali kuagiza sukari na wamepewa *incentive,* mimi ni muumini mzuri sana wa viwanda na sina maana kwamba, viwanda vyetu vya sukari vinafanya vibaya, lakini wanafanya vitu ambavyo vina-*abuse* soko na kumuumiza mlaji wa mwisho, ambaye ni mwananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya, nikupe mfano mdogo. Mwaka jana Wizara ya Kilimo ime-*analyze gape* la sukari kwenye nchi wakapata tani 60,000. Wakawaita wenye viwanda

wakakaanao chini wakawaambia agizeni hii sukari. Nakwambia Mheshimiwa Waziri kama sio makusudi viwanda vyote vya sukari viligoma kuleta sukari nchini, *why should be like this?* Hivi kweli tuingie gharama ya kuwapa mzigo watanzania walaji wa mwisho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sukari ilifika mpaka shilingi 7,000. Mheshimiwa Waziri, mimi leo nataka kusema harakisha, ikiwezekana mngekuwa mnaweza kurekebisha Kanuni, *Finance Bill* ije haraka, tutaipitisha kwa msimamo mmoja, Wabunge wote tutaipitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Taifa hatuwezi kuruhusu *monopoly* ya kuagiza sukari inafanywa na watu saba. Wakipewa vibali wanachukua wanakwenda kuviuza kwa watu kwa *expense* ya kuja kuwapa mzigo walipa kodi ambao ni raia wa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo jambo nikiwa kama Mbunge ninayetokana na Chama Cha Mapinduzi, Mbunge ambaye kazi yangu ni kuja Bungeni, kusimama na kuyasemea masilahi ya walipa kodi ambao wamekiamini Chama changu kilichopo madarakani kwa ajili ya kuwapigania katika *welfare* zao, hatuwezi kuruhusu jambo hili. Kwa hiyo nataka nimwambie Waziri wa Fedha pamoja na Watu wa Mipango, hiyo *Finance Bill* tutaipigia debe kwa sababu inagusa masilahi mazima ya walipa kodi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nalotaka kuishauri Serikali yangu; Hayo mengine sina lengo la kumwingilia Mheshimiwa Spika na Kamati yake, yako kwenye Kamati ya Maadili, Mheshimiwa Mpina amepelekwa kwenye Kamati ya Maadili, sitaki kuingilia. Hata hivyo, nachotaka kukuambia ni kwamba Serikali yoyote duniani itakapokosa kuwa na nguvu ya kuingilia soko inapoona raia wake wanafanyiwa makusudi na kuibiwa, Serikali hiyo inakosa *legacy* ya kuiongoza nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia na Serikali yake hawawezi kuona kuna wafanyabiashara wachache wanajipanga kuona bei sukari inafika shilingi 7,000 Rais akae

ametulia aseme kwamba; "Eeh, tunalinda viwanda vya ndani." Hata ingekuwa ni mimi nisingeruhusu hiyo hali. Jukumu la kwanza la Serikali yoyote iliyochaguliwa na wananchi ikaaminiwa jambo la kwanza ni kulinda *welfare* ya watu wake, hiyo ndiyo kazi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kuna hoja huku zimezungumzwa, mimi sina lengo la ku-*interfere* mambo ya Kamati. Unaposema kwamba Serikali imepata hasara ya shilingi bilioni 500, *where do you get these economic calculations*? Unazitoa wapi? Siku zote tunapoagiza *shortage* ya sukari na tunapoangalia *sugar gap* tunatoa *exemption* ya uagizaji wa sukari. Sasa hizo shilingi bilioni 500 zinatoka wapi? Hili kama siyo lengo la kutaka kuichonganisha Serikali na wananchi walioko nje waone kwamba Mama Samia ameshindwa kuisimamia Serikali anataka kuumiza wananchi. Haya mambo kwa Wabunge makini, tuliosoma kwa kodi za walipa kodi, tunaojua thamani ya Taifa letu *we will never allow them to happen over our dead body* kwenye Taifa letu, hatuwezi kukubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukachekeana, tukaoneana haya kwenye mambo, *when it comes* kwenye mambo yanayohusiana na masilahi ya Taifa letu tutailinda Serikali yetu kwa wivu na gharama kubwa kwa masilahi ya Watanzania. Hili nalisema wazi mchana kweupe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nilishauri kwenye bajeti ya Mheshimiwa Nape. Mheshimiwa Mwigulu nataka nikuongeze wigo wa kukusanya kodi. Tulizungumza na kaka yangu Mheshimiwa Sanga; tulisafiri na wewe kaka yangu kwenda Marekani, tulichojionea kwenye mataifa makubwa ambayo Watanzania siku zote mnatoa mifano; "Eti kwa nini Marekani wana barabara nzuri, kila kitu angalia Ulaya." *Those guys* wanalipa kodi. Lazima tujenge utamaduni wa watu kulipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kwenye Taifa letu mkiangalia kwenye *statistics*, zinaonesha wanaotubeba kwenye kulipa kodi ni watu wasiozidi 5,00,0000, Taifa lenye watu milioni 60 lakini nguvu kazi tuseme ni watu milioni 30, wangapi wanalipa kodi? Watu

hawalipi kodi. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu nakupa mfano mdogo na nataka nikuulize swali, ni madereva wangapi wanaoendesha *tax* mtaani mmewasajili kidigiti na mnjua hela wanzokusanya kwenye *tax*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo kuna taxi zinapaki *Airport*, kila siku natoka *airport* nashuka inanileta nyumbani na ninalipa shilingi 20,000. Nani analipa kodi kwenye ma-*tax* haya yanayoendeshwa barabarani? Nani analipa kodi kwenye majumba? Mimi mwenyewe nina nyumba zangu nimepangisha watu wanakaa, hata mimi nazungumza hapa sijawekewa mfumo na Serikali kuhusiana na hela ninazozipata kwa kulingana na kodi za nyumba zangu, kodi za Serikali zinakwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanadanganya, mtu ananunua kiwanja anauza, *value* imepanda anadanganya Serikali ameuza kiwanja shilingi milioni 200, ameiba zaidi ya shilingi milioni 160. Serikali haya mnashindwa kuya-*monitor*. Kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu nataka nikusaidie mawazo, *digitalize* uchumi wa Tanzania, ondoeni *cash economy*. Ninawambia *tax base* ya nchi itaongezeka, Serikali mtakusanya mapato. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, mtajenga uchumi wa kisasa utakaoweza kuwasaidia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ninaloshauri Serikali yangu. Kaka yangu Mheshimiwa Bashungwa unafanya kazi nzuri na kubwa katika Wizara yako. Wewe pamoja na timu ya watu wako tunakuona mpaka umekwenda kula chakula sijui kinaitwa mlonge, tukasema labda utamsahau Mama Alaska na utahamia kule lakini tunamshukuru Mungu ulirudi. Ninaomba nitoe ushauri kwa Wizara yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na changamoto ya ma-*engineer* kule kwenye mikoa. *Sometimes* unakuta mtu ambaye hana fani ya *engineer* anakwenda kusimamia barabara. Nakushauri kupitia bodi zako sijui *ERB* na akina nani, tengeneza *pool* ya vijana waliomaliza chuo kikuu ambao ni ma-*engineer* wawekeni kwenye *list* hakikisheni kila mkandarasi anayepata kazi kwenye Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anawachukua vijana

wasiopungua watano waliomaliza vyuo vikuu wapate *skills*. Wakimaliza mradi kwanza watapata kipato, pili mtakuwa mnatengeneza *technology transfer* kwa zile kampuni ngeni kwa vijana wa Kitanzania. Baada ya miaka mitano kampuni za wazawa wa Kitanzania zitakuwa na uwezo wa kuchukua *tender* kubwa. Mheshimiwa Bashunga ninalisema hili nikiwa na imani na wewe kama Waziri kijana unaweza ukalifanya kwa lengo la kusaidia nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho lakini siyo kwa umuhimu. Kaka yangu, Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, umepewa Wizara kwa muda mfupi umefanya kazi kubwa na ya kizalendo. Kwa mara ya kwanza nimepata muda wa kusoma mpango wote, hongera sana. Hivi ndivyo watu wa Singida wanavyofanya, hivi ndivyo Singida inavyotoa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi naweza kusema kwamba, kwa mpango huu na kwa miaka ijayo, alisema Mheshimiwa Askofu Gwajima watu wakafikiri anatania, jitahidini mipango tunayoipanga tui-*reinforce* kwa sheria ili kiongozi yeyote anayekuja kwenye Taifa letu apite kwenye njia ya mipango na maono ya Taifa kwa miaka 100 inayokuja. Tukiweza kufanya namna hii tutakuwa tumelijengea heshima Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo na kwa haya niliyoyasema kwa uimara wa uchumi wa Taifa letu, Rais wetu anavyohangaika kutafuta fedha huku na huko, ninakiri na kusema hadharani mchana kweupe kwamba Rais Mheshimiwa Dkt. Samia ameonesha uzalendo mkubwa, ujasiri mkubwa na nguvu kubwa kama mwanamke. Mimi Mbunge wake nasema Mitano tena kwa Mama, mwenye wivu ajinyonge. Mimi Mbunge wa wananchi ndiyo nimekwishasema sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Elibariki Kingu. Nilimtaja Mheshimiwa Ahmed Shabiby.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuwa mmoja wa wachangiaji kwenye bajeti kuu. Mimi nitanyoosha maelezo, sitosifu sana kwa sababu sitoki Singida. Tutazungumza yale ambayo yana ukweli. Ili Waziri wa Fedha na Waziri wa Uwekezaji muonekane mnafanya kazi ni lazima kazi yenu ionekane kwa wananchi. Kwa hiyo, siyo kwa sababu tuko CCM pekee humu basi tunasifiana sifiana tu hata kama vitu haviendi vizuri. Kama vitu vinakwenda vizuri tusifiane ndio ubinadamu na kama vitu vinakwenda vibaya tutaambiana ukweli. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu penda sana watu wanaokwambia ukweli kama sisi hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka leo nijikite kwanza kwenye barabara. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu naomba unisikilize vizuri sana. Mimi niko kwenye Kamati ya Miundombinu, kwenye Kamati ya Miundombinu barabara ambazo zimechoka Tanzania kongwe ni 71 ambazo muda wake umekwisha na sasa hivi ziko hoi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukua mfano tu Barabara ya Shinyanga - Mwanza, Lindi – Dar es Salaam, Njombe – Songea, Morogoro – Dodoma. Pia, chukua barabara za mijini na nyingi nyingi tu, barabara ziko hoi tu. Ukiangalia bajeti ambayo mmeipangia Wizara ya Ujenzi ni shilingi1,700,000,000,000 lakini madeni ni shilingi 1,200,000,000,000. Kwa hiyo, ina maana wao watabakia na shilingi bilioni 500, shilingi bilioni 500 itafanya kazi gani? Hamna chochote tunachotengeneza kwenye hizi barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutawalaumu hawa *TARURA* na *TANROADS* wao wanafanya kazi nzuri, na ni lazima tuwashukuru hawa ma-*MD* wa *TARURA* na *TANROADS* wanafanya kazi nzuri. Mheshimiwa Waziri, mimi hapa kama hii ndiyo bajeti na kama bajeti ya Ujenzi, bajeti ya *TARURA* hazitaongezewa pesa za barabara, mimi ndiyo nitakuwa wa kwanza kupinga bajeti. Chukua yale maoni tuliyokupa kutoka Kamati ya Miundombinu ya kuongeza vyanzo vya uhakika vya barabara, huo ndiyo ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sitaki kuzungungumzia habari ya sukari, sijui ya nani na nani kwa sababu ukichimba kote, hawa na hawa tukiongea hapa itakuwa balaa, bora tunyamaze lakini tujikite kwenye hizi barabara zetu. Mheshimiwa tafuta vyanzo vya uhakika, chukua ushauri wetu wa Kamati ya Miundombinu agalau tupate shilingi trilioni 2.2 kwenye *TANROADS* na tupate shilingi bilioni kama 400 kwenye *TARURA* ili Wabunge tukienda kule tuonekane tumefanya kazi ndugu zangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine mwaka 2022 ulisema Serikali inatumia zaidi ya shilingi bilioni 500 kwa ajili ya kuagiza magari ya Serikali Tanzania lakini bado najiuliza swali moja, hii Serikali ni tajiri sana au kuna shida gani? Umekuja ukalalamika na ukaleta mpango kwamba sasa hivi kwa kuondoa gharama hizo kila mtumishi atanunua gari lake ili alionee uchungu atalimiliki. Mwaka huu sijalisikia, sasa inaonekana na sijajua imekuja mpya au ile imeshindikana au vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha msingi mimi najiuliza hivi twende Halmashauri zote za Serikali za Mitaa, Manispaa zote, majiji yote na twende Serikalini kwenye Wizara zote haya magari mabovu mpaka yanaoza na mengine hayauziwi na yakiuzwa, wanajiuzia wenyewe. Hivi hii nchi ina utajiri wa kiasi gani kwamba haipigi mnada yale magari? Nani alishawahi kusikia hapa kwamba kuna gari la Serikali linauzwa kwenye minada? Haijawahi kutokea. Kwa hiyo, magari yote mnajiuzia wenyewe tena kwa *tender*. Unakuta gari ambalo lingepigwa mnada kwa shilingi milioni 70, shilingi milioni 80 utakuta limenunuliwa kwa milioni tano, milioni sita. Halafu tunazungumzia habari ya kwenda kuwaminya watu wadogo wadogo hawa huku chini wakati huku kuna pesa nyingine zimelala lala tu, hicho kitu hakiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, twendeni pale kwangu Gairo tu nina magari saba, ukienda hapa kwenye Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma huwa napitapita magari yako kibao. Ukienda manispaa zote yanauzwa vipi? Yanatakiwa yauzwe kwa mnada, tunaomba usimamie vitu kama hivyo. Mimi ukitekeleza hivyo na ukinijibu hivyo nitaunga mkono hoja yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni habari ya hii pesa. Hizi taasisi zenu za Serikali mnakwenda mpaka huko mnazisifu kwamba fulani wameweka gawio bilioni tatu, Bandari wameleta shilingi bilioni nne, *EWURA* shilingi bilioni tatu halafu mnashangilia kweli sasa hivi taasisi zetu… Haya *National Housing* bilioni ngapi wakati ina madeni kibao? Sijui nani ana bilioni ngapi. Sasa mimi najiuliza swali hivi sasa hivi kila taasisi imekuwa *TRA*? Yaani sasa hivi hatuna *TRA*. Pamoja na kuwa Serikali inategemea *TRA* kukusanya kodi na kufanya maendeleo ya nchi lakini sasa hivi kila taasisi ya Serikali ikianzishwa inakuwa *TRA*. Ikianzisgwa sijui *EWURA* inakuwa *TRA,* ikianzishwa *LATRA* inakuwa *TRA,* ikianzishwa Bandari inakuwa *TRA, OSHA* nayo *TRA* yaani kila mtu anakuwa *TRA*. Ukienda kule *TANAPA* nayo imekuwa *TRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nafikiri ule mpango wa awamu ya tano ulikuwa siyo mbaya wa kuchukua zile pesa zote halafu wao waandike bajeti kwamba sisi ni taasisi fulani bajeti yetu ya mwaka ni hii. Ninyi *BOT* mnachotakiwa kufanya ni kuwafungulia akaunti tu iwe *single treasury account*. Wafungue *single treasury account* ili pesa zote wanazokusanya ziingie kwenye akaunti kuu ya Serikali halafu wao wanakuwa na bajeti na ninyi msiwache kuwapelekea. Halafu zinazobaki kwa mwaka ndiyo gawio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ikibaki labda kwenye taasisi fulani imekusanya shilingi bilioni 100 lakini bajeti yao ilikuwa ni shilingi bilioni 50 maana yake pale tayari kuna shilingi bilioni 50 zetu. Sasa mnawaachia wao wanapanga, wanatengeneza, wanatunga na wanatandika (wanazila) zile pesa halafu zikija huku mnashangilia vihela vidogovidogo. Mnapewa vihela vidogo, aah, hii taasisi inajiendesha na ina gawio shilingi bilioni tatu. Hivi kweli bilioni tatu kwenye taasisi zinazokusanya pesa namna hii, halafu tunakuja hapa tunakuwa washangiliaji. Mimi siwezi kuwa mtu wa kushangilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndiyo ukweli na ukiona Wabunge wametulia namna hii ujue wanasikiliza kwa makini, hii inawangia, ndiyo ukweli. Kwa hiyo, nilikuwa nakuomba Mheshimiwa na nakuona hata unavyopata taabu. Juzi hapa

nilikuona unapata taabu sana ya kutafuta pesa lakini kuna baadhi ya taasisi zako zilikuwa zinakupinga, hiyo mimi ninaijua lakini ukiwa Waziri wa Fedha unatakiwa uwe ngangari. Kama umeshindwa kuwa ngangari unatakiwa uachie nafasi ili hata mimi nije nikae hapo. Mheshimiwa Waziri uwe ngangari, unafanya kazi nzuri lakini kuwa ngangarti kwenye hivi vitu. kila mtu akitaka achukue pesa na Mheshimiwa Waziri hapo ukitaka kuwa mzuri kwa kila taasisi hiyo kazi haiwezekani. Nchi imefikia mahali sasa hivi na lazima tuseme ukweli, wapigaji wamekuwa wengi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapigaji ni wengi na wengine utasikia tu Mama anaupiga mwingi. Siyo anaupiga mwingi kwamba anamsifia kwenye moyo, hapana anaupiga mwingi yeye anaiba hela. Anatandika pesa halafu akija huku anajifanya anasifia. Hata wewe Waziri wa Fedha na taasisi yako ya Mamlaka ya *TRA* nyie ndio mnaopata taabu. Ninyi lazima mkusanye kodi, mzilete kwenye mishahara, lazima ninyi huku ndiyo mzipeleke kwenye maendeleo wakati ukiangalia kuna taasisi nyingine mkizichanganya zinakusanya nusu ya *TRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo sitaki kuongea mambo mengi. Nafikiri amenielewa na ndiyo maana ameweka mikono hivi najua hapo amenielewa. Ahsante sana kwa kunielewa naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ahmed Shabiby na huyo ndiyo mchangiaji wa mwisho kwa siku ya leo. Sasa nina tangazo moja la wageni ambao wamekuja Bungeni jioni hii.

Kwanza ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge: kuna wageni watano wa Mheshimiwa George Boniface Simbachawene ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambao ni wachungaji na viongozi wa madhehebu ya *TAG* na KKKT kutoka Kijiji cha Makuyuni Monduli huko Arusha. Karibuni sana Wachungaji na viongozi wetu. *(Makofi)*

Tuna wageni 110 wa Mheshimiwa wa Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu,

Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kutoka Taasisi ya Walimu Wanawake Tanzania (TAWAWATA). *(Makofi)*

Tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Aloyce Kamamba amba oni wapiga kura wake kutoka Kakonico Mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

Tuna wageni 45 wa Mheshimiwa Leah Komanya ambao ni Watendaji wa Kata na Vijiji kutoka Jimbo la Meatu Mkoa wa Simiyu, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni 21 wa Mheshimiwa Josephine Chagula ambao ni wanafunzi wanaosoma Udaktari kutoka Ifakara Mkoa wa Morogoro, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni 28 wa Mheshimiwa Japhet Hasunga, Wanakwaya ya *Baptist* Aman kutoka Vwawa Mkoa wa Songwe, naona hawakuingia.

Pia kuna wageni 35 wa Mheshimiwa Nicodemas Maganga amba oni Wenyeviti wa Kata wa CCM kutoka Mbogwe Mkoa wa Geita; Makatibu wa Kata wa CCM kutoka Mbogwe Mkoa wa Geita; na Askofu Simon Nkwabi Miyeye wa Kanisa la *Tanzania Church of God International* kutoka Kahama. Pia kuna wapiga kura wake wawili ambao ni Mwanajuma na mwenzake kutoka Mbogwe. *(Makofi)*

Pia tuna wageni 25 wa Wabunge wote wa Mkoa wa Kigomaambao ni Timu ya Mpira wa Miguu ya Wasichana ya *Kigoma Queens* na viongozi wao, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Tuna wanafunzi 50 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, Ndaki ya Mipango na Maendeleo ya Jamii, karibuni sana wanafunzi wetu kutoka huko chuo kikuu. *(Makofi)*

Wanafunzi 48 kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)* Kampasi ya Dodoma Ndaki ya Masijala na Kumbukumbu. Karibuni

sana wageni wetu wote katika Bunge letu kwa ujumla wenu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza shughuli zetu jioni ya leo kwa hiyo ninawatakia jioni njema na ninaahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 12.22 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 21 Juni, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*